KAULI YA QURAN NA KAULI ZA AHLI BAIT WA MTUME SAW KUHUSIANA VIPENZI VYA ALLAH

Mtunzi :*Sheikh Abdallah bin Jawaran*
Mfasiri:*Juma Yusuf Khamis*
Kimepitiwa na: *Ustadh Talib Juma Ali*

AFRICA MUSLIMS AGENCY

ZANZIBAR

ماقاله الثقلان في أولياء الرحمن – لغة سواحيلي

بسم الله الرحمن الرحيم

KWA JINA LA ALLAH MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

YALIYOMO

UTANGULIZI **7**

DIBAJI **9**

MLANGO WA KWANZA **10**

Maana ya neno Sahaba **10**

MLANGO WA PILI **16**

Sifa za Thaqalaini **16**

MLANGO WA TATU **36**

Vipi fitina baina ya Masahaba(r.a) ilizuka?: **36**

MLANGO WA NNE **49**

NJAMA DHIDI YA UISLAMU NA WAISLAMU **49**

MLANGO WA TANO **57**

MSIMAMO SAHIHI (WA HAKI) TOKA KWA MASAHABA **57**

WA NABII S.A.W **57**

MLANGO YA SITA **60**

Majina na ukwe baina ya Masahaba na Ahlil Bait (r.a) . **60**

MLANGO WA SABA **70**

SUALA NA JAWABU **70**

Neno la Mwisho **99**

UTANGULIZI

Hakika shukurani zote zimemthibitikia Allah Mola wa viumbe vyote na namsalia na kumsalimu aliyetumwa kuwa ni rehema, mwongozo na rehema na nuru kwa walimwengu wote na juu ya jamaa zake , mishumaa ya mwongozo na taa za kuangazia kiza, Masahaba wake, wachaji, wafikishaji wa Wahyi wa mbinguni.

Ama baada ya utangulizi huu;: ni neema ya Allah iliyokamilika na hisani yake ya kiwango cha juu kutupelekea Mtume miongoni mwa nafsi zetu, hima na lengo lake likiwa ni kututakasa na kututowa toka kwenye viza na kutupeleka kwenye mwangaza, kutoka kwenye matatizo na kutupeleka kwenye mafanikio ya duniani na akhera .

Baada ya kufariki dunia Mtume (S.A.W) bendera hii iliyobarikiwa baada yake ilibebwa na kundi lililokuja kutokana na uteuzi wa Ar Rah'maan (S.W),kwani alielewa yaliyomo kwenye nyoyo zao na kile kinachofanyiwa pupa na nafsi zao, hivyo akawateremshia uradhi na kuwapa msamaha .wake(S.W) .

Uradhi huu mkubwa na msamaha ulioenea kamwe haukuwahalalikia ila baada ya kubainika habari ya kundi hili lililotakasika na kusafika kwa hali na kauli zilizomfadhaisha adui kabla ya kipenzi, kama ilvyosemwa
'Kila chungu huivisha kile kilicho ndani yake" .

Lakini pamoja na kila walichokitowa na nafsi zao kuzitowa kamwe kundi la watu ima kwa kutoelewa uhakika wa Masahaba(r.a), au upya wao katika uislamu umefichua ufinyu wa elimu yao kwa Uislamu , na kutozama kwa imani yao kwenye dini ya Arrahmaan ,hivyo kundi likatanua elimu kuhusiana na Masahaba hao (r.a),na jengine kutoelewa likiongozwa na huruma kwa kujingikiwa na kinachoendelea nyuma ya kauli batili za

kihadaa, ili kung'oa nguzo ya Dini Tukufu kwa kufukua toka kwenye msingi wake, na kupigia mbio kung'oa mimea yake, na

hivyo ni kwa mbio za mwenye pupa kwenye njia ya kutisha, zingatia! Nako :ni kutia ila (Masahaba) wateule (r.a).

Vikurasa hivi kwa idhini ya Allah (S.W) ndani yake umo ubainifu wenye kutosheleza na ubainifu wa kundi hilo miongoni mwa wanaume na wanawake, kwani anaempenda mtu basi hupenda vipenzi vyake na kuvikubali vyema, na kuwachukia maadui zake na wanaomchukia, na huu ndio mwenendo wa viumbe asiokwenda kinyume nao ila asiekuwa wa kawaida au watu wa ajabu; kwani hakika sisi tunampenda kila aliempenda Nabii (S.A.W), na kufa akiwa radhi nae; kwani dini yetu muhimili na nguzo ya msingi wake ni mapenzi katika Allah (S.W) kwa vipenzi vyake, na kuchukia katika Allah (S.W) kwa maadui zake.

Na hata iwapo nimefanya mapungufu kwenye kuelezea upande huu, sababu yake ni kwamba ni jambo lililowazi linalojulikana halihitajii kubainshwa, na kauli ya kuwekwa kwake wazi hutia ugumu akili , kwani kilicho wazi hakizidishwi na uelezewaji wake isipokuwa ugumu na kutoeleweka, kama ilvyosemwa (Na akatafsiri maji kwa maji baada ya juhudi kubwa).

Na huu ndio uwaz,i iwapo sikukamilisha pande zake basi kamwe sitokosa nasaha toka kwa kipenzi mwenye kunasihi anielekeze kwenye usahihi na kunielekeza kwenye mantiki na jibu bora ,ili mguu uzame kwenye njia ya mapenzi kwa Nabii (S.A.W) , jamaa zake waliotoharika na Masahaba zake wateule(r.a) na awaghufirie.

DIBAJI

Wengi wa watu wamechanganyikiwa kwenye kutofautisha baina ya ufahamu wa usuhuba kwenye Lugha toka kwenye ufahamu wake wa kiistilahi, miongoni mwao ni:

1-Upungufu wa ufahamu na kuangalia kwao kwenye upande huu
2- Kutoelewa kwao upembanuzi wa hili kwani , bidhaa yao kwenye Lugha ni ndogo na yenye ubakhili .

Kwa sababu hizi mbili tunaona miguu yao imeteleza kwenye ufahamu sahihi, hivyo wakawanasibishia Masahaba (r.a) kauli na maneno batili ,na kuwasingizia nyingi za hatari kama vile unafiki, ridda na nyenginezo, wakitolea dalili juu ya hilo aya wasizoziewa maana yake, au karina na dalili, katika fahamu zao ngonjwa, na nadharia tasa, kwa kuokotaokota maneno yaliyotawanyika kwenye Hadithi Sahihi Mutawatiri, na toka hapo kuzifanyia taawili batili, zenye dalili ya ufinyu wa elimu na ubovu wa fahamu yao .Na kwa kutoelewa Lugha ya Kiarabu, ya kutolea dalili madai yao kwa riwaya dhaifu na uzushi zisizotihibiti usahihi wake toka kwa Nabii (S.A.W), wakazishikilia mshiko wa mwenyekughariki kamba batili za udhaifu wa mawazo jambo linaloashiria kutoelewa kwao, kutosoma, kutokua thabiti).Hivyo kabla kuingia kwenye kubainisha uadilifu wa Masahaba, ni vyema kubainisha jumla ya mambo muhimu kwenye maulizo yafuatayo :

- ***-Nini maana ya Sahaba ?***
- ***-Jee wanafiki ni katika Masahaba ?***
- ***-Jee waliortadi baada ya kifo cha Nabii (S.A.W) jina la Sahaba linawahusu.?***
- ***Ni zipi kauli za Ahlil Bait kuhusiana na wao?***
- ***-Kwanini pakatokea ugomvi na tofauti baina yao ikiwa Allah (S.W) amewaridhia***?

Maulizo na shubuhati tutayapatia majibu yake pale tutakaposoma kurasa hizi ambazo ni maalum kwa kuwa na kauli na ushahidi wa.. (Kitabu cha Allah na Ahlil Bait) kwenye uadilifu na cheo cha Masahaba (r.a) idhini ya Allah.katika milango ya kitabu hichi: Na ndani yake umo mkusanyiko wa mawazo ambayo hudhihiri kwenye akili za waislamu, na baada ya kusikia yale wanayosingiziwa Masahaba baadhi ya maulizo, udhibiti wa shubuhati uondowaji wa kughafilika kukilkoota kutu kwenye baadhi ya nyoyo za waislamu, tutawafikishwa baada ya hapo kwenye usahihi na haki inayoridhiwa na Allah (S.W) kwetu. kwa idhini yake.

MLANGO WA KWANZA:

Maana ya neno Sahaba

Ni lazima juu yetu kabla ya kuingia kwenye ubainishaji unaojulisha juu ya uadilifu wa Masahaba(r.a), kubainsha ufahamu wa neno (sahaba) kwa uwazi wa neno hili, ubainifu wa mipaka ya kuitwa kwake, nani mwenye kusifika nalo,na nani anaemaanishiwa neno hili tukufu –imo tawfiki ndani yake ya elimu na kusoma baadae, ubainifu huu hauwi ila kwa njia mbili za Kilugha na Kiistilahi.
Mwanzo ::Maana ya neno Sahaba katika Lugha .

Sahaba:limenasibishwa na Sahib ,nalo linayo maana kadha zenye kuzunguruka kwa ujmla wake kwenye kushikamana na ufuataji.[1]
Kabla ya kubainisha baadhi ya matumizi ya suhuba katika Lugha,inatupasa kuelewa kwamba baadhi ya matumizi haya kamwe hayatokani na kwenye ujumla wa maana ya kiistilahi,kwa vile ni kulingana na maana ya Kilugha yasiyodhibitiwa na udhibiti madhubuti kulingana na tutakavyoelewa, hivyo nimewajibikiwa kuleta jumla ya maana ya usuhuba wa kilugha ili kuhifadhi wakati wa kuitia neno hili na miongoni mwao ni:

1 Lisanul A'rab 1/519)

1-Suhuba -ya kimajazi :nalo huitiwa wawili ambao baina yao upo wasifu wa pamoja kwao, na inawezekana ikawa baina yao ni kipindi kirefu, kama ile kauli ya Mtume (S.A.W) kwa baadhi ya wake zake: "**Hakika nyie ni Sawahibu Yuusu f**" [2]

2- Suhuba idhw'aafiyyah –usuhuba wa kutegemezea :nao ni ule unaotegemezewa kwenye kitu kwa sababu ya kuwepo kinachoambatana nacho ,kama inavyosemwa :Sahibul Maal , Saahibul I'lmi …" yaani mwenye mali mwenye elimu….

3- Suhuba ya utekelezaji wa majukumu :Na hili ni kama ilivyokwenye kauli yake Taa'la:**{Nakamwe hatukuwafanya -As-habun Naar- wadhamini wa moto ila Malaika }**[Al Maaidah :3]

4- Suhuba ya kukutana:Huitiwa usuhuba kukutana baina ya wawili, angalau mara moja kwa sababu husika na ukakatika.Na huu ni kama ulivyokuja toka kwa Nabii (S A.W.) amesema :"Wauzianaji wako kwenye hiari pale ambapo bado hawajafarikiana au mmoja wao kumwambia mwenzake:"chagua… "[3]

(Hadithi), hivyo mnunuzi ameitwa mnunuzi (Sahib) pamoja na kwamba kukutana kumetokea mara moja, pamoja na kwamba muuzaji alinunuwa bidhaa toka kwake.

5- Suhubatul Mujaawarah: - Usuhuba wa ujirani- nao ni ule unaoitiwa mwenyekuamini ,kafiri na kinyume chake,nako ni kwenda samba samba na Kauli yake Taala:**{Akamwambia swahiba waka -mwenzake-nae akiwa ni jirani yake, hivi umemkufuru Yule amabe amekuumba toka kwenye udongo na tone la mbegu za uzazi na akakuumba vizuri ukawa mtu kamili** [Al Kahf:37]

Na kama ilivyo kwenye Kauli yake Taala:**{ Hivyo akamwambia Swahib mwenzake huku akimjadili ,mimi ni mwingi wa mali na mwenye nguvu zaidi kuliko wewe }**

2 Bih'aarul anwaar(28/137)

3 Musadrakul Wasaail :(19/327)

Inajuzu Suhuba kuitiwa kwa asiemuelewa mwenzake na hakukutana nae kamwe hata siku moja kama alivyosema Abdulr Rahman bin Auf (r.a) kwa vijana wawili wa Kiansari waliokuwa wakimtafuta Aba Jahl kwenye Vita vya Badri wakiwa wanataka kumuuwa kwa sababu ya kumtukana Nabii (S.A.W), hivyo akawambia "Huyu ndie sahib wenu ambaye munamuulizia "[4]

Kulingana na yaliyotajwa, matumizi ya maana ya suhuba haiwezi ikaenea na kutumika kwa yeyote na pahala popote, kwani lau Sahaba angejulikana kwa usuhuba wa kilugha kulingana na matumizi yaliyotangulia, sisi sote lau tugechukulia maana hizo basi mayahudi wanafiki, wakristo na washirikiana waliokutana na Nabii(S.A.W) wangelikuwa nao ni masahabkutokana na tamshi hilao
Ama baada ya utangulizi huo: Ni neema ya Allah iliyokamilika na hisani yake ya kiwango cha juu kutuletea Mtume miongoni mwa nafsi zetu, hima na lengo lake liwe ni kututakasa na kututowa toka kwenye kiza na kutupeleka kwenye mwangaza, kututowa kwenye matatizo na kutupeleka kwenye mafanikio ya duniani na Akhera .

Baada ya kufariki dunia Mtume (S.A.W), bendera hii iliyobarikiwa baada yake ilibebwa na kundi lililokuja kutokana na uteuzi wa Arrahmaan (S.W), kwani alielewa yaliyomo kwenye nyoyo zao na kile kinachofanyiwa pupa na nafsi za kwa hivyo akawateremshia uradhi na kuwapa msamaha .wake (S.W) .

Uradhi huu mkubwa na msamaha ulioenea kamwe haukuwahalalikia ila baada ya kubainika habari ya kundi hili lililotakasika na kusafika kwa hali na kauli zilizomfadhaisha adui kabla ya kipenzi ,kama ilvyosemwa (Kila chombo huivisha kile kilichopikwa ndani yake).

Lakini pamoja na kila walichokitowa na nafsi zao kuzitowa kamwe kundi la watu ima kwa kutoelewa au kutokana uhakika wa Masahaba (r.a), au upya wao katika uislamu umefichua ufinyu wa

3 Musadrakul Wasaail :(19/327)

4 Bih'aarul anwaar(28/137)

elimu yao kwa uislamu , na kutozama kwa imani yao kwenye dini ya Arrahmaan, hivyo kundi likatanua elimu kuhusiana na Masahaba hao(r.a),na jengine kujingikiwa likiongozwa na huruma kwa kutoelwa kinachoendelea nyuma ya kauli batili za kihadaa, ili kung'oa nguzo ya Dini Tukufu kwa kufukua toka kwenye msingi wake ,na kupigia mbio kung'oa mimea yake.,na hivyo ni kwa mbio za mwenye pupa kwenye njia ya kutisha, zingatia! Nako ni kutia ila (Masahaba) wateule (r.a).

Na vikurasa hivi kwa idhini ya Allah (S.W) umo ubainifu wenye kutosheleza na ubainifu wa kundi hilo miongoni mwa wanaume na wanawake, kwani anaempenda mtu basi hupenda vipenzi vyake na kuvikubali vyema, na kuwachukia maadui zake na wanaomchukia ,na huu ndio mwenendo wa viumbe asiokwenda kinyume nao ila asiekuwa wa kawaida au watu wa ajabu; kwani hakika sisi tunampenda kila aliempenda Nabii (S.A.W), na kufa kiwa radhi nae; kwani dini yetu muhimili na nguzo ya msingi wake ni mapenzi katika Allah (S.W) kwa vipenzi vyake ,na kuchukia katika Allah (S.W) kwa maadui zake.

Iwapo nimefanya mapungufu kwenye kuelezea upande huu, sababu yake ni kwamab liliwazi linalojulikana halihitajii kubainshwa, na kauli ya kuwekwa kwake wazi hutia ugumu akili, kwani kilicho wazi hakizidishwi na uelezewaji wake isipokuwa ugumu na kutoeleweka, kama ilvyosemwa (Na akatafsiri maji kwa maji baada ya juhudi kubwa).

Huu ndio uwazi iwapo sikukamilisha pande zake basi kamwe sitokosa nasaha toka ckwa kipenzi mwenye kunasihi anielekeze kwenye usahihi na kunielekeza kwenye mantiki na jibu bora ,ili mguu uzame kwenye njia ya mapenzi kwa Nabii (S.A.W) Nabii (S.A.W), jamaa zake waliotoharika na Masahaba zake wateule(r.a) na awaghufirie.

Tanbihi : Katika kisa cha kujikweza kwa Abdillahi bin Ubayya bin Saluul juu ya Nabii (S.A.W), Omar (r.a) aliomba kwa Nabii (S.A.W) ampe idhini amkate shingo yake ,akamwambia hapana :"muwache watu wasije wakasema kwamba Muha'ammad anauwa

Masahaba zake ”[5] Hivyo Nabii (S.A.W) katika alitaja usuhuba kwa mnafiki kwenye Hadithi hii lakini alikusudia matumizi ya Kilugha na sio ya Kiistilahi, na hii ni katika Balagha na hikma zake (S..A.W) ujuzi wake juu ya walivyozowea warabu kwenye Lugha yao,na kamwe hapakuwa na :

Kwanza :Hakika kuitiwa kilugha hakukusudii kutifautisha baina ya imani na unafiki ;kwani hakuna kidhibiti chochote kile.

Pili : Nabii (S.A.W) alieleza sababu ya kumzuwia Omar (r.a) asimuuwe mnafiki (Watu wasije wakasema ..Muhammad anaua masahaba zake…),na watu waliotajwa hapa ni kundi lililo dhidi ya Masahaba (r.a).,kwani Qur-anilipokuwa ikzungumza na watu wa imani ilikuwa ikiwahutubia kwa kauli yake **{Enyi ambao mumeamini }** [Al Baqarah : 153] na ilpokuwa ikelekeza kauli kwa makafiri au kwa ujumla wa watu waumini na makafiri wao ilikuwa ikwasemesha **{Enyi watu } [** Al Baqarah : 21]

Tatu Kwamba Nabii (S.A.W) Katika mambo yanayojulikana kiakili tu kwamba makafiri ndio watu wenye uadui mkubwa na pupa la kumtia kasoro Nabii (S.A.W) na Daawa yake, na hivyo pale Nabii (S.A.W) atakapomuuwa (Abdillahi bin Ubayya bin Saluul ,basi kamwe makafiri wasingesema kwamba ameuwa mnafiki ,bali watasema::”**Hakika Mohammad anauwa Masahaba zake**” na kwamba taarifa hiyo ingeenea kwa waarabu na lile dai la linalorembewa na makafiri nalo ni kuwazuwia watu wasikubali daawa hii na wasizingatie yale yaliyo kwa Nabii (S.A.W) na kamwe huu haukuwa mpaka wa kilugha na hivyo haukuleta uzito wala tatizo lolote katika kufahamu maana ya Sahaba kwa makafiri au mbele ya wanafiki seuze waislamu wengine wa mwanzo, kwani wao ni wenye Lugha, weledi na mabingwa wa vichochoro na nyanja zake, hivyo aliyefata fahamu yao na akenda kwenye mwenendo wao basi Allah atamuwafikisha

5 Sher’hu Uswuulil Kaafy / Maulaa Muh’ammad Saalim Al Maazindraany: (12/478),na angalia :As Swah’iih’ minas Syrah /Seyyid Jaa’far Al Murtadh’waa (6/163)

kwenye fahamu sahihi na rai ongofu kwa mengi yenye mapinzo na yaliyojificha maana zake.

….: Maana ya Sahaba katika Istilahi :

Ibara zenye kuweka wazi maana ya Sahaba katika istilahi zimekuwa nyiungi, na za wazi na kina zao zaidi na zenye kukusanya bayana zaidi ni ni ile (Yeyote mwenye kukutana na Nabii akiwa katika hali ya kumuamini na akafa katika Uislamu).

Amesema Shahidi wa Pili[6]**(.Sahaba ni Yeyote mwenye kukutana na Nabii(S.A.W) akiwa katika hali ya kumuamini na akafa katika Uislamu, ,japo ridda yake ikiingilia kati baina ya kukutana nae akiwa amemuamini na baina ya mauti yake akiwa muislam u kwa dhjhiri , na muradi wa kukutana -nae -ni kule kwenye maana pana zaidi kuliko kukaa na kwenda naye pamoja,na mmoja wao kuwasiliana na mwengine, hata asipokuwa amesema nae na hakumuona)**[7]

Na kwa kuweka wazi maana hiyo iliyotangulia nasema :

(Mwenye kukutana na Nabii(S.A.W)) yaani :kwenye uhai wake, ni sawa alimuangalia, au asiyeweza kumuangalia kama vile Abdillahi bin Ummi Mktuum; kwani yeye alikuwa kipofu na mwenye kukutana na Nabii (S.A.W) nae hakumuona. (Mwenyekumuamini) yaani inashurutishwa kumuamini Nabii (S.A.W) na alichokujanacho Nabii (S.A.W) hivyo aliyekutana na Nabii (S.A.W) nae yuko katika waliopewa Vitabu, wanafiki na wengineo, ni sawa awe amesilimu baada ya kifo cha Nabii (S.A.W) au hakusilimu, huyo hanao usahaba.

(**Na akafa katika Uislamu**) :Yaani aliyekufa katika hali ya kurtadi baada ya kifo cha Nabii (S.A.W) basi kamwe hatoitwa swahahaba,wala hana hadhi yoyote ile.

Ufupisho: Na hayo yaliyotangilia yanatudhihirikia bayana umuhimu wa kufanyia kazi lugha na istilahi katika kubainisha mustalahati za kisheria kulingana na ufahahamu wa waliojikita -kwenye fani za Lugha-,kuliko mbali na tafsiri kwa rai au

6 Al A'llaama /Nuurud Diinil a'aamily Al Jabai'y (aliyefariki :965 H)

7 Ar Ria'aya (uk. :339)

matamanio ya nafsi, na kutokana na umuhimu wa upande huu wenye kutowa msingi wa ufahamu uliosahihi wa yatakayokuja hivyo nimependea kuubainisha kama kiingilio katika masuala haya, na hilo ni kabla ya kuingia kwenye kiini cha maudhui yenyewe, ambayo ni Sifa za Thaqalaini (Qur-ani na A'tra –jamaa wa Nabii (S.A.W)-) juu ya Mawalii wa ar Rah'maan (Masahaba-r.a-)

MLANGO WA PILI

Sifa za Thaqalaini (Kitabu cha Allah na Jamaa wa Mtume – s,a.w-) juu ya Masahaba (r.a)

Ni wajibu juu ya kila muislamu kuitakidi utukufu wa nafasi ya Masahaba wa Nabii Mohammad (S.A.W), na kwamba ndio umati na karne bora zaidi ya kiislamu ni ile karne yao, na hivyo ni kutokana kutangulia kwao katika Uislamu, na hadhi ya umakhsusi wao wa ushuhuba wa mwisho wa Manabii na Bwana wa Mitume Mohammad (S.W.A), kupigana pamoja nae, kutobeba kwao Sheria toka kwake, na kuwafikishia waliokuja baadae. Na kwamba muislam aitakidi vile vile kwamba Masahaba wa Nabii (S.A.W) hawapo kwenye daraja moja katika ubora na daraja, bali daraja zao hutofautina kulingana na kutangulia kwao katika Uislamu , Jihadi ,Hijra na kwa kulingana na amali walizofanya kwa ajili ya Allah, Nabii na dini yao .

Hivyo waislamu wanawatanguliza Muhajirina juu ya Answaar, wanawatanguliza ahli Badri juu ya ahli Baiati Ridhwaan, huwakuwatanguliza waliosilimu kabla ya ukombozi -Fat-hu Makkah – na kupigana juu ya wengineo, kulingana na ilivyotajwa na kubainishwa utajo wao toka kwa Thaqlaini (Qur-anna Jamaa wa Mtume) ambao Nabii (S.A.W) ameusia kupendwa kwao .
Hakika Thaqalaani wameshuhudia juu ya uadilifu wa Masahaba (r.a), na riwaya zinazojulisha kusifiwa kwa wema na wao zimeenea, kutokana na matendo yao mazuri na utukufu wa kauli yao. Na kutaja sifa hizi kwa yule mwenye kuzipata ndio usukani katika utafiti huu , kulingana na **Sehemuu zifuatazo:**
Sehemu ya Mwanzo: Sifa za Thaqlaini (Kitabu cha Allah na Ahlil Bait) juu ya (r.a) Masahaba wa Mtume(S.A.W)

Sehemu ya Pili: Sifa za Thaqlaini juu ya (r.a) Masahaba wa Nabii(S.A.W)
Sehemu yaTatu: Sifa za Thaqlaini juu ya (r.a) Muhajirina na Answaar (r.a)
Sehemu ya Nne: Sifa za Thaqlaini juu ya Watu wa Badri(r.a)
Sehemu ya tano : Sifa za Thaqlaini juu ya alietowa na kupigana Vita Kabla na Baada ya Fat-h(Ukombozi):

Sehemu ya Mwanzo:
Sifa za Thaqlaini (*Kitabu cha Allah na Ahlil Bait*) **juu ya (r.a) Masahaba wa Mtume(S.A.W).**

Hakika muislamu mwenye akili timamu husoma Qur-ani na kizingatia Aya zake , kwani Aya za Qur-an zilizotaja fadhila za mema ya Masahaba wa Mtume(S.A.W) na namna ya kuteuliwa kwao na Allah, kuwachaguwa na kuwafanya waadilifu, kuwatakasa na kuwasifu kwa sifa za kukubalika zimeenea .

Sifa za Masahaba wa Mtume(S.A.W) kwenye Kitabu cha Allah:

Amesema Allah Taalaa:**:{ Muhammad Mtume wa Allah na wale walio pamoja nae ni wakali dhidi ya Makafiri ,Wenye kurehemeana baina yao utawaona wenye kusujudu kwa wingi wakitafuta radhi toka kwa Allah na radhi zake alama zao zimo kwenye nyuso zao kutokana na athari za kusujudu huo ndio mfano wao kwernye Tawrat na hivyo hivyo kwenye Injili, ikaitia nguvu ukautia umadhubuti ukakaa sawa juu ya kigogo chake ili iwachukize makafiri , Allah ametowa ahadi kwa walioamini na kutenda amali njema kuwa watapata msamaha na malipo makubwa } [Al Fat-h 29]**

Amesema Muhammad Baaqir an Naasiry : { Muhammad Mtume wa Allah na wale walio pamoja nae ni wakali dhidi ya Makafiri ,Wenye kurehemeana baina yao utawaona wenye kusujudu} yaani wanatafuta kwa hilo ziada ya neema za Allah na fadhila zake, **{ alama zao zimo kwenye nyuso zao kutokana na athari za kusujudu }** alama yao siku ya Kiama ni kuwa na weupe mkali ,{**na mfano huo o uko kwernye Tawrat na}** hivyo hivyo kwenye **{Injili}** yaani .wafuasi wake **,{ikaitia nguvu}** ikajikita na kuusaida basi mmea huo ukapata nguvu ukasimama juu ya kigogo

na asili yake mpaka ukafikilia kikomo, amesema al Waahidy **:**"huu ni mfano uliopigwa na na Allah kwa Muhammad na Masahaba zake.

{ili iwachukize makafiri} [Al Fat-h 29]
yaani katika jambo muna kuwachukiza makafiri kwa wingi wa waumini na kukubaliana kwao juu utiifu.[8]
: **{ Na wa mwanzo waliotangulia miongon imwa muhajirina na ansari ambao walimfata kwa wema , Allah ameshawaridhia na wao amwmridhia Allah}** [At Tawbah:100]

Amesema Sheikh Amiinud Diin Abu Ali Atibrisy :
Hao ni wale waliosali kuelekea Vibla viwili, ikasemwa kwamba ni watu wa Badri, miongoni mwa Ansar na, watu wa Baiati Alaqabat ya mwanzo nao walikuwa wanaume kumi na wawili na watu wa Akaba ya pili nao walikuwa wanaume sabiini nao ni wale walioendewa na Mus-ab bin Umeir na kuwasomesha Qur-ani [9]
Tanbihi:
Kundi katika watu wa fitina na matamanio ya nafsi wamejaribu kuziweka mbali Aya hizi toka kwenye tafsiri yake iliyo ya wazi na sahihi kwa pongezi juu ya Masahaba, na kusema kwamba aya hizo hazijulishi pongezi juu ya ujumla wa Masahaba kwani Allah amesema kwenye mwisho wa Aya ya Mwanzo **:{ Allah ametowa ahadi kwa walioamini na kutenda amali njema kuwa watapata msamaha na malipo makubwa} [Al Fat-h 29]** na akasema kwenye Aya ya pili : **{ Na wa mwanzo waliotangulia miongoni mwa Muhajirina na Answari}** [At Tawbah:100]
Hivyo tamshi (منهم)na (من) katika Aya mbili ,linamaanisha: katika miongoni mwao ,na sio Masahaba wote,tunabainsha mambo yafuatayo :
Kwanza :

[8] Tafsiir Majmaail Bayaan ,angalia Jaamiil Jawaamii,min Wahyil Qur-aan (Suratil Fat-h :29)

[9] Angalia Jaamiil Jawaamii, na angalia Tafsiir Wahyil Qur-aan,Al 'Ayyaashy (Surati Tau
:100)

Hakika Allah (S.W) kwenye Kitabu chake amebainisha Ayaat Muhkamaat –Yaani uwazi – zisizokuwa na ta-awili ndani yake, na yeyote atakayejaribu kutafiti taawili yake basi habari yake itamfedhehesha, na kuporomoka kwake kukashifika .
Na miongoni mwao ni Ayatumutashabihati, yaani :ndani yake imokushabihiana kwa dalili juu ya wengi wa watu au baadhi yao, hivyo asili ni kurejesha Mutashabih kwenye Muhkam kwa hivyo aliyefanya hivyo ameongoka, na aliyefanya kinyume chake atakuwa amekwenda kinyume na haki.

Pili :Hakika maaana ya neno(منهم) kwenye kauli yake Taala **{ وعد الله الذين آمنوا و عملوا الصالحات منهم مغفرة و أجرا عظيما}:** [Al Fat-h] na neno (من) kwenye kauli yake **{ Na wa mwanzo waliotangulia miongon imwa Muhajirina na Answari}** (AtTawbah:100)Maana ya mwanzo :Ni kwamba (من) ni kwa maana ya jinsi yao , na miongoni mwa mifano yao Na hii ni kama ilivyo kwenye Kauli yake Taala: **{Hivyo ni kwamba yeyote yule mwenye kutukuza vielelezo vya Allah basi hiyo ni kheri kwake mbele ya Mola wake,na wamehalalishwa kwenu wanyama isipokuwa tu wale wale waliotajwa kwenu, basi jiepushen ina vinavyoabudiwa visivyokuwa Allah na mujiepushe na kauli za uongo.}**
[Al Hajj:30]

Wala maana haikai sawa kwamba Allah (aamrishe kjiepusha na badhi ya awtthaan (masanamu au chochote kinachoabudiwa kisichokuwa Allah- S.W-) bila ya mengine bali ametuamrisha kujiepusha na authani zote kwenye kali yake (S.W):**{ Hivyo jiepusheni na uchafu –min- katika authan na jiepusheni na kaul iza uongo }**[Al Hajj:30] yaani :jiepusheni na authan katika jinsi na mifano ya masanamu (authani) .
Maana ya Pili : Kwamba neno (من) linakuja kwa ajili ya msisitizo na kwa ajili ya jinsia –aina -
Pia ndivyo ilivyo kwenye kauli yake Taa'la: **{Na tumeteremsha (من) katika Qur-anyaliyo ponyo na rehema kwa waumini na kamwe haitowazidishia madhalimu ila hasara}** [Al Israa: 82] hivyo basi jee yuko mwislamu mwenye akili mwenye kufahamu maana ya Aya kuwa baadhi ya Qur-ani ni ponyo na rehema , na baadhi yake haiko hivyo ?

Lakini mwislamu anafahamu kwamba Qur-anyote ni Ponyo na rehema , na kwamnba Allah (S.W) amewatilia nguvu kwenye Aya tukufu iliyotangilia kwamba Qur-anyote ni Shufaa na rehema.
Tatu : Kwamba mtiririko wa Aya ya mwanzo ndani yake zimo sifa za Masahaba wote na hamna upondwaji wa Sahaba ye yote yule – baadhi yao-. Amesrema Allah Azzaa wa Jallah :**{Wakali juu ya Makafiri ,warehemevu baina yao ,utawaona ni wingi wa kurukuu , wingi wa kusujudu }** [Al Fat-hu:29], hivyo Allah amewatakasa kwenye siri na dhahiri zao kwa kusujudu, kurukuu na kujidhalilisha kwake na akawatakasa kwenye siri na dhahiri zao vile vile kwenye kauli yake Taala: **{ Wanatafuta fadhila toka kwa Allah na uradhi wake}:**[Al Fat-hu :29]

Bali Tabaraka wa Taala anapotaka kuangamiza kaumu hubainisha dhahiri na undani wao, kama alivyosema Allah kuhusiana na wanafiki :**{Hakia wanafiki wanamuhadaa Allah nae ni mwenyekuwahadaa -vile vile - , na wanaposimima kwenda kuswali basi husimama katika hali ya uvivu , wanajionesha kwa watu na hawamkumbuki Allah ila kidogo tu - }**
[An Nisaa :142]

Iinatubainikia kwamba Allah anawapa ahadi wale ambao wameamini na kutenda amali njema katika wao kupata maghufira na malipo makubwa :[Alfat-h : 29] na kauli yake Taalaaq

{Na waliotangulia wa awali katika Muhajirina na Answaar}

[At Tawbah :100] yaani :katika jinsi yao, na kutilia msisitizo juu ya hali yao pamoja na Nabii (S.W.A).

Sifa za Ahlul Bait Juu Ya Masahaba Watukufu :

Sifa hizi zilibarikiwa na kwenye Kitabu cha Allah ilikuwa ni habari njema iliyokuwa kwa mwenye kuwadiriki Masahaba au kumuona mmoja wao, amesema Nabii (S.A.W):”Mafanikio kwa mwenye kuniona, habari njema kwa mwenye kumuona alieniona na habari njema kwa mwenye kumuona aliemuona alieniona ” Ni Fahari iliyoje kwa Amiril Muuminiin Alinae akiwa mwelevu kwa

habari za kaka zake baada ya kuwajibu watu Al-Kufa na kuona ukosefu na upungufu utetezi wao kwake ,akisema akiwa mwenye kukumbusha na kuwasifu Masahaba wa Mtume (S.A.W):"Hakika nimewaona Masahaba wa Mtume (S.A.W)- basi sikumuona yeyo yule aliyeshabihiyana Na yeyote yule katika nyie, hakika wao walikuwa wakiamka katika hali ya nywele timtim wenye mavumbi na wao wamekesha katika hali ya kusujudu, kusimama -kwa kuswsali – wakigeuka baina ya nyuso za o,wakisimama mfano wac kaa la moto kwa kukumbuka marejeo yao, kama kwamba baina ya macho yao kuna miguu ya mbuzi kutokana na urefu wa kusujudu kwao, Allah atajwapo macho yao hububujikwa na machozi mpaka vifua vyao kurowa kwa machozi ,wakiinama kama inavyoinama miti siku ya upepo mkali, kutokana na hofu ya adhabu na kutarajia malipo "[10] Imam Ali anaieleza hali yake na ile ya Masahaba wa Mtume (S.A.W) na ushujaa wao wote mbele ya uso wa maadui kwa kaul iyake:"Kwa hakika tulikuwa pamoja na Mtume (S.A.W) tunauwa mababa zetu, watoto wetu, makaka na maaami zetu, yote hayo hayatuzidishii ila imani, kujisalimisha –kwa Allah- na kuendelea kwenye vita ,uvumilivu juu ya maumivu na jitihada juu ya kuwapiga vita maadui, mtu miongoni mwetu na mwengine katika maadui zetu wanatiana mieleka kama wanavyosongana mafahali wawili akimvizia mwenzake yupi kati yao atamnywesha mwenzake kikombe cha mauti ,basi mara ushindi huwa wetu dhidi ya maadui zetu,na mara huwa maadui zetu dhidi yetu, hivyo Allah alivyouona ukweli akateremshwa kushindwa juu ya maadui zetu na kututeremshia, mpaka Uislamu ukajikita kwernye makazi yake,naapa lau tungefanya kama munavyofanya nyie-qakimaanisha wafuasi wake -Diniushindi "
.anadamu,hivyo Allah atatuma upepo mweusi, na hapatobakia asiekuwa Allah Taalaa ila Allah atakichukuwa. "[11]

Nabii (S.A.W) alimuombea dua ya kheri na rehema kwa kila atakae chukua nafasi yake baada ya yeye ,bila ya kuainisha alieainshwa kwa uimamu-uongozi, na akajaalia sifa ya atakaechukua nafasi yake kuwa ni mwenendo wake juu ya mwongozo wake (S.A.W), hivi ni kutokana wa ujulishaji wa

10 Nahjul Balaagha (uk.43) na angali Al Kaafy(236 /2),Bihaarul Anwaar⊛307/66)

11 Bih'aarul anwaar (309/22)

makubalino -Ijmai'-juu ya neno la Masahaba juu ya watakaomchagua baada yake. Imepokewa kutoka kwa Ridhwa (a.s), kutoka kwa mababa zake, amesema Allah Taalaa **:{ Muhammad Mtume wa Allah na wale walio pamoja nae ni wakali dhidi ya Makafiri ,Wenye kurehemeana baina yao utawaona wenye kusujudu kwa wingi wakitafuta radhi toka kwa A na radhi zake alama zao zimo kwenye nyuso zao kutokana na athari za kusujudu } [Al Fat-h 29]**

Ni wajibu ya kila muislamu kuitakidi utukufu wa cheo cha Masahaba wa Nabii (S.A.W).

SEHEMU YA TATU :SIFA ZA THAQLAINI JUU YA MUHAAJIRINA NA ANSWAAR;

Allah amewafanya bora Muhajirina na Answaar baina Masahaba wengine (r.a). Hivyo ni kutokana na kutangulia kwao kuitikia wito wa Mtume (S.A.W), kuingia kwao mumo na kustahamili kwao maaudhi kwa ajili yake. Allah amewafanya bora Muhajirina juu ya Answaar, kwani Muhajirina wamekusanya baina ya Hijra na nusra. Na wakawacha jamaa, mali na nchi zao na kutoka kwenda kwenye nchi ambayo wao ni wageni wakitafuta malipo na nusra tu ya Allah (SW)

Ama Answaar basi wao walijiwa na Mtume (S.A.W) kwenye nchi yao wakamnusuru ,wakagawa mali wake zao kwa ajili nusra ya Allah na Mtume wake (S.A.W).

Na Thaqlaan (Kitabu cha Allah na I'tra –jamaa wa Nabii- (S.A.W) wamelishuhudia juu ya fadhila na kuridhiwa kwao, Aya Tukufu zimefatana na kuenea zikiweka wazi hali ya Masahaba, zenye kubainisha fadhila zao kubwa na uradhi wa Mola wa walimwengu wote kwao, na ibara kuhusiana na hili zimekuja kwa aina mbali mbali zikiwa ni tafsiri za Aya mbali mbal

Sifa za Qur-ani Tukufu juu ya Muhajirina na Answaar:

Amesema Ta'alaa:**{Ni kwa ajili ya Muhajirina waliotolewa toka kwenye nyumba zao na mali zao wakitafuta fadhila za Allah na uradhi, na wanamnusuru Allah na Mtume wake hao ndio wakweli na wale ambao walikaa kwenye nchi na imani kabla**

yao wanawapenda wale waliohamia kwoa na kamwe kwenye nyoyo zao hawana haja yoyote ile kwa yale waliopewa –answaar –na hata kwamba wanayohaja , na ye yote aliyeepushwa na choyo cha nafsi yake basi hao ni wenye kufanikiwa}

Amesema Sheikh Muhammad Baaqir an Naaswiry :

{Ni kwa ajili ya Muhajirina }waliohamia Madina wakikimbia toka Makkah na kwengineko **{waliotolewa toka kwenye nyumba zao na mali zaowiokuja wakitafuta fadhila za allah na uradhi }** yaani wanainusuru dini ya Allah .**{ na wanamnusuru Allah na Mtume wake hao ndio wakweli na wale ambao {walikaa kwenye nchi }** yaani Madina walipoishi Answaar kabla ya Muhajirina,au kabla ya kuamini kwa Muhajrina nao ni wanaume sabiini watu wa bayat Al-aqabah waliom-bayi' Nabii(S.A.W) juu ya kupigana vita dhidi ya weupe na wekundu **{na imani kabla yao wanawapenda wale waliohamia kwao}** nao kwa hakika waliwatendea mema Muhajirina, na kuwaweka kwenye nyumba zao na kuwashirikisha kwenye mali zao, na kamwe hawana hasadi yoyote wala chuki kwa waliyopewa Muhajirina na kukoseshwa wao toka kwenye mali za Bani Nadhw'iir,**{ kamwe kwenye nyoyo zao hawana haja yoyote ile kwa yale waliyopewa –Answaar –na} hata kwamba ikiwa wanayohaja}** yaani pamoja na ufakiri wao na haja zao**, {na ye yote aliyeepushwa na choyo cha nafsi yake}** yaani anayejiepusha na ubakhili wa nafsi yake**{basi hao ndio wenye kufanikiwa}** waliofanikiwa na kufuzu .

Amesema Sheikh Muhammad As Sabzawaary An Najafy :

{Ni kwa ajili ya Muhajirina} walioiwacha Makkah na kukusudia Madina, Mahamizi ya Nabii(S.A.W) na toka kwenye nchi ya vita kwenda kwenye nchi ya amani nao ni **{ waliotolewa toka kwenye nyumba na mali zao}** walizokuwa wakizimiliki **{wakitafuta}..**
{ fadhila za Allah na uradhi }wakitafuta fadhila uradhi na rehema zake**{na wanamnusuru Allah}** yaani :wanahama kwa ajili ya

kumnusuru na wananusuru …**{ na Mtume wake}** kwa kumpa nguvu dhidi ya maadui zake **{hao ndio wakweli}** kikweli kweli, kwani wao walikusudua kuinusuru Dini , na kumuitikia Allah na Mtume wake (S.A.W), na baada ya kuwasifu watu wa Makkah na wengineo miongoni mwa Muhajirina amewasifu Answari katika watu wa Madina kwani wao waliridhisha nafsi kutokana na –Fayi- waliamua wagawiwe Muhajirina wanaohitajia akasema
{ na wale ambao walikaa kwenye nchi }{na imani} kwa vile hawakuamini kabla ya muhajirina, bali walioamini baada ya Kuhamia kwao Nabii (S.A.W) kwao isipokuwa kidogo tu miongoni mwao. Ama kuunganishwa imani na Unabii, ni kuunganishwa ni kwa kidhahiri na lile la kimaana kwani imani haikai, na makadirio yake na wakaona bora imani kuliko ukafiri **{kabla yao}** yaani kabla ya muhajirina hawajahamia kwao pale walipowafanyia wema,kwa kuwaweka kwenye nyumba zao na kuwashirikisha kwenye mali zao **{wanawapendelea wale waliohamia kwoa }**

{na kamwe kwenye nyoyo zao hawana haja yoyote ile kwa yale waliopewa }–Answaar –yaani kamwe sio wenye choyo ,chukii wala hasad nafsi zao kwa sababu ya yale yaliyochukuliwa na Answaar katika Fay, iliyomilikiwa kwenye mali ya Bani Nadhw'iir,bali nafsi zao zilipendezewa na walikuwa **{na wananyima nafsi zao } yaani wanawatanguliza na wanaawafadhilisha katika upewaji na hata kwamba wanayohaja }** yaani hata wakiwa juu ya nafsi zao wanayohaja na ufakiri,na hivyo ni kutokana na huruma kwa ndugu zao na kutafuta malipo na thawabu**, { na ye yote aliyeepushwa na choyo cha nafsi yake basi hao ni wenye kufanikiwa}**Yaani wenye kufuzu kwa thawabu za Allah wakitarajia Pepo na neema zake.
Amesema Allah Taa'laa:**{ Na wale ambao walihama na kupigana kwenye njia ya Allah na wale ambao walikaa na kunusuru hao ndio wumini wa kweli wameshathibitikiwa na maghufira na riziki tukufu . pamoja nao basi hao ni miongoni mwenu, na jamaa ni bora wao kwa wao kwenye Kitabu cha Allah hakika Allah ni mjuzi juu ya kila kitu }**
[Al –Anfaal :74-76].

Amesema Sheikh Muhammad As Shabzawaary An najafy :

{Na wale ambao walihama na kupigana} yaani wale ambao walimsadiki Mtume (S.A.W) kwa yale aliyokujanayo toka kwa Allah ,na kuyakinisha kuwepo kwa Allah na upweke wake ,na kuwacha nchi zao wakikimbia kwa ajili ya Dini yao pamoja na Mtume (S.A.W) na kupigana .pamoja nae ili kunusuru Dini na Sharia yake **{hao ndio waumini wa kweli}**Al –Anfaal :74-76].hao ni wakweli kikweli kweli ,kimaneno na kivitendo, kwahakika walithibitisha imani yao mpaka wao wakapata dalili kwamba hiyo ndiyo imani ya kweli, hivyo basi **{wameshathiboitikiwa na maghufira.}**.

Yaani Allah amewaandalia wao **{maghfira}:**kwa kusamehewa makosa yao, na riziki tukufu za wasaa kubwa isiyosibiwa na tatizo lolote **{Na wale ambao waliamini baadae na kuhama na kupigana}** [Al –Anfaal :75].yaani walioamini baada ya Ukombozi wa Makkah ,na imesemwa kwamba ni wale walioamini baada ya kuamini kwenu .**{Na wakahama }**kwenda kwa Nabii(S.A.W) baada hijra yenu ya mwanzo **{ Na wakapigana pamoja nanyi}** wakawapiga vita makafiri na washirikina pembeni mwao **{hivyo hao ni miongoni mwao }**basi hao ni katika nyie kiimani ,kihijra na kijihadi na kihukmu katika kuwaunga mkono ,mirathi na nusr; pamoja na imani na Hijra yao kuchelewa .
Na akasema Allah Taa'laa :**{Na wale ambao waliamini na wakahama na wakapigana katika njia ya Allah kwa mali na nafsi zao wao wanayo daraja kubwa na wao ndio wenyekufuzu**

Amesema Seyyid Muhammad Husein Fadhlullahi :

{Na wale ambao waliamini na wakahama na wakapigana } na kuhimili waliyoyahimili miongoni mwa kuhama nchi , kuelekea kwenye pahala ambapo mtu anamiliki uhuru katika Daa'wa na Jihadi na kujitenga toka kwenye mwahala mwa ukandamizaji ambamo kunaweza kumhatarishia imani yake, na hiyo ni dalili ya ikhlasi kubwa kwa ajili ya Allah na katika yale yanayoonesha juu ya kila huruma za kinafsi kwenye mambo ya kishenzi, kwa ajili ya Allah pekee ,na wale ambao walipigana Jihadi **{katika njia ya Allah kwa mali na nafsi zao}** kwa yale waliyoyatowa katika mali zao kwa ajili ya Da'awa na Jihadi ,kwa yale waliyopambana nayo katika makosa ya kimadia na kimaana kwenye muelekeo huu, pale

walipokosa kila maana kwa upande wa kibinadamu katika mule wanamoishi, na kuelekea kwenye kundi lenye harakati kwenye nyanja za ujumla wenye kuambatana na Allah , na kwa uhai,hao **{wao wanayo daraja kubwa}** kuliko kila mfano mwengine ambao huweza kufanya kheri katika nyanja maalum**{ na wao ndio wenyekufuzu }**kwa rehema,ridhaa na Pepo yake.

Na akasema Allah Taala:**{Ewe Mola wetu hakika sisi tumemskia mlinganiaji akilingania imani kwamba muaminini Mola Wenu hivyo tumeuamini ewe Mola basi tusamehe madhambi yetu na tufutie maovu yetu na utufishe pamoja na -watu- wema. Ee Mola wetu! na utupe yale uliyotuahidi juu ya Mitume yako na usituhuzunishe Siku ya Kiama kwani hakika Wewe kamwe hukhalifu ahadi . Basi Mola wao akawatekelezea kwamba hakika mimi kamwe sibezi amali ya mfanyaji amali ye yote yule, awe mwanamume au mwanamke wao kwa wao, hivyo wale ambao wamehama na na kufurushwa toka kwenye nchi zao na kuudhiwa katika njia yangu na wakapigana na kuuliwa, hakika nitawafutia maovu yao na hakika nitawaingiza Peponi -ambazo – chini yake hupita mito, yakiwa ni malipo mbele ya Allah, na Allah kwake Yeye yapo malipo mema.**
A mesma Seyyid Abdullahi Shibr:

{Basi Mola wao akawatekelezea} yale waliyoyataka**{ kwamba hakika mimi} {kamwe sibezi amali ya mfanyaji amali ya ye yote yule awe mwanamume au mwanamke }** bayana ya amali zao **{wao kwa wao }** kwa mkusanyiko wa wanaume na wanawake miongoni mwao ni asili moja au uislamu **,{hivyo wale ambao wamehama}** shirki, nchi zao au kaumu zao kwa ajili ya Dini **{ na kufurushwa toka kwenye nchi zao na kuudhiwa katika njia yangu}kwa ajili ya dini yangu na sababu yake{ na wakapigana}**na washirikina **..{ na kuuliwa}**wakastash-hid na nah ii haimaanish iutaratibu kwa vile muradi ni pale walipoambiwa piganeni … **{ hakika nitawafutia maovu yao}{ na hakika nitawaingiza Peponi -ambazo – chini yake hupita mito ,yakiwa ni malipo mbele ya Allah }**wanayostahiki toka kwake.**{ na Allah kwake yeye yapo malipo mema.}** juu ya amali asioweza-kutowa - ye yote yule asiekuwa yeye.

Hivyo ewe msomaji, mpenzi wa Ahlil Baiti Rasuulillahi - yatie akilini hayo **y**aliyotangulia, madogo mepesi miongoni mwa yaliyokuja katika fadhila za Masahaba. wote.

Sifa za Thaqlaan
(Kitabu cha Allah na I'tra –jamaa wa Nabii-(s.a.w))-
Juu ya Makhalifa watatu (r.a))

Na baada ya kutubainikia namna sifa na madaha zilivyochupa mpaka juu ya Masahaba wa watukufu, umekuja umakhsusi na ufungaji wa juu wa sifa hizo maalum juu ya Makhalifa watatu waongofu wa mwanzo (r.a). Nabii-(s.a.w) aliwaowa bint Abubakri Sidiq(r.a) na Hafswah bint Omar bin Khattab, bali kamwe hakuowa mwanamke wa Kihaashimiyyah nae akiwa na wake kumi na mmoja, akawamuzesha Othman bin Affaan(r.a) mabinti zake wawili Ruqayyah na Ummu Kulthuum. Imam Ali (as.) akamuozesha Omar ibn Khattab binti yake Ummu Kulthuum.[12] Na watoto wake akawaita kwa majina yao na hivyo hivyo watoto wake yeye pia waliwaita watoto wao kwa majina yao.[13]

Inawezekana kutolea dalili hali hii juu ya mahusiano haya mazuri wenyewe kwa wenyewe., na yale waliyokuwanayo miongoni mwa mapenzi, na utii wao kwa Allah na kwa Nabii wake-(s.a.w), na kwamba hili linaonekana wazi kwa yule ambaye moyo wake na kuondokewa na kizibo cha ubaguzi toka kwenye macho yake, na akageuza geuza macho yake kwenye vitabu vya Historia kwa mambo na kadha na riwaya tofauti.

Lakini ninatoshelezeka na baadhi ya riwaya zilizotolea na maulamaa kwenye vitabu vyao toka kwa maimamu (a.s) ambazo zinajulisha juu ya pongezi hizi .

Amesema Imamu Ali (a.s) "Naapa hakika cheo chao kwenye uislamu ni kikubwa ,na kwamba hakika walisibiwa na majeraha

12 Angalia al Kaafy (115/6) , ,Ii'laamil Wurraa (uk.141).

13 Angalia uk….wa kitabi hichi.

makali kwenye uislamu, Allah awarehemu na awalipe malipo makubwa kwa waliyoyafanya)[14]

Amesema (a.s) akiwapongeza Makhalifa watatu na wale waliowabayi (r.a):"Hakika kaumu iliyonibayii ni ile kaumu iliyowabayii Aba Bakri Sidiq(r.a) , Omar na Othman bin Affaan (r.a) juu ya waliyowabayiia wao, na kamwe haimpasii mwenyekuwepo kuchagua wala aliekuwa hakuwepo yeye kupinga , shura ilikuwa ya Muhajirina na Answaar, hivyo wanapomteuwa mtu yeyote na wakamwita Imamu, jambo hilo huwa ni ridhaa ya Allah (S.W) , na akitoka kwenye amri ya makubaliano yao kwa kutia kasoro , bid-a au upotevu atakuwa ametoka kwenye makubaliano hayo, na akikataa watampiga vita juu ya kufuata njia ya waislamu na Allah atamsaliti kwa lile alilolipa mgongo)[15]

Akasema Imamu Ali (a.s) akimpongeza Omar bin Khattab (r.a) "Hongera za Allah zimwendee fulani mefanya mema, akatibu matatizo, akasimamisha Sunna ,akaipa mgongo fitina, akaondoka akiwa ni mwenye nguo safi, mchache wa aibu,akaboresha habari zake ,shari zake akazitangulia, akatekeleza utiifu wake kwa Allah,na kujiepusha na shari kwa sababu ya haki yake[16]"

Nae kasema vile vile kumwambia Omar bin Khattab (r.a) kwenye uhai wake, akiwa amemshauri kuhusiana na kwenda kwenye vita na Warumi" Hakika ewe utakapo kwenda mwenyewe kwenye adui huyu likatokea la kutokea basi waislamu hawatokuwa na pakukimbilia wala pahala pa kutiliwa nguvu, hawatokuwa na pakukimbilia isipokuwa nchi zao zilizombali, baada ya wewe hakutakuwa na marejeo, hivyo mpeleke mtu mwenye ujuzi wa kupigana na nasaha, Allah atakapotupa ushindi basi hilo ndilo tunalolipenda na ikiwa vyenginevyo basi wewe utakuwa ndio makimbilio ya waislamu . "[17]

14 Waqatu Swaffaini (uk. :88) ,Sherhu Nahjil Balaaghah(86/15)

15 Nahjil Balaaghah(uk. 366), Bih'aarul anwaar(76/33)

16 Nahjil Balaaghah (uk. 350)

17 Nahjil Balaaghah(uk. 192), Bih'aarul anwaar(135/31)

Na cheo toka kwa Ahlil Bait (a.s) kwa Abubakri Sidiq(r.a) Omarbin Khattab (r.a) kikachupa mpaka hata baada ya kufariki kwao kwa muda mrefu ,kiasi kwamba walikwenda juu mwongozo wao na kamwe hawakubadilisha chochote bali walikuwa wakichota toka kwenye visima vya elimu zao na fatawa zao (r,a), na dalili ya haya ni :

Vile alivyosema Imamu Ali (a.s) pale alipotakiwa kurejesha Fadak –Nae wakati huo akiwa Khalifa :"Hakika mimi namuonea haya Allah kurejesha kitu kilichozuwiwa na Abubakri Sidiq na kuendelezwa na 'Omar"[18]

Nae Imam Muhammadul Baaqir akalihimiza kundi lake kufanya kama alivyofanya yeye, pale alipomfata Abubakri Sidiq, pale alipoulizwa kuhusiana na kujuzu kwa kupamba upanga, akasema "Naam hakika amepamba Abubakri Sidiq upanga wake kwa fedha !muulizaji akasema :unasema hivi? Imam akondoka pahala pake akasema:"Naam Sidiq Naam Sidiq ,yeyote asiemwita Sidiq basi Allah kamwe hatomsadikisha kauli yake Duniani na akhera"[19]

Basi hao ndio Ahll Bait ya Rasuulil Lahi (a.s) nao ndio watu wazama za karibu na Abubakri Sidiq na Omar bin Khattab (r.a) kamwe hawakupitikiwa na walichokifanya wala kuondokewa na walichokifanya , hivi haitutoshelezi ushahidi na rai zao kwa kundi hilo la watu , au tanaka mongozo na na kauli zisizokuwa mongozo na kauli zao (a.s)?

Sifa za Nabii (S.A.W) na I'trah Juu ya Muhajirina na Answaar:

Kumekuja riwaya sahihi zenyekuenea toka kwa Ahlil Bait (a.s), zinazojulisha juu ya fadhila za Muhajirina na Answaar miongoni mwao, ninazileta hapa : Toka kwa Jabir bin Abdillahi toka kwa Nabii (S.A.W) amesema:" Muhajirina na Answaar ni vipenzi wenyewe kwa wenyewe duniani na Akhera,na waliowachiwa katika Makureshi, na waliochiwa huru katika Thaqiif, ni vipenzi wenyewe kwa wenyewe duniani na Akhera"[20]

[18]Sherhu Nahjil Balaaghah(252/16)
[19] Kashful Ghummah (147/2)
[20] Angalia Aamaalit Tuusy(uk.268) na Bih'aarul anwaar(22/311)

Katika habari inayotoka kwa Ka'ab bin Ujrah :" Hakika Muhajirina na Answaar na Bani Hashim walitofautiana kuhusu Mtume (S.A.W) ni yupi katika sisi kwake yeye ni vipenzi zaidi amesema:" amesema: " Mtume (S.A.W):"Ama nyie enyi kundi la Answaar basi hakika mimi ni kaka yenu wakasema:" Allahu Akbar! tunakwenda nae tunaapa na Mola wa Kaaba!,ama nyie enyi kundi la Muhajirina basi hakika mimi ni katika nyie wakasema:" Allahu Akbar! tunakwenda nae tunaapa na Mola wa Kaaba! akasema:" Ama nyie kundi la Bani Hashim basi hakika nyie ni katika mimi na toka kwenu basi sote tukasimama tukijifakharisha kwa Mtume (S.A.W)"[21]

Na kutoka kwa Abi Sai'idil Khudry , hakika alimsikia Mtume (S.A.W) akisema:"Hakika mimi nimekuwachieni kwenu vizito viwili isipokuwa tu kimoja vyao ni kuikubwa kuliko chengine akasema zingatieni, hakika watu wa nyumba yangu ni jicho langu ninalokimbilia, zingatieni na hakika Answaar ni ngome yangu basi wasemeheni matendo yao,na msaidieni mtenda wema wao"[22]
Na nasi hizi tukufu kamwe hazikuwa mbali kwenye akili za Ahlil Bait, bali hakika walizihifadhi na kuzitia akilini ,na katika hilo ndio iliyokuwa sifa ya Imam Ali (a.s) kwa Muhajirina kwenye jibu lake kwa Muawiya, anasema:"Hivyo watu waliotangulia wametangulia kwa utangulizi wao na Muhajirina wa mwanzo wameondoka na fadhila zao".[23]
Nae akasema (a.s): "Na katika Muhajirina zimo kheri yingi tunazozielewa, Allah awalipe malipo mema"[24]

Hasan amesimulia toka kwa Nabii (S.A.W) kwamba amesema: " Yeyote aliekimbia kwa ajili ya dini yake toka nchi kwenda kwenye nchi ,hata ikiwa ni shubiri moja ya ardhi basi huyo amethibitikiwa na Pepo, na atakuwa rafiki wa Ibrahim na Muhammad (S.A.W)."[25]

21 Al Manaaqib(331/3), Bih'aarul anwaar(22/312)

22 Bih'aarul anwaar(22/311)

23 Nahuj Balaaghah (uk.374), Bih'aarul Anwaar(33/104) ,Waqa'atu Swiffiin (uk.149)

24 Bih'aarul Anwaar(33/1104) ,Waqa'atu Swiffiin(uk.88)

25Bih'aarul Anwaar(31/19) ,, Majmuua'tu Warraam (33/1) Tafsiirus Swaafy (490/1),Tafsiiru Nuuruth Thaqalaini (491/1)

Na hayo yaliyotangulia ni mtiririko katika mitiririko, na matone toka kwenye bahari kubwa inayotiririka juu ya nyoyo, hivyo yawe ni mwongozo unaotosheleza, na nuru ya kuangazia, imuhuwishe yule aliekuwa kasahau, au alietaka kundi lao.afate fadhila na mienendo yake, Wallahi hongera Muhajirina na Answaar Ahlil Bait (a.s) pale walipowasifu Masahaba(r.a) na kamwe hawakumkuta yeyote toka kwenye sifa na mad-hi hizi.

Sehemu Ya nne:Sifa za Thaqlain juu ya Watu wa Badr:

Baada ya sifa za ujumla juu ya Masahaba(r.a) na kwa vigawanyo vyake Muhajirina na Ansar (r.a),kumekuja ubainishwaji wa makundi maalum ya Masahaba (r.a), kwa sababu ya kutofautika kwao kutokana na amali tukufu au sababu muhimu hivyo wakajichukulia ziada ya fadhila kuliko wenzao wengine.
Allah (S.W) akajaalia ubora na daraja kubwa kwa Masahaba waliohudhuria vita vya Badri miongoni mwa waislamu, ambapo wakati huo walikuwa kidogo na kamwe hakujitayarisha na mapambano dhidi ya vigogo wa kikureshi pale mlinganiaji alipowajia kwa ajili ya kupambana na msafara wa makafiri wa kikureshi.

Ushindi ulio wa wazi ulipatikana kutokana na fadhila na wema wa Allah juu ya mikono ya wachache hao, ambao waliowatisha waarabu na kuwafanya waogope ,na Vita hivi vikawaletea hadhi kubwa baina ya makabila ya kiarabu .
Kwa hakika Allah aliwatunza watakatifu hao na kuwapa habari njema kwamba wao kamwe hawatakufa kwenye kufuru na kwamba madhambi yao yamefutwa kwa idhini yake (S.W) (nasi Allah atujaalie hivyo)..

Na hivi ndivyo alivyomuhakikishia Omar bin Khattab pale alipotaka idhini akate kichwa vha Khatib bin Abi Baltah’ (r.a) hivyo Nabii (S.A.W) akamwambia:"Na kitu gani kinakujulisha ewe Omar huenda Allah ameona amali za watu wa Badri akawambia :’Fanyeni munavyopenda kwa hakika nimeshakusameheni “[26]

26 Angalia :Bih’aarul Anwaar(92/21),Sherhe Nahuj Balaaghah (89/17)

Utakaso huu na shahada ya milele toka kwa Allah (S.W) juu ya ulimi wa Nabii (S.A.W) kwa watu wa Badri na kwamba yeye yuko radhi nao mpaka siku ya kiama.

Sehemu ya Tano :Sifa za Thaqlaini juu ya alietowa na kupigana Vita Kabla na

Baada ya Fat-h(Ukombozi):

Baada ya kusifiwa kwa watu wa Badri (r.a), kutokana na hima yao ya kupigana pamoja na Mtume (S.A.W) bila ya ulinganio wala ahadi ,wigo wa sifa umeongezeka ili uchanganye wale ambao walitowa na kupigana kabla ya Fat-h.

Muislamu anaamini ubora wa hao waliotowa kabla ya Fat-h. na kupigana mingoni mwa Msawahaba (r.a) juu ya wale ambao walitowa baada ya Fat-h. na kupigana baada ya Fat-h..

Fat-h.iliyokusudiwa ni (Suluhu Hudaibiyyah) kama alivyosema Allah Taa'la **{ Hakika sisi tumekukombolea ukombozi ulio wa wazi -ukombozi uliomkubwa - }**[Al Fat-h:10]

Na H'udaibiyyah:Ni kisima karibu na Makkah ,hapo ndipo palipotokea baia't Ridhw'wan, na Suluhu Hudaibiyyah ilikuwa hapo.pale Makureshi walipomzuwia Mtume (S.A.W) na **Masahaba zake(r.a) kuingia Makkah hivyo wakambayii'(wakampa ahadi ya kumtii)** juu ya kifo.

Na wamefanywa makhsusi watu wa Fat-h(Ukombozi) au Suluhu Hudaibiyyah kwa sifa hii makhsusi na miongoni mwa fadhila na hadhi kubwa kwa mahitaji ya kiwango cha juu yaliyokuwa kwa Nabii (S.A.W). na Masahaba zake (r.a) katika wakati wake kwa idadi na hesabu kwenye mazingira yake mazito , Suluhu na na yale yaliyotokea baadae miongoni mwa ahadi za utii baina ya Masahaba (r.a) na Nabii (S.A.W) .Fat-h (Ukombozi) ulio bayana kwa ajili ya matokeo makubwa makubwa yaliyofatilia baada ya hapo.Na kwa kweli Mtume (S.A.W) aliwabayii waislamu, na idadi yao ilikuwa haizidi Masahaba (r.a) na kutokuhudhuria kwa Othman kwenye mubayaa'-ni matokeo ya kwenda kwake kwa ajili ya ukaa kati tokea kwa Nabii (S.A.W) kwa watu wa Makkah-,

Nabii (S.A.W) alinyanyua mmoja wa mikono yake mitukufu juu ya mwengine kwa ajili ya mubayaa' wa Uthman bin Affaan (r.a).

Waislamu walisema hongera kwa Othman ameshatufu Al Kaabah nae amekwenda baina ya Swafa na Marwa na ameshatoka kwenye ihram Nabii (S.A.W) akasema " hakuwa wa kufanya hivyo,basi Othman(r.a) alipokuja akaulizwa na Nabii (S.A.W) jee umetufu? akasema :" Sikuwa mwenyekufu wakati Mtume (S.A.W) bado hajatufu .

Hivyo basi Bay-a'a hii ikaitwa Fat-h (Ukombozi) kutokana na yaliyopatikana baada na kwa sababu yake miongoni mwa kheri nyingi na nusra kwa waislamu, na Allah Mtukufu akawasifu watakatifu hao, na kuwatakasa dhahiri na kwenye siri zao hivyo (S.W) akasema:**{ Hakika Allah amewaridhia waumini pale walipokubayi'i chini ya mti , basi Allah ameyaelewa yale yaliyomo kwenye nyoyo zao ,hivyo akashusha utulivu juu yao na akawalipa ukombozi uliokaribu }** [Al ;Fat-h:18]
Amesema Sheikh Amiinud Diin Abu Aliat Tw'ibrasy Abu Aliat Tw'ibrasy :

" Imeitwa Baia'tu Ridhw'waan kwa sababu ya Aya hii,
(kwani wao) walimbayii' Nabii (S.A.W) Hudaibiyyah chini ya mti maarufu nao ni mti wa samura **{basi Allah alishelewa yaliyomo kwenye nyoyo zao}** miongoni mwa ukweli katika vita, uvumilivu na utekelezaji wa ahadi, na idadi yao ilikuwa elfu moja na mia tano au tatu hivyo akashusha utulivu juu yao na dhamiri ni kwa ajili ya waislamu. **{na akawalipa ukombozi uliokaribu } yaani Ukombozi wa Khaibar.**[27]

Amesema Allah Taa'la :{Kamwe hawawi sawa miongoni mwenu yule aliyetowa kabla ya Ukombozi na akapigana huyo ni mwenye malipo makubwa kuliko wale ambao wametowa baadae na kupigana na wote –hao- Allah amewaahidi mema na Allah kwa munayoyafanya ni mwenye habari }[Al Hadiid :10]

27

Tafsiir Jaamii'l Jawaamii',na angalia :Muqtanyaaud Durar,Taqriibul Qur-aanil Kariim

Amesema Sheikh Muhammad As Sibzawnaary An Najafy

{Kamwe hawawi sawa miongoni mwenu yule aliyetowa kabla ya Ukombozi na akapigana huyo ni mwenye malipo makubwa kuliko wale ambao wametowa baadae na kupigana na wote –hao- Allah amewaahidi mema na Allah kwa munayoyafanya ni mwenye habari} [Al Hadiid :10]

{kamwe hawaai sawa miongoni mwenu} { yule aliyetowa} toka kwenye mali yake kwenye njia ya Allah { kabla ya Ukombozi na akapigana} namakafiri, kwani **{huyo ni mwenye malipo makubwa kiliko wale ambao wametowa baadae}** yaani baada ya ukombozi wa Makkah Allah, hivyo kutowa kwa ajili ya Jeshi la kiislamu pamoja ma Jihadi kabla ya fat-h, ni malipo makubwa mbele ya Allah kuliko kutowa kupigana baadae**{ na kupigana na wote –hao- Allah amewaahidi mema}**yaani amewaahidi hawa kuwapa Pepo hata wakizidiana kwenye daraja yake **{ na Allah kwa munayoyafanya ni mwenye habari }** yaani ni mjuzi kwa kila munalolifanya na kamwe hafichiki na chochote katika hali, matamshi ,kutowa na Jihadi, bali yeye ni mjuzi zaidi kwa matendo na nia zenu zote .

Na Kwa hakika Allah Taa'laa ameamulia Pepo kwa yule aliemuahidi mema kwa kauli yake**:{Hakika wale ambao yametangulia kwao mema toka kwetu hao ni wenye kuwekwa mbali na Moto. Kamwe hawasikii suti yake na hao watakuwa humo milele, kwenye kile kinachopendwa na nafsi zao kamwe, hawatohuzunishwa na na fazaa kubwa .}**

Amesema Abuu Jaafar Atuusy ;

{Hakika wale ambao yametangulia kwao mema toka kwetu}: yaani :ahadi ya Pepo.. akasema "Allah akatowa habari kwamba katika sifa hizi ni kuwekwa mbali nao na pepo."[28]

Na kama hali ilvyokuwa ya shida na dhiki juu ya masahaba kabla na wakari wa Suluhu Hudaibiyyah,vita vya Tabuuk vimetofautika na vyengine kwa kubainisha hali ya inayoweka wazi wanafiki toka kwenye wenye ikhlasi katika Madina**,** na katika kipindi cha wakati

28 Tafsirut Tibyan,Tafsiiril Jadiid:kwenye tafsiiri ya (Suratl Anbyaa)

wenye hadaa kwenye nyoyo za baadhi ya watu, pale Qur-ani ilipokuja wazi wazi katika hilo, hivyo akasema kuhusiana na Masahaba(r.a) ambao walitoka pamoja na Mtume (S.A.W) kwenye vita vya Tabuuk :**{ Kwa hakika Allah amemsamehe Nabii na Muhajirina na answaar ambao walimfata kwenye wakati wa shida baada nyoyo za kundi miongoni mwao na akawasamehe hakika yeye kwao wao ni mpole mwingi wa rehema}**
[At Tawbah :17].

Amesema Seyyid Muhammad Taqiyyul Madrasy:
{ Kwa hakika Allah amemsamehe Nabii na Muhajirina na Answaar} tawba ya allah juu ya Nabii inamaanisha ziada kwenye baraka zake juu yake, ila kuhusiana na Muhajirina na Answaar inaweza ikamaanisha kusamehewa makosa yao ,lakini kwanini na kwa vipi wamesamehewe madhambi yao ? kwasababu wao walimfuata Mtume (S.A.W) katika wakati wa shida, na hivyo ni kwa sababu hiyo ilikuwa kazi kubwa na Allah (S.W) husamesamehe madhambi madogo kwa sababu ya mema makubwa, kwa hivyo Aya ikatilia nguvu uhakika huu **[ambao walimfata kwenye wakati wa shida**}hivyo subira kwenye wakati wa shidani amali kubwa sana Allah anayosamehea kwa sababu yake makosa madogo mengine[29]**„**

Amesema Sheikh Ttw'ibrasy :
Mtume(S.A.W) alijiandaa kwa ajili ya vita na Waromu mwezi wa Rajab na akayaandikia makabila ya Kiarabu miongoni mwa walioingia kwenye Uislamu na kuwapelekea wajumbe kuwahamasisha juu ya Jihadi na vita basi mpaka alipojiandaa kwa ajili ya kutoka alisimama kuhutubia akamshukuru Allah na kumsifu ,akahamasisha juu ya kusaidia na kumtia nguvu dhaifu na kutowa ,basi ikawa wa mwanzo alietowa ni Othman bin Affaan,aliekuja na vyombo vya dhahabu na fedha akavirusha kwenye mapaja ya Mtume (S.A.W), akwaandaa watu miongoni mwa wenye udhaifu, nae ndie aambiwae :kwamba yeye aliandaa Jeshi la shida na Abbaas akaja kwa Mtume (S.A.W) akatowa utoaji mwema na akaandaa, nao Answaar wakakimbilia kwenye utoaji nao Abdul

29 Tafsiirul min Wah'yil Qur-an, Tafsiiril Jadiid,(Suratit Tawbah:117)

rahmaan ,Zubir na Tw'alha wakatowa, nao watu katika mwa wanafiki wakatowakwa ajili ya kujionyesha na kusikilizika."[30]
Hivyo kila yaliyotangulia miongoni mwa Aya na riwaya madhubuti zinatosha na zinaweka wazi hadhi ya ya kundi hilo waliotowa kila kitu katiaka kuinusuru Dini ya Allah (S.W) na kunyanyua cheo cha Mtume (S.A.W) .
Na mwenye kufatilia kauli za maulamaa wanaowapenda Ahlil Bait wa Nabii (S.A.W), punde iliyopita ,na akangalia kwa jicho la kiakili na kwa mwangaza wa insafu, itambainikia kwake fadhila za kundi hilo lililobarikiwa lenye matendo ya ikhlasi yenye kuangaziwa kwa Nuru ya Unabii kutokana na kukamatana kwao na Sunna ya Mustafa (S.A.W), hivyo vizito viwili vimeshuhudia cheo hichi cha hali ya juu .

MLANGO WA TATU

Vipi fitina baina ya Masahaba(r.a) ilizuka?:

Baada ya kubainisha riwaya zinazojulisha ubora wa Masahaba (r.a) na zinazodhihirisha ukubwa wa cheo chao -kwa fadhila za Allah(S.W) – mbele ya maimamu na maulamaa na hayo ni kwenye Aya za Qur-ani na aya zilaonukuliwa toka kwa I'trah (a.s), akili za kundi katika waislam ulitakimbilia kujiuliza masuala muhimu; Vipi mtafaruku na tofauti ilitokea baina ya Masahaba(r.a) amao ndio wenye ubora na ufataji wa Dini ya Allah?

Kwanza wa mwanz o –moto wa - fitina baina ya waislamu:
Huenda maisha mazuri yaliyoitukuza jamii ya Masahaba(r.a) wingi wa kombozi zilizobarikiwa na kushinda kukubwa juu ya maadui wa Allah kuanzia kufukuzwa kwa mayahudi itatoka kwenye ardhi ya Bara Arabu, kukfatiliwa na kipindi cha kung'oka

[30] Angalia 'ilaam:uk.121, Bih'aarul Anwaar(244/21)

kwa kiti cha enzi cha Fursi na uingiaji wa makundi mapya kwenye dini ya kiislamu na kuishi pamoja na waislamu huku wao wakiwa watu wa fikra na tamaduni -za dini - zilizotangulia ambazo bado hawajajing'oa toka kwenye akili zao,walipata udongo wenye mbolea kwa kupandia mipasuko na mifarakano kwenye safu za umma wa kiislamu.

Pamoja na yalipita kubainshwa kwake mongoni mwa maisha mazuri na wingi wa kombozi .yote hayo hayakuwa mazuri kwa watu wa matamanio ya nafsi, wakajaribu kupanda mbegu za njia za mfarakano kwenye jamii hii iliyobarikiwa ya kimfano na kujitahidi kuwasha moto wa mfarakano na uzushi kwenye dini ya kiislamu kwenye safu za Masahaba(r.a).

Hivyo maingilio ya mwanzo ya shari yakawa kuwasha moto wa fitna na upandaji wa mbegu za shubha kupitia kwenye uhadaaji wa nafsi ngonjwa,basi kadhia ya utiaji kasoro kwenye Masahaba (r.a) na Nabii Masahaba(r.a) (S.A.W) kukakamilika, iliwadhoofishe umoja wa Masahaba (r.a) na kufarikisha safu za waislamu na mtu mmoja alimwambia mtu mmoja alimwambia mtu mmoja alimwambia mtu mmoja alimwambia mtu mmoja alimwambia kudhoofisha nguvu yao.

Hivyo akawa alieyewalia ukuu wa jambo hili,na kunyanyua bendera ya njama hizo mbaya alikuwa Abdullahi bin Sabai, myahudi aliyehemua watu mwanzoni, kumuasi na -kwa kumuuwa Khalifa wa waislamu Othman bin Affaan, na baada ya hapo akafanyakazi ya kuzua juu ulimi wa Imam Ali (a.s), na kumnasibishia idadi kubwa ya kauli na itikadi za kiyahudi, na kuzipenyeza na kuzieneza baina ya wengi wa wapungufu wa nadhari , dhaifu wa imani na wapenda fitina.

Na pale cheche za bidaa hizi za hatari kuenea baina ya watu, na shetani kuwapambia amali zao , kauli zao zilifika kwenye masikio na kujua kwa Amiiril Mu-u-miniin Ali bin Abi Talib (a.s), basi akaghadhibika na kamwe hakuzembea wala kufumbia jicho maneno haya maovu, hivyo hakuwa na hatua yo yote ile ila kuchimbua mashimo, akakoka moto ndani yake na kutishia kumchoma moto kila ambaye hatorejea toka kwenye uzushi huu wa

hatari., hivyo akaunguza idadi kubwa miongoni mwao, na kuihamisha kaumu nyengine.

Majlisy amenukuu kwenye Bihaar yake kwamba mtu mmoja alimwambia Amiiril Mu-u-miniin Alibin Abi Talib (a.s): kwamba:" Kwenye mlango wa msikiti wapo watu wanadai kwamba wewe ni mola na mtume wao ! hivyo akawaita akwambia ole wenu ! hakika mimi ni mja wa Allah kama nyie, ninakula chakula, nakunywa vinywaji, basi mcheni Allah na murejee .

Hivyo wakamjia kwenye siku ya pili na ya tatu ,wakamwambia kama hivyo, basi (a.s) akawambia :Wallahi tubuni vyenginevyo nitakuuweni mauaji mabaya mno, akaagiza kombora na kuwa aletewe nyundo, akafukua mashimo baina ya msikiti na kasri akaagizia kuni akazirembea na moto ukiwemo na akawaambia hakika mimi nitakurembeeni au murejee! wakakataa akawarembea shimoni mpaka wakaungua .

Baadhi ya watu wake wamesema:"kamwe hakuwaunguza , ila alitia moshi tu juu yao (a.s) akasema:

"Pale jambo nilipoliona ni jambo baya
Niliwasha moto wangu na kuagizia kombora
Na nikachimba shimo na shimo
Na kombora linatowa linawaka muwako waajabu"

Hivyo ewe mpenzi msomaji tahadhari kuchukuliwa na fikra kwamba (mtu) shakhsiyya hii ilyopika njama hizi ilkuwa ni ya kubuni, au alikuja toka kwenye maneno yasiyo ya msingi, bali alikuwepo kwenye nyanja za kiislamu, akipanga na kufanya mikakati, na kwamba wanavyuoni hawakughafilika kubainsha hali yake, na kufichua siri zake, hivyo wametaja nafasi yake mbaya kwenye kufarikisha ukoo wa Kiislamu,ulio mmoja,akaeneza machafuzi ya hatari kwenye akili za wasio na elimu.

Saa'd bin Abdillahl Ash-a'ril Qummy (301H): amesema:" Kikundi hichi kinaitwa Sabaiyyah wafuasi wa Abdillah bin Sabai, nae ni Abdullahi bin Wahab Ar Raasiby Al Haddaany ,na akasaidiwa juu ya hilo na Abdillahi bin Hirsy na Ibin Aswad, nao ndio wafuasi

wake wakubwa, nae ndiye aliyekuwa wa mwanzo kudhihirisha kuwatowa kasoro Abubakri, Omar, Othman na masahaba na kujiweka mbali nao .[31]

2- An Nawbakhty (310 H):
Akasema watu wa Abdillahi bin Sabai nae ni katika waliokuwa wakidhihirisha kuwatowa kasoro Abubakr, Omar, Othman na MSahaba (r.a) na kujiweka mbali nao, na akasema hakika Ali ameamrisha, basi Aliakamchukua, akamuuliza kuhusiana na kauli yake hii, akakiri na akamuuwa, watu wakampigia kelele :" Ewe Aamiril mu-u-miniin hivi unamuuwa mtu anaelingania kupendwa kwa Ahlil Bait, kwenye utawala wako na kujitenga na maadui zako!" Basi akamuhamishia Madain, mpaka aliposema na mpaka Abdillahi bin Saba'i akatolea habari za kifo cha Imam Ali akamwambia yule ambaye amemueleza alimpa habari za kifo chake :umesema uongo lau ungekuja na ubongo wake kenye mabindo sabiini, na ukasimamishia mashahidi sabiini waadilifu juu ya kuuawa kwake tungejuwa kuwa kamwe hajafa wala kuuawa, na kamwe hafi mpaka atawalie Dunia.[32]

3-Al Kishshy (369H): Akasema kuhusiana na watu wa Abdillah bin Saba'i: :"Nimemsikia Aba Abdillah (a.s) anasema:Allah amlani Abdillah bin Sabai yeye amedai uungu wa Amiiril Mu-u-miniin(a.s) na -Wallahi - Amiiril Mu-u-miniin (a.s).ni mja wa Allah na Mtume wake, ole wake kwa alietuzulia uongo.na kwa kweli kaumu inatusemea tusiyosema sisi kwenye nafsi zetu, hakika tunajitenga nao.

Akasema vile vile:" Baadhi ya wenye elimu wameeleza kwamba Abdillah bin Sabai alikuwa myahudi akasilimu, na akamuunga mkono Ali(a.s),nae akiwa yuko kwenye uyahudi wake alikuwa akisema kuhusiana na Yashuuu' bin Nuun Musa kuwa aliusia kuwa na ghuluu ,[33] hivyo baada ya kusilimu kwake baada ya kifo cha M tume (S.A.W) akasema kama hivyo kuhusiana na Ali (a.s), nae

31 Al Maqaalaat wal Firaq(uk.20), Firaqi Shiia'h22)

32Angalia Rijaalul Kishshy:u (.107,108)

33 Kuchupa mpaka kwenye itikadi

ndye wa mwanzo kutangaza kauli ya kufaradhishwa kwa uimamu wa Ali (a.s) na kudhihirisha -baraa- kujiweka mbali na maadui zake, na kufichua wanaokwenda kinyume nae na kufuru yao, akadhihirisha ghuluu .

4-Sheikh Twaaifah Abu Jaafar At Tuusy (460) :Pale alipomuelezea Abdillah bin Sabai kwenye watu wa kitabu chake mlango wa watu wa (Ali(a.s)) akasema :Abdillah bin Sabai ambaye alirejea kwenye ukafiri akadhihirisha ghuluu.

Na imekuja kwenye hashiya ya kitabu hicho: Abdillah bin Sabai :Ni mwenye ghuluw mwenye kulaaniwa, alichomwa moto na Amiiril Mu-u-miniin Ali(a.s), nae alikuwa akidai kuwa Ali (a.s) ni mungu na yeye ni nabii.[34]

5- Al A'llaamah Ali Al Qahaaby:Kasema kwenye watu wa kitabu chake : Abdullahi bin Sabai ambaye alirejea kwenye ukafiri akadhihirisha ghuluu.

6- Al A'llaamah Al Arbily : Ni mwenye ghuluu mwenye kulaaniwa …na kwamba alikuwa akidai uungu wa Alina unabii wake.[35]

7- Myrza An Nuurilt tw'risy: Ameeleza kwenye kitabu chake Mustadrakul Wasaail katika mlango (Hukumu ya Ghulaat na Qadariyyah) riwaya toka kwa Ammaaris Saabaatw'y , amesema:" -baraa- kujiweka mbali Amiiril Mu-u-miniin (a.s) alikuja Madaain ,akafikilia ikulu ya Kisra , nae alikuwa pamoja na Dalf bin Mujeir mnajimu wa Kisra, basi mpaka Jua lilipopinduka wewe ni alimwambia Dalf simama pamoja nami mpaka aliposema:"na akaona fuvu lililochakaa, akawambia baadhi ya watu wake lichukuwe fuvu hili ikulu! nalo lilikuwa limerembewarembewa, akaja kwenye ikulu akaagizia kitasa akamimina maji kwenye kitasa akamwambia liweke fuvu hili kwenye kitasa, akasema (a.s):"Nakuapia ewe fuvu -uniambie- mimi ni nani ? na wewe ni

34 Jaami'ir Ruwaat (485/1)

35 Mustadrakul Wasaail(168/18), Madiinatul Ma'aajiz(226/1)

nani? Fuvu likasema : kwa lugha fasaha, nna kusema:”Ama wewe basi ni Amiiril Mu-u-miniin (a.s), na bwana wa wawekewa wasia, ama mimi ni mja wa Allah na mtoto wa kijakazi cha Allah Anushrawaan ” basi kaumu ikaondoka kwenda kwa watu wao nao [36]waliokuwa pamoja nae ni watu wa Sabatw’ na kuwapa habari kuhusiana na yale yaliyokuwa na kuyasikia toka kwenye fuvu, wakatofautiana na kukhtalifiana kwenye maana ya Amiiril Mu-u-miniin (a.s), na kumjia na baadhi yao na kusema kama walivyosema manasaara juu ya Masihi, mfano wa alivyosema Abdillahi bin Sabai na watu wake, hivyo watu wake wakamwambia :”**ukiwawacha kwenye kufuru hii!”** basi aliposikia hivyo akwambia:”mungependelea niwafanye nini ”wakasema “wachome kwa moto, kama ulivyomuuguza Abdillahi bin Sabai na watu wake”

Basi hivi ndivyo walivyofanya maulamaa -Allah awaghufirie- katika kuweka wazi ukweli kuhusu waharibifu na kauli zao kuhusiana na wachupaji mipaka waliozushia uongo, sumu na uchupaji mpaka kwenye Sharia hii yenye kubarikiwa, jee tutazingatia haki hii iliyowazi na yale waliyoyasema waliotangulia kwenye haki ya Amiiril Mu-u-miniin (a.s)?

Kuanza kwa fitina baina ya Masahaba (r.a):

Hakika kutokea kwa fitina na vita baina ya Masahaba wa Mtume (S.A.W) kulitokea baada ya kumalizika kwa njama alizoziwasha……

Na imekuja kwenye Abdillah bin Sabai myahudi kukiwa matokeo ya keneza na kutapakaza sumu na chuki baina yya wajinga na wenye imani dhaifu miongoni mwa waislamu wa miji mbali mbali, na hakika njama hizi zimeleta matunda yake maovu yaliyovunwa na mapepe kwa kumuasi Khalifa Othman bin Affaan (r.a) na kumuuwa kwenye nyumba yake Othman bin Affaan (r.a).

Na mambo yalizidi kuwa mabaya baada ya kustash-hid (kuuliwa) Khalifa Othman bin Affaan(r.a),pakaenea maovu ya shari kwenye safu za waislamu kutokana na kuenea kwa sumu yake,hivyo ni baada ya alipobayiiwa Ali bin Abii Talib kuwa

36 Nahjul BalaaghaH@UK. 243) , :Bih’aarul Anwaar (502/31).

Khalifa wa waislamu ,waasi hao wa kisabaiya walipenya kwenye safu za watu wa Madina na majeshi ya Kiislamu na hakukuwa kwenye uwezo wa.Imam Ali bin Abi Talib (a.s) katika wakati huo kuwatowa na kuwasafisha, na kulipiza kisasi cha Khalifa Othman bin Affaan (r.a) kwa ajili ya kuhofia kuenea kwa fitina na mauaji baina ya watu wa Madina, kama alivyofanya Khalifa aliedhulumiwa Othman bin Affaan(r.a).

Watu wa Madina walipotaka kuadhibiwa waliomletea shari Khalifa Othman bin Affaan (r. a) Imam Ali bin Abii Talib aliwaambia:"Enyi ndugu zangu hakika mimi sio kuwa sielewi nyie munachokielewa, lakini vipi nitakuwa na nguvu na waliokuleteeni balaa lao wao wanatumiliki, sisi hatuwamiliki, na hawa sasa watumwa wenu wanajiunga nao, waarabu wamevutika nao wamo baina yenu namna wapendavyo, na jee papo pahala munanapoona mimi naweza mnachokitaka? hakika jambo hili ni la kijahilia na kwa kweli watu hawa wanao msaada,-wanapoendesha jambo – dhidi ya mambo, kundi linaona munavyoona nyie na kundi linaona musivyoona nyie,na kundi halioni hili wa lile, hivyo vumilieni mpaka watu watulizane, nyoyo zikae kwenye nafasi zao, haki zichukuliwe kwa wepesi, hivyo nitulizieni, muangalie jambo langu lipi litakujieni, musifanye jambo la kutikisa nguvu ikaanguka na kupelekea unyonge na udhalili, na jambo hili nitalikamata kama ninavyolikamata,na nisipokuwa na budi basi dawa ya mwisho ni moto.

Tokea kipindi hicho fitina zilianza kutokota baina ya Masahaba wa Mtume (S.A.W) na zenyekupelekea kugawanyika kwao kwenye makundi makundi ,ijtihadi zilikuwa nyingi, hivyo kuna kundi lililoona uwajibu wa kufanya haraka ya kuchukuwa kisasi kwa wauaji wa Khalifa Othman bin Affaan (r.a) na jengine kuna uwajibu wa kungojea mambo yatulizikane kwa Amiiril mu-u-miniin, hivyo watu wa uharibifu na maovu wakapenya baina ya pande hizo zenye kufanya jitihada.

Na matokeo ya mtafaruku huu kamwe hayakutulizanisha mawazo yao, bali walichukulia fursa ya kila mnasaba kuwashia moto wa fitina na uovu, hivyo wakachukua fursa kutoka kwa kundi la Makkah kuelekea Iraki,wakakimbilia kuchochea mawazo kwamba

hakika wao walitaka shari na kusambaratisha safu za waislamu ..na pakatokea vita vya ngamia.

VITA VYA NGAMIA(Maa'rakatul Jamal):

Riwaya za kihistoria zinaashiria kwamba kamwe Talha, Zubeir na Ummul Mu-u-miniin Aisha pamoja na waliokuwa nao hakwenda Iraq kwa ajili ya kupigana, wala kudai au kuwa na tamaa ya kupora Ukhalifa toka kwa Ali(r.a) bali walitoka kwa ajili ya kufanya suluhu na kuondosha tofauti, na kuwakusanya waislamu kwa ajili ya kuunganisha umoja wao , na kulipiza kisasi kwa wauwaji wa Othman bin Affaan (r.a) na kuwatowa toka kwenye safu zao ndani ya Iraq, haya ndiyo yaliyoelezwa na vitabu vya Historia, na kamwe vita vya ngamia havikuwa vya mwisho , lakini baada ya muda vilifuatiwa na vita vya Swiffiin .

Tukio hili kubwa linaweza kufupishwa katika yafuatayo :
Pale wakati wa fitina baina ya jeshi la Ali na lile la Talha na Zubeir juu ya kuwatowa waasi hawa toka jeshini na kuuliwa ilipofika, kila safu ilibakia kwenye kambi yake, baada ya amri hii waasi hao walipinga makubaliano hayo matukufu ya safu mbili na utulivu, kwani ni makubaliano juu ya kuuliwa kwao, hivyo wakaenda mbio kutapakaza fitina baina ya majeshi mawili, na kuanzisha vita baina yao kwa njama inayifichua ujanja na hadaa zao, hivyo walipanga njama usiku kuuwa mtu mmoja toka kila kundi, ili kila kundi lidhanie kwamba limevamiwa na kundi jengine, na njama hii ilifichika kwa kila kundi, hivyo ikawa sababu ya kuripuka vita baina ya safu mbili .

Vita vya Swiffiin :

Vita vya Swiffiin havikuwa tofauti na vile vya Jamal kwa mwanzo na malengo yake, na kwa hivyo Maulamaa wa Historia wametaja kuwa sababu ya ikhtilafu na vita baina Ali na Muawiyah kule Swiffiin haikuwa kwamba Muawiyah alikuwa na tamaa ya kutaka Ukhalifah kama wanavyodai na kueneza wengi wa waandishi .

Kwani Muawiyah kamwe hakunyanyulia kichwa chake Ukhalifah, na kamwe hakubayii'wa na yeyote katika waislamu ,na hakupigana na Alikwamba yeye kwamba Muawiyah ni Khalifah, bali sababu ya tofauti baina ya Khalifa Alina kiongozi wa Shaam Muawiyah ni kwamba hakutekeleza lile aliloamrishwa na Khalifah wa waislamu la kumuuzulu toka kwenye ukuu wa Shaam na kumkubali yeye kuwa ni Khalifah .

Mua'awiyah alikuwa akitaka kutekelezwa kisasi kwa wauwaji wa Othman, Khakifa wa waislamu aliefanyiwa njama, na kwamba ilienea baina ya wakazi wa Sham kwamba Khalifa Aliamekataa kuwaadhibu wauwaji wa Othman pale alipokamata Ukhalifa na badala ya hilo akawapiga vita watu ngamiana, vile vile kuiwacha Madina na kuishi Kufa nayo ndiyo makazi ya wauwaji wa Othman na kwamba kwenye jeshi lake yumo mtuhumiwa wa mauwaji wa Khalifa aliyetangulia.

Na kwa ajili ya pupa la Amiril-miniin la kuweka wazi suala hilo, na kubatilisha suala hilo na kubatilisha madai yaliyokuwa yakienezwa ,na kwanini waislamu, alipeleka barua kwa Mua'wiya akimbainshia humo kuthibiti kwa Ukhalifa kama ulivyothibiti kwa walomtangulia pamoja na kuwa mbali na damu ya Othman (r.a) akasema:"Kwa hakika wamenibayi' kaumu waliomb-yii' Abubakri ,Omar na Othman juu ya yale waliyomfanyia mubaayaa, hivyo hakuwa kwa aliyekuwepo kuchagua ,wala asiekwepo kupinga, kwani shura ilikuwa ya Muhaajirina na Answaar, hivyo wanapokubaliana juu ya mtu na kumwita Imamu hilo linakuwa ni ridhaa ya Allah, basi anapoasi jambo hilo kwa kutukana au bidaa wanamrejesha kwenye lile aliloliasi, basi iwapo atapinga watampiga vita juu ya kufuata njia ya waislamu, na Allah atamtawalishia kile alichikikengeuka, naapa ewe Muaawiyah utakapoangalia kwa akili yako bila ya kuangalia matamanio yako ya nafsi utaniona ni mwenye kuepukana kutokana na damu ya Othman kuliko yeyote yule, na hakika utaelewa kuwa mimi nilikuwa kwenye kujitenga na damu ya Othman ila utakapokengeuka, basi hapo kulikudhihirikia nacho kitakengeuka., (Wassalam).

Hivyo basi mpaka vita vilipopamba moto bina ya safu za waislamu, na damu ikachuruzika baina yao, vita vilimalizika kwa jeshi la Muawiya(r.a) kunyanyua Msahafu wakitaka suluhu baina kwa vile anavyoridhia Allah A'zza wa Jallah hivyo, Khalifa wa waislamu Ali(r.a) akaliridhia ombi hilo na kurejea Kufah nae Muaawiyah akarejea Sham kwa sharti waliokubaliana pande hizo mbili.Amiril Mu-u-miniin Ali (r.a) alikielezea kisa hicho kwa miji mbali mbali na kutowa taarifa ya yale yaliyotokea baina ya waislam **{Na iwapo makundi mawili miongoni mwa waislamu}** na wao waliona kwamba wako kwenye haki .[37]

Hakika tofauti na fitina zilizotokea baina ya Masahaba wa Mtume (S.A.W) katika vita baina yao, pamoja na kuchupiana baina yao na yale yaliyotokea baina yao katika kufanya suluhu kwa yale yaliyoridhiwa na Allah (S.W), na kukubalika kwa suluhu hii na kila upande,kwani inatukumbusha kauli yake Taa'la **{Na iwapo makundi mawili miongoni mwa waislamu yatapigana basi suluhisheni baina yao, iwapo moja wapo litachupa mpaka juu ya jengine basi lipigeni vita lile lililochupa mipaka mpaka litakaporejea kwenye amri ya Allah, likirejea basi musuluhishe baina yao kwa uadilifu na mufanye uadilifu, hakika Allah anapenda waadilifu kwani waislmu ni ndugu hivyo suluhisheni baina ya ndugu zenu wawili na muogopeni Allah ili mpate kurehemewa}** [Al Hujraat:9-10]

Amesema Sheikh Muhammad Baaqir An Naaswiry kwenye Tafsiri yake:

{Na iwapo makundi mawili miongoni mwa waislamu} yaani iwapo makundi mawili miongoni mwa waislamu moja limepiga vita jengine {**basi suluhisheni baina yao}** na toweni wasaa katika kwasuluhisha { **iwapo moja wapo litachupa mpaka juu ya jengine** } kwa kutaka kisichostahiki,na kupigana kwa dhuluma **{basi lipigeni vita lile lililochupa mpaka}** kwani ni dhalimu { **mpaka litakaporejea kwenye amri ya Allah** }mpaka

37 Tafsiiru Majma'ail Bayaan (308) na vile vile angalia Tafsiiril 'ain ,Bayaaniis Sa'adah , Tafsiirul Muqtanayaatid Durar,Al Miizaan ,Al Kaashif fii Tafsiiril H'uraat(9-01).

litalkaporejea kwenye utiifu wa Allah na kuwa kuchupa mpaka na dhuluma likirejea na kutubu basi rejeeni kwa kufanya suluhu baina yao **{ kwa uadilifu}** bila ya kuelemea upande wowote ule **{ na mufanye uadilifu}, {kwani waislmu ni ndugu }** katika Din suluhisheni baina ya makundi mawili, mumsaidie mwenye kudhulimiwa na mumuondoe dhalimu toka kwenye dhuluma yake.

Na jitihada za juu ya suluhu na ya kuwakusanya waislamu waliotofautiana lilikuwa ndio tarajio la Amiril Mu-u-miniin Ali (r.a) ,hivyo kwa mbali na toka kwenye kila kinachowatia waislam kwenye kuchukiana na kutofautiana, hivyo Amiiril muuminina alifanya jitihada kuwatenga waislamu toka kwenye kila kilichochochea chuki na mfarakano kwenye safu za waislamu na katika hayo :ni kauli mbaya, hivyo aliwakataza waliokuwa kwenye jeshi lake wasitukane wala kulaani jeshi la Muaawiyah bin Abi Sufiyan, pamoja na kutokea vita baina yao.[38]

Hivyo toka kwa Abdillahi bin Shariik amesema:"Hijr bin Ady na Omar binl Hamq walitoka wakidhihirisha kujitenga na laana kwa watu[39] wa Shaam, hivyo Aliakawapelekea ujumbe :"kwamba wacheni hayo yaliyonifika toka kwenu kuhusiana nanyi, ,hivyo akawaendea akawambia wakamwambia :"Ewe Amiril muu-minin jee sisi hatuko katika haki ? akasema:" ndiyo. Wakasema :" Jee wao sio madhalimu ? akasema ndiyo .Wakasema:" hivyo kwanini unatuzuwia kuwatukana ?akasema :" Nimechukizwa nanyi kuwa ni watukanaji walaanifu, lakini lau mngetaja amali zao,mkasema katika mwendo wao ni kadha wa kadha, kwenu ingekuwa sahihi zaidi, na ukomo wa kujiondolea udhuru, na pahala ili kuwalani na kujiweka mbali nao mkasema: Ewe Mola zihifadhi damu zao na zetu na kumwagika, tusuluhishe baina yetu na wao na waongoze kutokana na upotovu wao, mpaka haki ieleweke kwa asieielewa, na aachane na uchupaji mpaka na uadui kwa anaeyatenda, hili lingekua zuri zaidi kwangu na kheri kwenu "[40]

38 Bih'aarul Anwaar Angalia ()Bih'aarul Anwaar(561/32) Nahuj Balaaghah (uk.323),

39 Kwenye asili :miongoni mwa watu wa Sham.

40 Musdrakul Wasaail(306/32)Bihaarul Anwaar :(399/32) ,Waq'qtul Wasaail (uk.102)

Katazo hili litokalo kwake(a.s) halikuwa maalum kwa kundi lake tu, bali alilidhihirisha na kuliusia jeshi lake (a.s)akikusudia kuchanganya kila wakati na pahala,hivyo akaliambia jeshi lake katika Swiffiin vile vile: “Nimechukizwa nanyi kuwa ni watukanaji walaanifu, lakini lau mungetaja amali zao, mkasema :katika mwendo wao ni kadha wa kadha,kwenu ingekuwa sahihi zaidi, na ukomo wa kujiondolea udhuru, na pahala pa kuwalaani na kujiweka mbali nao mkasema:Ewe Mola zihifadhi damu zao na zetu na kumwagika, tusuluhishe baina yetu na wao. ". [41]

Baada ya kuuliwa Imam’Ali (a.s):

Na baada ya kuuawa kwa Amiiril Muuminiin Ali (a.s) kwa kuwa shahidi kwenye mikono ya Khaarjii mwenye hila Ibn Muljim alimbayi’i mwanawe’ Husein (a.s) kwa ajili ya Ukhalifa wa waislamu, hivyo hakuwa na hatua yoyote ya kuchukwa ila kukusanya safu za waislamu , na kuhakikishika miujiza ya Nabii (S.A.W) .

Hivyo toka kwa Abubakri ibn Alharith Athaqafy amesema :” Nilimuona Mtume (S.A.W) na Hasan bin Ali (a.s) yupo kwenye ubavu wake na huku akiwaelekea watu mara hii na mara nyengine akimuelekea yeye, huku akisema "Hakika mtoto wangu huyu ni bwana na huenda Allah akayasuluhisha makundi mawili makubwa miongoni mwa waislamu kwa sababu yake.”[42]
Imam Hasan bin Ali.(a.s) alifanya moja ya masharti ya suluhu pamoja na Muawiyah (r.a) kuwa ni kuamua kwa watu kupitia Kitabu cha Allah (S.W)na Sunnah na juu ya mwenendo wa Mkhalifa waongofu.[43]

Na katika yanayojulisha juu ya mshikamano wa udugu na kurehemeana wa kidini baina ya Amiril Mu-u-miniin Ali na Muawiyah (r.a) -pamoja na hayo yaliyokuwepo baina yao katika tofauti za kijitihada – ni kwamba Muawiyah (ra.)alikuwa kila

41Bih’aarul Anwaar(561/32) Nahuj Balaaghah (uk.323),

42 Kashful Ghummah(519/1), Bih’aarul Anwaar (298/42),’Awaalil La-a-ly(102/1)

43 Angalia Kashful Ghummah(570/1),Bih’aarul Anwaar(64/44),

napomtaja Ali baada ya kustashhidi kwake akilia kutokana kumkosa kwake na kumrehemu.

Toka kwa al Aswbagh bin Nabaatah amesema:"Dhwiraar bin Dhwamuratin Nahshaly aliingia kwa Muawiyah bin Abi Sufiyan (ra.) akamwambia nisifie Ali ! akmwambia: "Jee unijejea?akamwambia hapana, bali nisifie.

Dhwiraar akasema:"Allah amrehemu Ali- Wallahi - alikuwa kama mmoja wetu, hutukaribia tunapomfanyia ziara, kamwe hatufungii mlango, wala kutuzingia bawabu ,-Wallahi –pamoja na kujikaribisha kwetu na ukaribu wake kwetu kamwe hatumsemeshi nkutokana na haiba yake, na hatujidhihirishi kutokana na utukufu wake, anapotabasamu basi ni mfano wa luklu iliyotungwa .

Muawiyah (ra.) akasema:"Nizidishie katika zifa zake.Dhiraar akasema :"Allah amrehemu Ali Wallahi alikuwa mrefu wa kukesha, mchache wa kulala, akisoma Kitabu cha Allahusiku mzima na kwenye pembe za mchana..

Akasema Muawiyah (ra.) huku akilia "inatoshelelza ewe Dhiraar! Wallahi hivyo hivyo ndivyo alivyokuwa Ali, Allah amrehemu Abalhasan"[44]

Hii ndiyo hali ya udugu katika zama zilizopita, kamwe tofauti katika jitihada haikuwazuwia kurehemeana na nyoyo zao kuepukana na chuki na choyo, na historia ni kisaidizi kikubwa kwa kufahamu matukio ya zama zilizopita, iko mbali na maneno na huruma za mamba zenye kurembea muislam kwenye kila uovo, na baada ya hapo hakuna chochote isipokuwa upotovu wa shetani na shubuhati zake, Allah atukinge na upotovu huo-.

[44] Bih'aarul Anwaar(14/41),Amaalis Swiddiiq (624)

MLANGO WA NNE :

NJAMA DHIDI YA UISLAMU NA WAISLAMU

Mustashrikina[45] na wale waliohadaika nao wanayafanya yale yaliyotokea baina ya Masahaba wa Mtume (S.A.W) kwenye kipindi cha fitina miongoni mwa khitilafu na kupigana kuwa ni sababu na tundu ya kupenyea kuwatukana, na kuchafua uadilifu wao

Baadhi ya matusi haya yametokea toka kwa waandishi wa kale na wasasa miongoni mwa wale wanaohadaika kwa kauli na toka kwa wale wanaocheza ngoma wasioijuwa, wanaosema wasiyoyajuwa hivyo wakafanya nafsi zao ndio mahakimu baina Masahaba wa Nabii (S.AW). wakiwafanya sahihi wengine na kuwakosoa wengineo bila ya dalili na hoja, hawana njia isipokuwa kufuata kiupofupofu watu wa istishraki.

Na hivyo waandishi hao katika kupaka matope kitarekhe wamejifanyia ili kutilia nguvu batili na maneno yao maovu, na kupanda fitina na bughudha baina ya waislamu, na miongoni mwa sababu hizo ni :

Kwanza :Kuporomosha uadilifu wa Masahaba:

Watu wa istishraki wamerembea shubuha mbaya sana yenye athari ya hatari kwenye dini yetu na miongoni mwao ni:

Hivi kweli inaingia akilini mtu kuchukuwa katiba yake madhubuti na mfumo ulionyooka unaokwenda sambamba na Qur-an tukufu toka kwa watu waliotokewa na matatizo na kwamba mtu hana imani na hali za mienendo yao?

Hivyo basi panaporembewa mfano wa sumu na shubuhati hizi kwa waislamu wasiokuwa na elimu, kwani mwenye kuirembea kamwe hakukusudia kumtuhumu Sahaba wa kishamba ambaye historia haikuelezea habari yake, au kwenye athari yake au Sahaba katika Masahaba wa kawaida aliezini, akakiri akarembewa mawe

45 Mustashrikina: Watu wanaosoma elimu za Mashariki (pamoja na Uslamu) kwa malengo mbali mbali likiwemo la kupaka matope.

na Nabii (S.W.A), au katika mtu aliepata mtihani wa kunywa ulevi akasimamishiwa hadi na-kutubu-,wala kwa shubuha yake hiyo hatakii mfano wa Khatib bin Abii Baltaa'(r.a) alieteleza na kutosibu kwenye rai yake,alipowapa Makureshi habari ya kuwasili Mtume (S.A.W) kwa ajili ya Ukombozi, kwani wote hao (r.a) walitubu kwa Allah (S.W,) ima kwa kustaghafiru au kwa kusimamishiwa hukumu juu yao.

wakubwa kupitia kwenye uzushi ya kuzima Nuru ya Allah (S.W) kwa kuzua visa kuhusiana na wao, na kudhihirisha khilafu baina yao na baina ya wengine ili kutandika njia kwa ajili ya kuzima Nuru ya Allah (S.W.) iliyo bayana .

Waliokwendea juu yao waislamu kwa kuporomosha uadilfu wa Masahaba na tokea hapo ili kuwawepesikia kugonga Kitabu cha Allah, walichokihifadhi na kukinukuu, na baada ya hapo Sunna ya Mtume wake Muhammad (S.A.W, ambayo ndani yake muna uboreshaji wa Sharia za Kiungu, ili baada ya hapo iwawepesishie usambaritishaji safu za Uislamu na waislamu, kufanya fitina na chuki zenye kuendelea baina yao.

Na linaonekana katika yale yanayoenezwa baina ya waislamu miongoni mwa upenyezaji na uenezaji wa hadithi za uongo juu ya Masahaba wa Nabii (S.W.A) zilizoenea kwenye vitabu vilivyokusanya hadithi na riwaya mbali mbali.
Ajabu kubwa ni kwamba hatukupata riwaya yoyote inayojulisha mfarakanonakhtilafubainayaMasahaba
(r.a) iliyo sahihi, yenye kunukuliwa kwa sanadi toka kwa waadilifu ambayo inategemezewa mfano wa madai hayo.
Lakini juu ya bayana na elimu :

1- Hakika sifa juu ya Masahaba zimepatikana kwenye Kitabu cha Mola wetu, na kwenye Sunna ya Nabii wetu Muhammad (S.W.A) .na hivyo hivyo kwenye ndimi za I'trah (s.a) [46]
2- Hakika Kauli (Hakika mingoni mwa Masahaba) wamo wanafiki ni uongo, kwani wanafiki sio katka Masahaba

46 Angalia (uk.) za kitabu hichi.

kimsingi na wanafiki wengi wao walikuwa maarufu kwa Nabii (S.W.A) na Masahaba, kwa uainisho na sifa zao.kwani Aya za Qur-anzimebainisha kila harakati na utulivu wao, bali hata myenendo ya nafsi zao

3- Kwa mfano vita vya Tabuuk ambavyo ndivyo vita vya mwisho vya Mtume (S.A.W), tunaona kwamba wapo waliowacha kwenda kwa nyudhuru zisizokuwa na msingi, kwa madai ya kuhofia kufitinika na wanawake wa Kirumi na nyenginezo dhaifu ambazo kwa kawaida wanafiki hutolea nyudhuru pale panapokuwa na Jihadi katika njia ya Allah .

Qur-ani imetaja katika mwahala tofauti pale Masahaba (r.a) wengi wao walipotoka pamoja na Mtume (S.A.W) na kamwe hakuna aliyebakia Madina ila mtu ambaye unafiki wake uko wazi, mwenye udhuru aliomsamehea Allah (S.W) kwo au alopewa idhini na Nabii (S.W.A) kubakia au kutokwenda.

Na mingoni mwa yanayojulisha kwamba wanafiki mabo yao yanajiliana na kwamba wao sio katika Masahaba (r.a), ni kwamba kwamba Allah (S.W) alitaja toba ya watu watatu miongoni mwa watu wa Madina wasiokwenda bila ya udhuru wa kisheria, na hivyo ni kwa sababu ya ukweli wa kutubu kwao na nguvu ya imani yao na kuilezea hali yao wakati wa kenda kinyme na kutotoka pamoja na Mtume (S.A.W). kwa kauli yake Taala:**{ Kwa hakika AllahameshawasameheNabiinaMuhaajirinana Answaar}[**[AtTawbah :117]

mpaka..**{na juu ya watatu ambao walikwenda kinyume mpaka ardhi ilipokuwa nyembamba nao pamoja upana wake na wakabanwa na nafsi zao mpaka wakawa na uhakika kwamba hakuna marejeo toka kwa Allah ila kwake, na akawasamehe ili wao watubu, hakika Allah ni Mwingi tawbah na mwingi wa rehma}** [[Attawbah :118] –hivyo Allah amewatowa kwenye - wanafiki kwa kutokwenda kama vile Imam Ali(a.s) na Ibn Ummi Maktum, na lile kundi la mafakiri ambalo halikupata cha kujikimia kwenye kutoka.

Hivyo Aya Tukufu za Surat Tawbah kwenye Aya ya mwanzo zimebainisha kwamba Arrahmaan amewasamehe Masahaba (r.a) walioshuhudia vita na kwenye Aya ya Pili kuwatowa wanafiki toka kwenye jamii ya Madina, wale waliokuwa hawakwenda nalo ni kundi la pili.

Allah (S.W) akatuelezea habari ya watu watatu wasiokwenda vitani miongoni mwa Masahaba (r.a), na kwamba Allah (S.W) ameshawasamehe kwa sababu ya ukweli wao nalo ni kundi la mwisho .

Hivyo basi upo wapi unafiki wa watu hao , pamoja na uwazi unaojulisha juu ya ukweli wa yaliyotokea.
Bali Masahaba (r.a) walikuwa watu wenye khofu zaidi kwa Allah (S.W) ili wasijeangukia kwenye unafiki.

Toka kwa Salaami bin Mustaniir amesema:"Nilikuwa kwa Abi Ja'afar (a.s), akaingia kwake Hamraan bin Ayun akamuuliza kuhusiana na mambo fulani, mpaka H'amraan alipotaka kundoka akamwambia Abaa Jaafar:"Tupe habari –Allah akurefushie kubakia kwako kwetu atuburudishe kwasababu yako –hakika sisi tunakujia na hatuondoki toka kwako mpaka nyoyo zetu zilainike na nafsi zetu ziliwazike toka kwenye Dunia na kutuwepesishia yaliyoko kwenye mikono ya watu miongoni mwa mali hizi, baadae ndio tutoke kwako, hivyo tunapokuwa pamoja na watu na matajiri tunaipenda dunia .Akasema Abu Jaafar (a.s) "Hakika hizo nyoyo mara huwa ngumu, na mara nyengine hulainika, na Abi Ja'afar (a.s) akasema " Ama hakika Masahaba wa Mtume (S.A.W) walisema:" Mtume wa Allah,-hakika–tunaogopa unafiki akasema "kwanini munaogopa jambo hilo?" wakasema:"Hakika sisi tunapokwa pamoja nawe ukatukumbusha na kuhamasisha huogopa, na husahau Dunia na huipuuza, mpaka tukawa tunaona Akhera, Pepo na Moto nasi tupo kwako, basi tunapoondoka toka kwako na tukaingia nyumba hizi tukanusa watoto na kuona familia, wake na watoto, hali zetu tulizokuwa nazo tukiwa pamoja nawe hukaribia kugeuka, mpaka –tukahisi –hatukuwa pamoja nawe, hivi basi jee unahofia hili kuwa ni unafiki ? Akasema Mtume (S.A.W):"La sivyo hakika ni hizi ni katika hatua za shetani ili akuhamasisheni kwenye dunia, naapa na Allah lau nyie mungedumu kwenye hali hii iliyoelezewa na nafsi

zenu -basi- Malaika wangekupeni mikono, na mungekwenda juu ya maji, na lau nyie musingekuwa munafanya madhambi mukataka maghufira kwa Mola wenu -basi – Allah angeumba viumbe vyengine wakakosea na wakataka maghufira, akawasamehe, hakika muuini ni mwenye kufanyiwa mitihani mwenye kutubu- kwani hukusikia **{Hakika Allah anawependa wenyekutubu –kwa wingi-na anawapenda wenye kujitoharisha –kwa wingi - }** [Al Baqarah:222] na Allah akasema:**{Mtakeni maghufira Mola wenu }**[Huud:13] [47]

Hakika Masahaba (r.a) ni wenye kukingwa kufanya makosa kwa umoja- kukubaliana –kwao, hivyo haiwezekani kukubaliana juu ya jambo katika madhambi makubwa au madogo wakalihalalisha na kulifanya, ama kutokea maasi toka kwa baadhi yao basi hiyo ni dalili juu ya kutokuwa wao ni maasum –wenye kukingwa kufanya makosa-kwa mmoja mmoja wao, na kamwe kuteleza huku hadhurishi kwenye uadilifu wao, wala kuporomosha cheo chao.

Ama katika yanayojulisha uadilifu wao kwa ujumla wao, ni kule kushughulikia Maimamu (a.r) katika uchunguzi wa riwaya za Masahaba (r.a) walizozisimulia toka kwa Mtume(S.A.W) na kwamba baada ya upekuzi mkali na uangalifu hawakuona
Sahaba yeyote (r.a) aliyesema uongo japo mmoja juu ya Nabii (S.A.W), na pamoja na kuenea kwa bidaa kwenye mwisho wa kipindi chao kama vile bid-a ya Qadariyya, Khawarij na Murjia, ambazo vianzio vyake ni akili ngonjwa na kuharibika kwa rai, ila kwamba milele hakupatikana Sahaba hata mmoja kwenye wazushi hao, na hili linajulisha kwamba Allah (S.W) amewateua na kuwachunga ,akawatofautisha na wengine, na kuwachagua kwa ajili ya Nabii (a.s)

Amesema Abu Abdillah (a.s): Masahaba wa MtumeS.A.W) (r.a) ni elfu kumi na mbili elfu wametoka Madina, elfu mbili toka Makkah na elfu mbili katika waachwaji huru, na kamwe hakuonekana kati yao Qadary, Murjii, Haruury, Muutazila wala watu wa rai,

47 Al Kaafy :(432/2)Bihaarul Anwaar: (41/6) Tafsiiril ‘Ayyaashy:(109/1) Majmuua’t Warraam :(21/2)

walikuwa wakilia usiku na mchana, wakisema:”-Ewe Mola tuondolee roho zetu kabla hatujala mkate wa hamira.”[48]

Hakika Imam Saadiq (a.s) methibitisha uadilifu wa Masahaba Nabii (S.A.W) (r.a) juu ya ukweli ya yale wanayiyaona kwenye hadithi zao za Nabii (S.A.W).

Toka kwa Mansour bin Hazim amesema:”nilimwambia :” Abi Abdillah (a.s):Kwanini nikikuuliza masuala unanijibu kwa jibu, na anakujia mwengine unamjibu kwa jibu jengine? akasema:”Hakika sisi hujibu juu ya ziada na upungufu !”akasema Nikasema "Basi nipe habari kuhusiana na Masahaba wa Nabii (S.A.W) wamesema kweli au wamesema uongo?'akasema nikamwambia wananini mpaka wakatofautiana "akasema hivi wewe hujuwi kwamba mtu anamjia Mtume (S.A.W) akamuuliza masuala akamjibu kwa majibu, baada ya hapo akamjibu kwa lile lililofuta jibu hilo, hivyo hadithi zinajifuta zenyewe kwa zenyewe”[49]

Lau atakuja mwenye kudai juu ya kutokea kwa uongo kwenye Masahaba (r.a) au kutokea kwa unafiki kwenye nyoyo za moja kwa moja angeambiwa :”Hivyo basi iko wapi dalili ya wazi juu ya kuwatowa hawa toka kwenye dai hili ?

4- Uadilifu wa Masahaba (r.a) haupelekei isma-kkukingwa-kwao kutokana na makosa kwani wao ni wanadamu wanakosea na kusibu, ila tukwamba makosa yao yamezamishwa kwenye bahari za mema yao.

Kwani wanayo waliyoyatanguliza mema na fadhila zisizofikiliwa na yeyote, kwani ni wao waliomnusuru Nabii (S.A.W) pale walipokusanyika juu ya Waarabu, wakapigana kwa mali, watoto na nafsi zao, wakawapiga vita mababa, makaka na jamaa zao na kutowa shingo zao kwa ajili ya kunyanyua Neno la Allah, na ikawa ndiyo sababu katika kueneza na kufikisha kwetu

48 Al Khiswaal:(639/2), Bihaarul Anwaar :(305/22)

49 Al Kaafy : (65/1), Bihaarul Anwaar :(228/2)

Dini hii Tukufu, hivyo hili –kwa idhini ya Allah – hupelekea msamaha uliotoka kwao, na hata yangekuwa ni madhambi makubwa madhali hayajafikilia kufuru.
Bihaarul Anwaar

Amesema Taalaa:**{Hivyo kwa sababu ya rehema toka kwa Allah, umelainika kwa kwao na lau ungekuwa mkavu wa moyo hakika wangelikumbia wale waliokuzunguka hivyo wasamehe ,uwatakie maghufira na uwashauri katika jambo – linalohusiana na Uislamu au jamii -, hivyo ukiazimia jambo basi mtegemee Allah hakika Allah huwapenda wenye kutegemea kwake }**[Aal I'mraan :159]

Amesema Al Majlisy :"Uondokapo uadilifu kwa kwa kufanya jambo linalotia ila, basi hurejea kwa toba bila ya tofauti ilyodhahiri ,hivyo hivyo aliyesimamishiwa hadi na akatubu uadilifu wake na ushahidi wake unakubalika, na baadhi ya watu wa madhehebu wamenukuu kukubaliana tofauti juu ya jambo hilo."[50]

Na amesema Seyyid Abul Qaasimul Khawny:" Uadilifu huondoka mara baada ya kufanya maasi, na hurejea kwa toba na kujuta, na kwamba hapatofautishwi baina dogo au kubwa katika hilo"[51]

Na akasema Seyyid Muhammad Husein Fadhlulah kuhusiana na uadilifu wa maimamu wa wakati wa sasa na ambao ni wenye hadhi ndogo zaidi kuliko wale Allah aliowakirimu usuhuba wa Mtume(S.A.W) (uadilifu sio na isma, muislamu muadilifu anaweza akakosea na akatubia baada ya kutanabahi kwake kwa kosa hilo, juu ya mwongozo wa Kauli yake Taala **{Hakika wale amabao wanamcha –Allah- wanapokumbwa na kundi la shetani hukumbuka basi mara wakajiona ni wenye kunusuriwa}** [Al Aa'raaf :220]
Ama vipi uadilifu unathibit?

50 Minhaajus Swaali'hiin:(12/2)

51 Bihaarul Anwaar :(30/85)

Hivyo ni kwa mujibu wa tabia zake za ujumla kwenye jamii ,kiasi kwamba watu wanamuona ni mwenye kuongoka kwenye dini yake tabia zake za kibinafsi huthibiti kwa kuenea kwa kunakojulisha elimu au utulivu, na au kijamii yenye kuambatana na mipaka ya kijamii kama vile unavyothibiti kwa habari ya Thiqah – mwenyekukubalika -kwa sababu ya uadilifu wake, na habari za uadilifu wa fasiki hazina kima cho chote za kumfanya mtu kuwa ni muadilifu au kupinga uadilifu wake."[52]

Upakaji matope histori ya Masahaba (r.a) .
Kutokana hayo yaliyotanguia kubainishwa na kuelezewa kwake tunaelewa kwamba hakika madui wa Kiislamu miongoni mwa mustshrikina na wasambaratishaji wa umoja wa waislamu wametumia mikakati ya hatari na ya namna kadha ili kufilia malengo lao, ambayo ni kupaka matopekuu maisha na sira za Masahaba wa Mtume (S.A..W) na kuhalalisha njia zote za kufikilia lengo hili, katika mambo yaliyopelekea matokeo mabaya na mwisho wenye maumivu , kama vile kuhalalisha kuwalaani na kuwatukana.na kuwagandishia nao kwa kila baya .

Na ziada ya juu ya yaliyopita kutajwa katika mbinu chafu tunazidisha kuyabainsha na miongoni mwao ni:
1 -kuzusha visa, sawa viwe juu ya ulimi wa Sahaba mmoja au kundi la Masahaba.

2- Kufanya kazi ya kufanyia taawili matukio kwenye aya za Qur-an,na Hadithi sahihi, taawili za batili zinazokwenda sambamba na matamanio ya nafsi zao, itikadi na bid-a zao kama alivyosema Taa'laa
kwenye Kitabu chake Kitukufu **{ ni yeye ambaye amekuteremshieni miongoni mwao zimo Ayaat Muhkamaat nazo ndizo msingi wa Kitabu na nyengine ni mushtabihat,basi ama wale ambao nyoyoni mwao kuna upotevu hufata zile ambazo ni Mushtabihat ili kutafuta fitina , na kutafuta taawili na hakuna yeyote aelewae taawili zake ila Allah, na waliozama kwenye elimu. }**

52 Al Masaail Fiqhiyyah:(178/2)

3- Kujikita kwenye kudhihirisha makosa ya Masahaba (r.a) yaliyotokea kwao kutokana na ukaribu wao na mwanzo wa daawa na uislamu –kwa ujahili na kutothirika kwao kutokana na mwanzoni mwao na kubeza mema, kujitowa muhanga na Jiahadi yao kubwa, baada ya kuthibitika malezi na imani kwenye nyoyo zao .

4-Kushughulikia utungaji wa mashairi yanayokubaliana madai yao kwenye kueneza fitina zao baina ya waislamu na kuzitilia nguvu, na kuzinasibisha kwa watu mashuhuri ,

Kama zile zilizonasibishwa kwa Amiril Mu-u-miniin (r.a) kwa uongo na uzushi na mingoni mwa maneno na beti za mshairi.[53]

MLANGO WA TANO :

MSIMAMO SAHIHI (WA HAKI) TOKA KWA MASAHABA WA NABII S.A.W

Hakika msimamo sahihi kwa yale yaliyotokea baina ya Masahaba wa Mtume (S.A.W) ni msimamo wa kati na kati ulio mbali na kuchupa mpaka kwenye mapenzi au kuchukia, kama alivyosema Taalaa **{ Na hivyo hivyo nakufanyeni kua Umma wa kati na kati }**{Al Baqarah :143}

Hivyo wajibu juu yetu ni kuwafanya marafiki Masahaba wote wa Nabii (S.A.W), hasa hasa wale waliotangulia kwenye Uislamu miongoni mwa Muhaajirina na Answaar, na hivyo hivyo wale waliowafata hao kwa wema,tutambue fadhila ,sifa,daraja zao kama alivyozitaja Allah kwenye Kitabu chake, na ilivyokuja kwenye Sunna ya Nabii wake, na tujizuwie kutokana na yaliojiri baina yao katika zama hizo .

53Angalia Bihaarul Anwaar :(72,118,146,238,264/20, 30,251/21),Musdrakul Wasaail(119/8) ,(75/13)

Tuelewe kwamba yale yaliyotekea baina yao baada ya mauaji ya Khalifa wa waislamu ‘Othman bin Affaan (r.a) miongoni mwa fitina na marejeo yake ni kwenye taawilina ijtihad, kwa vile kila mmoja wao alidhania kuwa yuko kwenye haki na sio mwenginewe, kama vile alivyokua akisema Imam Ali (a.s) kwa wapiganaji wake :”Hakika sisi hatupigani nao kwa sababu ya kuwakufurisha, wala kupigana nao kwa sababu ya kutukufurisha, lakini tumejiona tuko katika haki nao wakajiona wako kwenye haki “[54]

Ni juu yetu ni kufuata na kutafuta miongozo kwenye miongozo ya maimamu (a.s) tusiwalaani wala kumtukana yeyote yule katika Masahaba wa Mtume (S.AW) ili tuwe katika wale Allah aliowasemea **{ Na waliokuja baada yao husema Ewe Mola tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwenye imani wala usijaalie chuki kwenye nyoyo zetu kwa wale walioamini, Ewe Mola hakika wewe ni mpole ni mwingi wa upole}**
[al Hashr:10]

Amesema Sheikh Muhammad Baaqir An Naaswiry :
{**Na waliokuja baada yao}** anamaanisha baada ya Muhaajirina na Answari mpaka siku ya Kiama **{ husema Ewe Mola tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwenye imani }** yaani wanaomba wakijiombea maghufira nafsi zao na wale waliowatangulia kwa imani

{wala usijaalie chuki kwenye nyoyo zetu kwa wale walioamini } yaani chuki, ghushi na uadui kwa waislamu, wala hakuna mashaka kwamba alieachukia, alieamini, na kumtakia ubaya kwa ajili ya imani yake basi huyo ni kafiri, na akiwa sio hivyo basi atakua na fasiki.[55]

Amesema Shikh Muhammad As Sibzawaary an <u>Najy:</u>
{ Na waliokuja baada yao} anamaanisha baada ya hawa na hawa, nao ni wafuasi wao wengine mpaka Kiama **{… husema Ewe Mola tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwenye imani }** yaani wanaomba wakijiombea maghufira nafsi zao na wale

54 Qurbul Isnaad (uk. 45),Bihaaril Anwaar (323/ 32)

55 Tafsiir Mukhtasar Majma’al Bayaan ,na angalai :Tafsiiril Kaashif,Al muniir(Suuratil Hashr :10)

waliwatangulia katika walioamini na kusamehewa makosa yao kwa imani
{wala usijaalie chuki kwenye nyoyo zetu kwa wale walioamini } yaani chuki, kuwachukia, ghushi na zijaalie nyoyo zetu zenye kuepushwa na hayoo zisiwapendelee ila kheri **{Ewe Mola hakika wewe umpole na mrehemevu}** yaani wenye kusamehewa makosa yao wenye kuwonea huruma kwa ajili ya riziki na msamaha.[56]

Na Allah amlipe mema Imam mwingi wa ibada na zahid (a.s) pale alipotuanzishia njia tukufu wapitie juu yake vipenzi vyake na kundi lake, hivyo ni pale alipo walipomaliza maneno yao hebu akawambianambieni hivi nyie ni muhajirina wa mwanzo **{Ni kwa ajili ya mafakiri wa kihajiri na waliotolewa na kuwacha nchi na mali zao wakitafuta fadhila toka kwa Allah na uradhi na kumnusuru Allah na Mtume wake hao ndio waislamu wa kweli}?** wakasema hapana akawambia hivi nyie ni wale ambao **.{ waliokuwa wakaazi na walioamini imani ya kweli kabla yao wanawapenda wale ambao wamehamia kwao na wala hawana haja yoyote kutokana na yale waliopewa na wanawapendelea kuliko nafsi zao hata kwamba wanahitajia .Na waepushwao wa nafsi zao hao ndio wenye kufaulu kikweli kweli . }** wakasema hapana Ama nyie mumeshajulikana kua mmoja katika makundi mawili haya, nami nashuhudia kwamba nyie sio katika wale Allah aliwaeleza **{Wanasema Ewe Mola wetu tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwa imani wala usitujale chuki kwenye nyoyo zetu kwa wale walioamini}** niondokeeni, Allah atakutendeni "mpaka hapa **.**[Al Hashr :8-9] ……

Na tujikumbushe kauli ya Allah (S.W) :**{ Huo ni Umati yameshapita waliyoyachuma na nyie mutastahiki muliyoyachuma na kamwe hamutoulizwa kuhusiana na waliokua wakiyafanya }**[Al Baqarah :134].

Amesema Muhammad Jawaad Mughniyah :
Aya hii inaashiria msingi wa ujumla, nao ni kwamba matokeo ya amali na athari zake kesho zitarejea kwa mtendaji pekee, kamwe hatonufaika kwazo anaenasibika nae zitakapokua za kheri, kama

56 Tafsiiril Jadiid (Suuratil Hashr :10)

vile ambavyo hatodhurika kwazo asiekuwa yeye na uislamu umeeleza msingi huu kwa namna tofauti, miongoni mwao ni Aya (164) katika suratil An A'am :**{ Na kamwe mbebaji hatobeba-mizigo ya- mbebaji mwengine }** na katika hizo ni Aya ya (39) katika Suratin Najmi **:{Na kwamba Mwanadamu hastahiki ila kile alichokichuma]**… na miongoni mwao ni kauli ya Mtume alietukuka kwa binti yake Fatma[57] **(Ewe Fatma , fanya amali wala usiseme :Hakika mimi ni binti ya Muhammad ;kwani mimi sitokusaidia chochote toka kwa Allah)** na mfano wa hizo ni nyingi, na utanuaji kwenye maudhui hii ikiwa itajulisha kitu basi inajulisha juu ya kwamba mpaka leo hatuelewi yaliyowazi zaidi na yaingiayo zaidi .

Na unapotaka kuona njia hii halisi kwenye maisha ya Aalil Bait ya Nabii (S.A.W) katika kudhihirisha mapenzi ya Masahaba na mshikamano uliokua baina yao hivyo soma yanayofata.

MLANGO WA SITA

***Majina na ukwe baina ya Masahaba na Ahlil Bait (r.a*)**

Wajinga hawakuweza kuficha uhakika wa kihistoria unaojulisha yaliotokea baina Masahaba na Ahlil Bait (r.a) katika mapenzi na wema baina yao na katika hayo ni :

Kuitana majina wenyewe kwa wenyewe,au ukwe uliotokea baina yao.

Hivyo watakatifu hao hawakuwaita au kuozesha watoto wao kwa maslahi ya kidunia, au kupata vyeo vinavyotoweka au kwa tamaa ya mali nyingi na heshima, lakini wao waliwaita watoto wao majina ya wale wenye kufatwa hali zao, wakawaozesha watoto wao watu wenye sifa njema wakitarajia kuzipata kama vile usalama wa dini na usafi wa nyoyo; na pupa hili lilikua limekuwa kutokana na kufuata kwao njia ya Bwana wa watu Mustw'afa (S.A.W), nao walikua wakiwauliza watu wao wenye ikhlasi .

[57] Kashful Ghummah (78/2)

Toka kwa Ibrahim bin Muhammad Al hamdaaniy amesema:
(Niliandika barua kwenda kwa Abii Ja'far, kuhusiana na kuoa, basi basi barua yake ikanijia kwa hati zake, amesema Mtume wa Allah :"Atakaekulieni yule munaeridhika na tabia na dini yake basi muozesheni ,**{musipofanya hivyo itakuwa ni fitina katika ardhi na uharibifu mkubwa}** [Al Anfaal :73][58])
Na katika Fiqhi ya ya Imam Ridhwaa (a.s) " Mtu aposapo kwako ambae munaridhia dini yake na tabia zake basi muozesheni wala usikuzuwieni ufakiri wake, na uaskini wake,amesema Taala :**{Na watakapokuwa maskini Allah atawatosheleza (kila mmoja) toka kwenye utajiri wake}"** [59]

Toka kwa Abi Abdillah (a.s) amesema:"Hakika Allah A'zza wa Jalla hakuwacha chochote katika yale anayohitajia mwanaadamu ila amemfundisha Nabii wake (S.A.W) hivyo ikawa miongoni mwa mafunzo yake kwake ni kwamba siku moja alipanda membari ,akamshukuru Allah na kumsifu na akasema :"Enyi watu :hakika Jibril (a.s) alinijia na habari kubwa akaniambia :"Hakika wari ni mfano wa matunda kwenye mti, iwapo utayaona matunda yake na usiyavune yataharibiwa na Jua na kusambaratishwa na upepo ,hali kadhalika wari wakipata wanayoyapata wanawake basi hawana dawa nyengine ila mume, na vyenginevyo hawaaminiki kutokana na uharibifu kwani ni wao ni watu.Akasema:"basi akasimama akamwambia :"Ewe mtume wa Allah! Basi nimuezeshe nani ?akamwambia kuf-u(wanaolingana): akamwambia "Ewe Mtume wa Allah ni nani huo kufu akamwambia waislamu ni kufu wenyewe kwa wenyewe.[60]

Akasema Saadiq (a.s):"Kuf-u ni kuwa mwenye kujitenga na maasi na kuwa na wepesi "

58 Al Kaafy (347/5),Tahdhiibil Kamaal (396/7),Wasaail Shiia'a (77/20)

59 Fiqhur Ridw'aa (uk. 234),Mustadrakulc Wasaail (188/14),Bihaarul Anwaar:(372/100).

60 Al Kaafy (337/5),Tahdhiibul ahkaam ;(397/7),Wasaaili Shiia'a (61/20)

Itrah (a.s) wametahadharisha kuozesha watoto wao kwa Nawaasib au wenye madhambi makubwa na maasi , na hasa hasa wanafiki waliortadi .

Na kutoka kwa Abi Abdillah (a.s) kwamba aliambiwa na Fudhw'ail :"Jee nimuozeshe Naaswibah ? akasema la, wala hakuna hadhi katika hilo.Nikamwambia najifanya kuwa fidya yako, Wallahi !hakika mimi nakwambia hili ,hakika mimi nakwambia mimi hili ,na lau angenijia na nyumba iliojaa dirham nisingefanya hivyo)[61]
Na toka kwa Abdillah (r.a) kwamba alisema :"Kumuoa myahudi au mkristo ni bora ,au alisema ni kheri kuliko kuoa naswibah au kumuozesha naswib.[62]

Toka kwa Ah'mad bin Mohammad ameinasibisha kwa Mtume(S.A.W), amesema Abu Abdillahi (a.s) :"Yeyote aliemuozesha binti yake mnywaji wa ulevi basi huyo amekata mawasiliano na jamaa zake"[63]
Na Mtume (S.A.W) amesema :" Yeyote aliemuozesha binti yake muovu atateremshiwa laana elfu moja juu yake kila siku, wala amali zake hazipandi mbinguni, wala dua zake hazikubaliwi, wala hakubaliwi swarf wala a'dli"[64]

Amesema Abu Abdillahi (a.s) vile vile :"amesema Mtume (S.A.W):"Mnywaji wa ulevi asiozeshwe anapoposa[65]
Na Mtume (S.A.W) amesema :" Yeyote aliemuozesha binti yake mnywaji wa ulevi basi ni kama aliempeleka kwenye zinaa"[66]
Na toka kwa Hasan bin Bishaar al Waasity :"Nimemuandikia Ridhw'aa (a.s):Ninae jamaa alieposa kwangu, na anao ubaya kwenye tabia ! akasema :"usimuzeshe akwa anayo tabia mbaya.[67]

61Man laa yahdhw'uruhl Faqiih (394/4)

62 Al Kaafy (351/5),

63 Al Kaafy (347/5), ,Tahdhiibul ahkaam ;(398/7),Wasaaili Shiia'a (79/20),A'waaly(341/3).

64 Irshaad)

65 Al Kaafy (363/5), ,Tahdhiibul ahkaam ;(398/7),Wasaaili Shiia'a (79/20),A'waaly(341/3).

66 Mustadrakul Wasaail (191/14), A'waaly(272/1).

67 Al Kaafy (363/5), Wasaaili Shiia'a (81/20) Mustadrakul Wasaail (1912/14) Wasaaili Shiia'a (61/20)

Man laa yahdhw'uruhl Faqiih (409/3) Bihaarul Anwaar:234/100).

Hivyo baada ya haya haingii akilini .na haiwezekani Ahlil Bait waliosafika wawaozeshe watoto wao watu waliotiliwa kwenye dini na tabia zao.

Na katika yanayojulisha juu ya kushughulikia kadhia hii muhimu – pamoja na nasaha zenye ikhlasi baina yao juu ya kusidiana juu ya kheri –ni kwamba Abubakri, Omar na Othman walishughulikia Fatimah kuolewa na Ali.

Toka kwa Adhw'ah'h'aak bin Muzaah'im amesema :"Nimemsikia Alibin Abi Talib akisema :"Alinijia Abubakri na na Omar wakanambia:' lau ungekwenda kwa Mtume (S.A.W) ukamtajia Fatimah)[68] .

Nasaha hii toka kwa Masahaba wawili watukufu kwa Imam Ali(a.s) inadhihirisha kupenda kwa Masahaba ukwe wa Ali bin abii Talib kwa Mtume (S.A.W) .Kwa kuwa Alihakua na hali nzuri kiuchumi ,alikua na uwezo mdogo hakuona ubakhili kutaka msaada toka kwa ndugu zake Masahaba alipotaka kuoa.

Katika walioshiriki katika kumsaidia Imam Alikwenye ndoa ya Fatmatiz Zahraa nui Othman bin Affaan(r.a) .

Anasema Imam Ali (r.a) akisimulia niliambiwa na Mtume (S.A.W) :"Ewe Abal Hasan sasa nenda ukauze ngao yako na unijie na thamaai yake ili nikuandalie wewe na binti yangu Fatimah yanayokufaeni Ali akasema :"Basi nikachukua ngao yangu nikaenda nayo sokoni nikaiuza kwa dirham mia nne za Kisud Hijriyyah kwa Uthamaa bin Affaan, basi mara nilipozitia mkononi dirham zile akanambia ewe Ali:" Hivi sio bora kwako kuwa na ngao na kuwa bora uwe na Dirham toka kwangu ?! Nikamwambia ndio ,akanambia basi ngao hii ni zawadi yako toka kwangu, hivyo nikachukua ngao na dirham mpaka kwa Mtume (S.A.W) nikamtupia, nikamuelezo aliyofanya Othman basi Nabii (S.A.W) akamuombea kheri.

[68] Angalia Aamaali cha At Tuusy (uk. 39), Bihaarul Anwaar (93/43).

Mambo hayakuishia hapo tu ,bali Mtume (S.A.W) aliwaamrisha Masahaba wamnunulie Faatimtiz Zahraa mahitajio yake chini ya usimamizi wa Abubakri Sidiq(r.a)[69]
Hivyo Makhalifa watatu hasa hasa,na wengineo katika Masahaba, ni katika walioshiriki, bali walioshuhudishwa na Nabii(S.A.W) ndoa ya Ali bin Abi Talib na Fatma (r.a) na kwamba walikua na mchango mkubwa na muhimu katika kukamilisha ndoa hii iliyobarikiwa.

Amesema Anas (r.a): aliniambia Mtume (S.A.W) :"Nenda kaniititie Aba bakri ,Omar, Othman, Ali, Talhah, Zubeir na idadi ya Answaar ,basi nikenda kuwaita ,wakaja na kila mmoja alipokaa pahala pake akawambia :"nakushudisheni kwamba nimemuozesha Fatima kwa Ali, kwa mithqali za dhahabu mia fedha~~~~~~~~~~.[70]

Elewa- ewe msomaji mpenzi –kwamba Ahlil Bait walikuwa ndio watu wenye kuchunga zaidi katika kuwaozesha watoto wao watu wema na wachaji, na waliokua mbali zaidi toka kwenye kuwaozesha watoto wao waovu na wanafiki na hasa hasa nawaasib na waliortadi, yeyote anaedai kinyume na hivyo basi hakika amewazushia uongo wa hali ya juu ,na kuwasingizia kusema wasioyatenda jambo ambalo Allah aliwachukia kwalo Bani Israail na wengineo amesema Allah (S.W) :**{ Hivi nyie munaamrisha watu kufanya wema na munazisahau nafsi zenu hali ya kua munasoma kitabu, hivi nyie hamuna akili?}** [Al Baqarah :44], na kipenzi huwatukuza Ahlil Bait kwa sifa hii,na kuamini kwamba kamwe hawakuwaozesha watoto wao ila waadilifu na watu wema.
Ewe ndugu msomaji yafuatayo ni baadhi ya ukwe na majina ya watoto wa kiahlil bait ili uelewe kiwango cha maingiliano na mapenzi baina ya I'trah na Masahaba(r.a); kwani wao wakiamini wema wa Masahaba wa Mtume (S.A.W) wakawaozesha, kuoa kwao na kuwaita watoto wao kwa majina yao:
Mtume (S.A.W): Katika wake zake ni :

69 Anglia Kashul Ghummah na Bihaarul Anwaar (130/43).

70 Anglia Kashul Ghummah (348/1)na Bihaarul Anwaar (119/43).

Aisha bint Abubakri Sidiq.
Hafswah bint Omar binil Khatw'aab.
Ramlah bint Abi Sufiyan.
Majina ya wakwe zake:
Alibin Abii Talib amemuzesha binti yake (Fatimah)
Othman bin Affaan amemuzesha mabinti zake Ruqayyah na Ummu Kulthuum.
Abul A'aasw' bnir Rabii' alimuzesha binti yake Zainab.
2) Ali bin Abi Talib:
Katika wake zake –baada ya kifo cha Fatma (a.s):
Asmaa bint U'mais (kizuka cha Abubakri Sidiq)
Umaamata bintil A'aasw bin Rabii'(mama yake ni Zainab bint Rasuulil Laahi)
Katika watoto wake :
Abubakri ,Omar ,Othman .
Majina katika wakwe zake:Omar binl Khatw'tw'ab ,(alieoa binti yake Ummu kulthuum).
A'bdil Rahmaan bin A'amir bin Kureiz Al A'amiry (alimuzesha bint yake Khadijah).
Mua'awiyah bin Marwaan bin Ahakam ,alimuozesha bint yake (Ramlah)
Al Mundhir bin U'baidah bin Zubeir ,alimuoa binti yake (Fatimah).
3) U'qail bin Abii Talib :
Katika watoto wake ni Othman.
4) Al Hasan bin Alibin Abi Twalib:
Katika wake zake :Ummu Ishaaq bin Talha bin Ubaidllaahi At Taymiy.
Katika watoto wake:Abubakri, Omar na Talha .
Majina ya wakwe zake:
Abdullah bin Zubeir bin A'wwaam ,nae amemuoa binti yake(Ummul Husein).
Amri bin Zubeir bin A'wwaam amemuoa bintie(Ruqayyah).
Jaafar bin Musab bin Zubeir,amemuoa binti yake (Maliikah).
5) Al H'usain bin Ali bin Abi Talib :
Katika wake zake
:Lailaa bint Abi murrah (mama yake ni Maymuunah bint Abi Sufiyan).
Ummu Ish-aaq bin Tw'alha bin U'baidillaahi At Taymy[71]
Katika watoto wake ni :
Abubakri ,Omar.

71 Nae alikua kaka yake Hasan alimuusia atakapokufa amuowe Ummu Ish-aaq

Majina ya wakwe zake:
Abdillaahi bin Amri bin Othman bin Affaan,nae alimuoa binti yake (Fatimah).
Musab bin Zubeir bin Alawwaam,alimuoa binti yake(Sakinah).
6)Is-h'aaq bin Jaafar bin AAbi Talib :
Katika wake zake:
Ummu Hakiim bintil Qasim bin Muhammad bin Abubakrii Sidiq
7) Abdullahi binh Jaafar bin abi Talib:
Katika watoto wake:
Abubakri na Mu'aawiyah.
Mkwewe:
Abdul Malik bin Marwaan ,alimuoa binti yake(Ummu Abiiha)
8)Ali bin Al Hasan bin Ali bin Abi Talib (Zanul A'aabdiin) na kun-ya yake ni Abubakri.[72]
Katika watoto wake:Omar
9)Zaid bin Al Hasan bin Alibin Abi Talib:
Mkwewe: Al Walid bin Abdil Malik bin Marwaan alimuoa binti yake (Nafiisah)
10) Al H'usein bin Al Hasan bin Alibin Abi Talib:
Katika wake zake: Amiinah bint H'amzah bin Mundhir bin Zueir binil A'awwaam,
11)Al Hasan(Al Muthannaa) bin Al Hasan bin Alibin Abi Talib:
Katika wake zake: Ramlah bint Sai'iid bin Zaid bin Amr bi nufail Al A'dawy .
Mkwewe: Al Walid bin Abdil Malik bin Marwaan alimuoa binti yake (Zainab).
12)Muhammad bin Omar bin Alibin Abi Talib:
Katika watoto wake: Omar
13)Muhammad (Al Baaqir) bin Ali bin Al H'usain bin Alibin Abi Talib:
Katika wake zake: Ummu Farwa bintil Qaasim bin Muhammad bin Abubakri As Sidiq.
14) Musal (Juun) bin Abdillahl Mah'dhw'Al Husain bin Ali bin Abi Talib:
Mkwewe ni ni mtoto wa kaka wa Al mansour bin Abbas ,nae akmuozesha bintie (ummu kulthuum.)

72 Firaqi Shiia'ah chaa Al Nubkhty (uk. 53).

Katika wake zake:Khalidah bint Hamzah bin Muswa'ab bin Zubeir binil A'wwaam.
U"baidllahi bin Muhammad bin Omar(al Atw'raf) bin Alibin Abi Talib:
Katika wake zake :Ammat bint Abi Jaafaril Mansour.
15) Al Husein bin Ali bin Abi Talib Aswaghar:
Katika wake zake: Khalidah bint Hamzah bin Muswa'ab bin Zubeir binil Awwaam.
16) Ubaidilahi bin Muhammad bin Omar (al Atw'raf) bin Ali bin Abi Talib:
Katika wake zake ni shangazi waq Abil Mansour.
Katiti watoto zake ni :Omar
17) Jaafar bin bin Muhammad bin Omar) bin Ali bin Abi Talib:

Katika watot wake ni Omar.
18) Al Huseinul Aswaghar Ali Zainil a'abidiin bin Al Husain:
Katika wake zake ni :Khalidah bin Musw-a'ab bin Zubair binil A'wwaam ;
19) Al Hasan bin Ali bin Al Hasan bin Alibin Abi Talib:
Omar
Katika watoto wake:
20) a'afaris Swaadiq bin Muhammad (Al Baaqir) bin Ali bin Al Husain bin Ali bin Abi Talib:
Amesema Al Imam Swaadiq (a.s):"Abubakri amenizaa mara mbili"[73]
21) Al Hasan (al Aftw'as) bin AliZainil A'abidiin bin Husein :
Katika wake zake:bint Khalid bin Abii Bakr bin Abdillah bin Omar ibnal Khataab.
22) Muhammad bin Omar bin Ali bin Al Husain bin Ali bin Abi Talib:
Katika wake zake :Ubeidah bint Zubeir bin Hishaam bin U'rwahbin Zubeir binil A'wwaam
23) Jaafarul-aAkbar bin Omar bin Ali bin Al Husain bin Ali bin Abi Talib:

73 Akimaanisha upande wa mama zake : kwani mama yake ni Farwah bintil Qaasim bin Muhammad bin Abii Bkrias Swiddiiq,na bibi yake mzaa mama yake Ummu Farwah ni : Asmmaa-u bint A'bdil Rahmaan bin Abi Bakr.Angalia Kasful Ghummah:(161/2). ni

24) Katika wake zake :Fatma bint U'rwah bin Zubeir binil A'wwaam.

25) Abdillahi binil Al Husein bin Ali bin Al Husein bin Ali bin Abi Talib:

26) Swafiyah bint Muhammad bin Muswa'ab bin Zubeir binil A'wwaam.

27) Muhammad bin Abdillah bin Al Hasan(Al Muthannaa) bin Al Hasan bin Alibin Abi Talib:
Katika wake zake:Fakhiitah bint Faliih' bin Muhammad bin Mundhir bnal Zubair.

28) Musa (Al Juun) bin A'bdilllahi bin Al Hasan bin Hasan bin Alibin Abi Talib:
Katika wake zake: Ummu Salamah bint Muhammad bin Talha bin abdillahi bin Abdir Rahmaan bin Abubakri Swiddiq.

29) Jaafar bin Omar bin Alibin Al H'usain bin Ali bin Abi Talib:
Katika wake zake: Fatma bint U'rwah bin Zubeir binil A'wwaam.

30) A'bdilllahi bin Al Husain bin bin Ali binil Husan bin Alibin Abi Talib:
Ummu A'mr bint Amr bin Zubeir bin U'rwah bin Zubeir binil A'wwaam.

31) Muhammad bin A'uf bin Ali bin bin Muhammad bin Alibin Abi Talib:
Katika wake zake:Safiya bint Muhammad bin Musab bin Zubeir bin Awaam.

32) Al Husain bin Zaid bin Ali binil Husain bin Alibin Abi Talib:
Katika watoto wake : Omar

33) Al Husain bin Ali bin Omar bin Alibin Abi Talib:
Katika watoto wake : Omar

34) Musal (Kaadw'im) bin Ja'afar bin Muhammad bin Alibin Husein bin Ali :
Katika watoto wake : Omar,Aisha.

35) Ali bin Al Hasan bin Ali bin Ali bin Al Husain bin Ali bin Abi Talib:
Katika wake zake: Fatimah bint Othman bin U'rwah bin Zubeir binil A'wwaam.

36) Yahya bnal Husain bin Zaid bin Ali binil Husain bin Alibin Abi Talib:
Katika watoto wake : Omar

37) Ali Ridha bin Musa bin Jaafar Sadiq na kuniya yake ni Abubakri.
Katika wake zake: Ummu Habib bintil; Maamuun Al Abasy, ana watoto watano wanaume na binti mmoja na jina lake ni Aisha. [74]

38) Jaafar bin Musal (Kaadw'im) bin Jaafar Sadiq:
Katika mabinti zake ni Aisha.

39) Muhammadul (Jawaad)Ali bin Musa (Alkadhim) bin Jaafar Sadiq:
Katika wake zake:Ummul Fadw'l bintil Maamun Alabasy [75]

40) Ali (Alhadiy) bin Muhammad bin Ali bin Musa :

74 Ameeleza An Nuuriy At Tw'ibrisy kwenye kitabu chake /An Najmuth Thaaqib fii Al Qaab wa Asmaa-I H'jjatil Ghaaib :14 Abuu Bakr ni moja ya kun-ya za Ar Ridw'aa kama alivyotaja Abul Farajil Aswfahaany kwenye Muqaatil Tw'alibiin .

75 Kashful Ghummah (267/2)

Katika mabinti zake ni Aisha. Katika mabinti zake ni Aisha

Mfungamano na mshikamano huu wa kifamilia uliobarikiwa ,baina ya Aal Nabiy (S.A.W), na baina ya Masahaba(r.a) na wengineo katika maelewano, na kuitana majina wao kwa wao, kuzidi kwa ukwe biana yao .kwa hakika ni dalili iliyo ya wazi juu ya mapenzi yao wenyewe kwa wenyewe, utengeneaji wa dini yao na usalama wa nyoyo na ndimi zao kwa yale yalio baina yao, na sio kama wanavyopakazia watu wa fitina,hivyo tanabahi Allah akulinde.

MLANGO WA SABA

SUALA NA JAWABU

Ewe msomaji mpenzi! Mbele yako kuna jumla ya masuali na maulizo tunayoyasiika baina ya wakati mmoja na mwengine kutoka kwa watu wa shubuhati, miongoni mwa wale wanaotaka kuusingizia Uislamu kwa sababu ya chuki zao, kueneza husuda kutokana na kuchukia zake kupitia kwenye matusi yasiokuwa na uzito wowote kama vile mangati,walionyuma ya njama hii wanataka kudhoofisha mahusiano ya udugu baina ya waislamu na Masahaba, miongoni mwao wakiwemo Aalil Bait ya Nabii (S.A.W), au kukusudia kejeli na udhalilishaji wa Masahaba (r.a), kupitia kwenye kudhihirisha kasoro na kuwagandishia tuhuma,kumbe anajingikiwa mjinga huyu kuwa kejeli na matusi yake yanamkumba mwenyewe na kamwe hayatodhuru jabali la kheri kwa vyo vyote vile.

Kama vile paa anaechoma jabali ili siku moja alidhalilishe Kamwe hatolidhuru nae ataumiza pembe zake.

Utakayoyana ewe msomaji mpenzi ni mkusanyiko wa shubuhati zinazohusiana na baadhi waliochupa mpaka katika kugeuza ukweli wa historia ya Kiislamu inayong'aa kuelekea kwa waliyotutangulia kwenye kufuata njia ya Nabii (SA.W)

Nimezifanya shubuhati kwa namna ya masuala, na kila suala linalo jibu lake ili haki ibainike kwa idhini ya Allah Taala na atuwafikishie wepesi juu ya njia ya haki iliyo ya wazi.
Suala la Mwanzo : Kauli ya kurtadi kwa Masahaba:

Vipi iwezekane tuseme kua Masahaba wote ni waadilifu,wakati Allah (S.W) ameeleza wazi kurtadi kwao wote mara baada ya Nabii wake isipoka watatu tu miongoni mwao[76], kama vile ilvyokuja kwenye kauli yake Taala:**{ Na Muhammad sie yeyote ila Mtume wamepita Mitume kadha kabla yake,hivi basi akifariki au kuuliwa mtageuka juu ya visigino vyenu,na yeyote atakaegeuka juu ya visigino vyake basi hilo halitomdhuru Allah kwa vyo vyote vile, n aatawalipa wenye kumshukuru }** [Aal I'mraan:144].
Jawabu:

Mwanzo :Ni wajibu juu ya msomaji wa vitabu vya tafsiri achague vile vya watafsiri wenye itikadi ilio sahihi walioshuhudiwa na Maulamaa Mujtahidiin kuwa ni wenye elimu na fadhila, nae awe na mwangaza kwenye elimu ya usuuli tafsiri kama vile sababu za kuteremshwa kwa aya, Nnaasikh na mansuukh, -khaas- na -aʾam-, na fani nyenginezo ili asijetafsiri au kufanyia taawili Maneno ya Allah (S.W) bila ya kuwa na elimu.

Pili : Maulamaa wa historia na kadhalika Tafsiri wameelelza kuwa Aya hiyo imeteremshwa kwa tukio maalumu nalo ni la kushindwa kwa waislamu kwenye vita vya Uhud, nalo lilikuwa ni tukio mwanzoni mwa mtiririko wa vita walivyopigana waislamu, hivyo iweje aya ilioteremshwa mwanzoni mwa Hijrah, na kwenye tukio maalumu, iwe ni dalili juu ya ridda ya Masahaba baada ya kifo cha Mtume(S.A.W)?!

Amesema Sheikh Naaswir Makaarim Ash Shiiraazy kwenye tafsiri yake :"Sababu ya kuteremshwa kwa aya, hakika aya ya mwanzo katika aya mbili vile vile ni zenye kuonyesha tukio jengine katika matukio ya vita vya Uhud, nao ni ukwenzi uliokuja ghafla kwenye

76 Angalia Rijaalil Kishy (uk.: 11),Bihaaril Anwaar (259 /28) (220/71),Al Ikhtiswaasw(uk6)

kilele cha vita baina ya Waslamu na washirikina :"Kwamba tumemuua Muhammad,tumemuua Muhammad [77].

Amesema Muhammad Jawaad Mughniah kwenye Tafsiri yake :Aya hii inaashiria kwenye tulio maalum nalo ni tukio la Uhud.
Tatu: Mtiririko wa aya haujulishi juu ya ridda ya Masahaba, bali ndani yake muna ukosolewaji na maelekezo toka kwa Allah (S.W) kwa Masahaba kutokana na ukaidi na kukata tamaa kwenye vita vya Uhud ,pale paliposemwa kuwa Nabii (SA.W) ameuawa, basi Allah aliliambia kundi hilo :Kwamba Muhammad ni mwanaadamu, alieteuliwa na Allah kwa ajili ya ujumbe wake kwa viumbe vyake na imepita Mitume kadha kabla yake, Allah aliwapeleka kwa kaumu zao wakafikisha ujumbe ,wakapita ,wakafa, na baadhi yao wakauawa , na kwamba kama walivyo Mitume kabla yake, nae pia atakufa (S.A.W), hivyo mauti sio kitu kisichowezekana kwake na pengine huenda akauawa, hilo akalitilia nguvu, akasema (S.W) :**{hivi basi jee akifariki au kuuliwa mtageuka juu ya visigino vyenu}** [Aal I'mraan:144]. Maana yake : Basi hivi Allah atakapomfisha, au makafiri wakamuuwa, mutartadi baada ya kuamini kwenu hivyo ridda ikaitwa kugeukia visigino: nako ni kurejea kwa kupumbaa, kwani ridda ni kutoka na kuelekea kwenye dini mbaya zaidi, kama vile ambavyo kuegekia visigino ni kutoka kuelekea kwenye mwendo uliombaya zaidi .

Na suala kwenye Kauli yake:**{…hivi basi jee akifariki..}** ni suala la kuchukiza, kama ilivyo kwenye Kauli yake Taalaa;**{Na hatukujaalia kuishi milele kwa mtu yeyote yule kabla yako hivi basi ukifa basi wao ni wenye kuishi milele?}**
[Al Anbiyaa :24]

Nne:Itakuwaje tuwahukumu Masahaba walioshindwa vitani kuwa ni wenye kurtadi wakati Allah (S.W) ameshawasamehe kwa kauli yake**:**
{Hakika Wale waliovipa mgongo- vita - miongoni mwenu siku majeshi mawili yalipokutana, hakika walitelezeshwa na shetani kwa sababu ya yale waliyoyachuma, na kwa hakika Allah

77 Tafsiirul Amthaal :(169/20)

ameshawasamehe, hakika Allah ni Mwingi wa Maghufira na ni Mpole}[Aal I'mraan :155]?

Tano: Hakika Aya inatukumbusha msimamo wa Abu Bakri (r.a),ushujaa, wake na nguvu za kufungamana na Allah Tabaraka wa Taala, na kuhudhurikiwa kwake na Aya zake katika hali ngumu baada kifo cha mtume (S.A.W) kwa kauli yake : :**{ Na Muhammad si yeyote ila Mtume wamepita Mitume kadha kabla yake, hivi basi akifariki au kuuliwa mtageuka juu ya visigino vyenu,na yeyote atakaegeuka juu ya visigino vyake basi hilo halitomdhuru Allah kwa vyo vyote vile na atawalipa wenye kumshukuru }** [Aal I'mraan:144].

Pale Masahaba walipokuwa kwenye kishindo kikubwa kilichowapata kutokana na kuondokewa na Nabii (S.A.W), wapo waliokana mauti kama vile Omar bin Khataab (r.a) kutokana na moyo wake kufungamana na mapenzi yake ,wengine wakajilazimisha na kukaa kimya nao wakiwa kwenye fazaa, vile vile watu wa majangwani wengi wakartadi kwa sababu ya kifo cha Mtume (S.A.W), na wengineo kuwacha kutoa Zaka na matukio mengine kama tulivyotangulia-kueleza - .

Sita: Ni jambo linajulikana kwamba hakika aliertadi baada ya kifo cha Mtume (S.A.W) haitwi Sahaba kwani Sahaba katika sheria ni Mtu aliekutana na Nabii (S.A.W) na akafa katika Uislamu ,na alietoka kweye Uislamu (Allah atulinde) hawi miongoni mwao ila atakaporejea upya kwenye Uislamu.

Suala la Pili (Hadithi ya Hodhi) :

Vipi itawezezakana vile vile, kumuhukumia uadilifu yule ambaye amehukumiwa ridda na Allah siku ya kiama na ubadilishaji wa vile dini yao, kama vile ilvyokuja kwenye hadithi ya Hodh, na wale Nabii (S.A.W) alivyosemea kuhusu wao :"Masahaba wangu, Masahaba wangu), baadae litamjia jibu kali toka kwa Mola wake: Hakika wao hawakuwacha kuwa wenye kurtadi tokea ulipotengana nao.!

Jibu :
Inawezekana kuelekeza utoleaji huu wa dalili kwenye fahamu sahihi kama ifuatavyo :
Kwanza: Hakika makusudio ya Masahaba wangu hapa ni wanafiki waliokua wakidhihirisha Uislamu wakati wa Mtume (S.A.W) kama alivyosema Allah (S.W) **{ Wanapokujia wanafiki husema tunashuhudia kwamba wewe ni Mjumbe wa Allah na Allah anajua kuwa wewe ni mjumbe wa Allah, na Allah anashuhudia kuwa hakika wanafiki ni waongo}**[Al Munaafiquun:1]

Na wanafiki wamo undani wake aliowaelewa Nabii (S.A.W)-nao ndio wengi- na wamo asiowaelewa na hao ndio aliowasema Nabii (S.A.W) ”Masahaba wangu, Masahaba wangu”walikua miongoni mwa wanafiki undani wao uliofichika kwa Nabii (S.A.W) kama alivyosema A’zza wa Jalla :**{Na miongoni m waliokuzungukeni katika watu wa majangwani wamo wanafiki na watu wa Madina mmezama kwenye unafiki ,wewe huwaelewi sisi -ndio-tunaowaelewa ,tutawaadhibu mara mbili na warejeswe kwenye adhabu iliyokubwa }**[At Tawbah :101].

Hivyo wale aliowasema (Masahaba wangu) kwenye Hodhi walikua wanafiki waliokuwepo Madina na wale ambao Nabii (S.A.W) alidhania kwamba wao ni katika Masahaba , na hawakua hivyo, kwa kutowaelewa (S.A.W) kwa sababu ya kutokuwepo na hali za undani mwa watu, na hukumu ya kisheria ililkua ikihukumia yale yaliodhahiri tu.

Pili:
Inawezekana ikawa Masahaba hapa ni wale waliortadi baada ya kifo cha Mtume, kama ilivyo hali ya wengi wa watu wa majangwani waliortadi ,na miongoni mwa waliosilimu katika miaka ya mwishoni.

Amesimulia Al Majlisy kwenye Bihar toka kwa Seyyid Ibni Taaus kwamba amesema :Ametaja Al Abbas bin Abdurahman :Uislam haukuendelea kwenye mataifa ya kiarabu baada ya kifo cha Mtume (S.A.W) ila kwa watu wa Madina, Makka, Na Ahli Taaif ,na watu waliobakia watoka kwenye Uislamu.

kasema : Banu Tamiim na Aribaab walirtadi na wakajiunga kwa Malik bin Nuwairah Al Yarbuiy, Rabiya wotewakartadi,nao walikuwa kambi tatu :Yamaamah, pamoja na Musailamatil Kadhaab, kambi pamoja na Maa'ruur As Shaybaany na ndani yake mukiwa na Bani Shaybaany na Bakri bin Waa-il wote na wakiwa kwenye kambi pamoja na Al Hu'twaimil A'bdy ,wakartadi watu wa Yemen,akrtadi Al Ash-a'th bin Qays katika Kandah, wakartadi watu wa Ma-a-rib pamoja na Al Aswadil Ansy na wakartadi Banu Aamir isipokua A'lqamah bin A'llaathah[78].

Tatu :Inaweza kuwa makusudio ya neno (Masahaba wangu, Masahaba wangu) ni kila aliekuwa na kwenye njia hii ilionyooka, japo hajamuona, na hilo linajulishwa na riwaya :" (umma wangu, umma wangu) na katika riwaya (hakika hao ni umma wangu).
Ama kauli ya Mtume (S.A.W) :"Nawajua", ni kwamba Nabii (S.A.W) ameainisha kwamba yeye anauelewa Umma huu kutokana na athari za udhu .

Hivi ndivyo kama alivyosema Allah A'zza wa Jalla kwenye ulimi wa Nabii (S.A.W) kwenye kauli yake Taala :**{Na atasema Mtume Ewe Rabbi hakika watu wangu wamifanya Qur-anhii kuwa ni yenye kuhamwa}** [Al Furqaan :30]. Hivyo Nabii (S.A.W) kamwe hakusudii kaumu kuwa ni Masahaba wake na katika wakati wake, bali anakusudia yale yatakayozushwa na wfuasi wake baada yake katika Umma wake kwa kuihama kwao Qur-an.

Abii Bakris Hivyo hao ambao Nabii (S.A.W) anawasemea:(Masahaba wangu Masahaba wangu) .akaambiwa wewe Hakika wewe hujuwi waliyoyazusha baada yako.. yaani:Hakika wao hawakuwcha kuendelea kuwa wenye kurtadi tokea ulipowawacha.

Suala la Tatu :

Kauli ya kwamba Allah ameliponda kundi katika Masahaba :

78 Bi'haaul Anwaar(11/28)

Itakuwaje tuseme kuwa Masahaba ni waadilifu ,na Allah amewaponda kwenye mwahala kadha kwenye Kitabu chake kwa Aya za waziwazi:

Mfano wa Kauli yake Taala :**{Enyi mlioamini muna nini mukiambiwa kimbieni kwenda kupigania dini ya Allah munafanya uzito kwenda kwenye ardhi ya mapambano, hivi munaridhia maisha ya dunia kuliko ya akhera, basi maisha ya dnia sio cho chote kwernye maisha ya akhera isipokua kidofgo tu }**[At Tawbah :38 .]

Vitisho vya Allah(S.W) vimekuja na tahadhari yake kwao:**{Enyi mulioaminia yeyote atakayetoka kwenye dini yake basi Allah ataileta kaumu anayoipenda na wanaompenda;wanyonge juu ya walioamini wakakamavu juu ya makafiri ,wapigane kwenye njia ya Allah na kamwe wa`sihofu lawama ya mwenye kulaumu , hiyo ni fadhila ya Allah anayompa apendaye na Allah ni mwingi wa elimu}**[Al Maaidah :54].

Vile vile ameponda kutokuwa kwao na unyenyekevu wa nyoyo zao kwa ajili ya kumkumbuka yeye, kama ilivyo katika kauli yake:**{Hivi wakati haujafika kwa walioamini kwa nyoyo zao kunyenyekea kwa kumkumbuka Allah na yale aliyoyateremsha katika Haki, na wasiwe kama wale waliopewa kitabu kabla (yao} na muda ukawarefukia hivyo nyoyo zao zikawa ngumu na wengi wao ni waovu}**[Ajl H'adiid:16].

Au pale walipomuwacha Nabii (S.A.W) wakati wa kufika biashara ,Akawambia Taala:**{ Na waonapo biashara au mchezo wanazikimbilia na wakakuwacha wewe umesimama,wambie yale yaliyo kwa Allah ni bora kuliko mchezo na biashara na Allah ndie mbora wa kuruzuku }**[Al Jumua':11].

Jibu :
Mwanzo : ni wajibu juu ya muislamu awe mtafiti kuhusiana na haki awache ukereketwa wa kimawazo ,awe mwenye kutafuta mwongozo kama tunavyosoma kwenye sala zetu kauli yake Taala:{ **Tuongoze njia iliyonyooka** }[Al Faatih'ah :6], na ajiepushe na batili japo ikiwa imetoka toka kwa mwanazuoni au

shekhe anaemfuata bila ya hoja, kwani Allah amewaponda watu wa ukereketwa,ambao walisema:**{Hakika sisi tumewaona mababa zetu wapo kwenye desturi zao na kwamba sisi ni wenye kufuata nyayo zao**}[Zukhruf:23].

Pili: Lazima tuelewe kwamba Masahaba (r.a) hawakuhifadhiwa na kutenda makosa, na uislamu umewakhafifisha kutokana na tabia mbaya za ujahilia.

Pale walipojiwa na Mtume (S.A.W) akiwalingania kwenye Tawhiid kwa kufanya mema,na kuwacha maovu waliyokuwanayo, walimkubali na kumuamini kwa hiari ,hivyo Allah akawaelekeza kwenye kheri na utengamano akawakataza na kuwatahadharisha na kutenda ya haramu, akawa anawaita kwenye Kitabu chake kwa kauli yake **: { Enyi mulioamini }**

Hivyo Masahaba wamejifunza kutokana na njia makosa yaliyotokana na baadhi yao kwa sababu ya kutoelewa kwao Dini yao mpya au kuathirika kwao kwa ujahila, hili ni pamoja na Masahaba katika Aalil Bait kama vile Abbas, Hamza, Ja'afaru At Tw'ayyaar na wengineo katika Masahaba wa Aalil Bait (a.s).

Amri, makatazo , kutahadharishwa huku hayakuwa na kamwe hayatokuwa makhsus kwa Masahaba wa Nabii (S.A.W) tu, bali hiyo ni hoja juu nyumati zenyekufuata mwongozo wa Mustw'afaa (S.A.W) , kwani shani ni ujumla wa matamshi na sio kwa umakhsusi wa sababu .

Tatu :
Allah Tabaraka wa Ta'ala ametofautisha kwenye wito wake baina ya Ahlil Iiman na ahlil kufr, hivyo anapoita watu wa imani alikuwa akisemesha kwa Kauli yake **{Enyi mulioamini }.**
Na pale anapoelekeza maneno yake kwa makafiri au watu wote ,walioamini na makafiri alikuwa akisema katika kusema nao **{Enyi watu }**.

Nne:
Tuchukulie hivyo hivyo hata kwamba sisi hatukufahamu Qur-an na kujua Tafsiri yake, litakuwaje jibu letu pale mmoja wa

mustashriqina wakereketwa atakapotwambia : Hakika Nabii wa Uislamu Muhammad bin Abdillahi anawatii makafiri na wanafiki kama ilivyokuja kwenye Qur-ani :**{ Ewe Nabii muogope Allah na usiwatii makafiri na wanafiki ,hakiak Allah alikuwa na anaendelea kuwa Mjuzi na Mwingi wa hikma }**[al Ahzaab :1].
Bali atowe madai juu ya Dini yetu aseme :"Hakika Nabii wenu anahalalisha aliyoyaharamisha Allah kwa kuridhisha wake zake tu, kama vileyaliyomo kwenye Qur-an**{Ewe Nabii kwanini unaharamisha aliyokuhalalishia Allah ,unafata ridhaa za wake zako , na Allah ni Mwingi wa kusamehe mwingi wa kurehemu }** [Tahriim;1],au Nabiiwenu alikuwa akitaka kuwaswalia wanafiki ili awatakie rehema:{ Na kamwe usimsalie yeyote miongoni mwao aliekufa milele, wala kusimama juu kaburi yake, hakika wao wamemkufuru Allah na Mtume wake, na wamekufa hali ya kuwa ni mafasiki }[At Tawbah :84].

Hivyo ni lazima, ewe mpendwa jibu lako liwe kwamba Nabii (S.A.W) hamuasi Mola wake katika aliyomuamrisha na zinatujulisha kwamba Allah Taa'laa amemfundisha Nabii wake Sharia na dini yake ili awafikishie watu, kama alivyosema Taala :**{Ewe Nabii hakika tumekutuma uwe shahidi na mtoaji habari njema na muonyaji}**[Al Ah'zaab :45].

Kama Allah alivyobainisha kwenye mwahala kadha kwenye kitabu chake kitukufu, kama vile kauli yake Taala:**{Ewe Nabii wapige vita makafiri na wanafiki na uwatilie ngumu juu yao}**[Tahriim :9] ..**{ Ewe Nabii waambie wake zako , mabinti zako na wanawake wa kiislamu wajiangushie mabaibui yao }**
[Al Ah'zaab:59].

Tano : Tuliyoyajibu ewe mpendwa, ni pale mmoja wa nawaswiba na anapotwambia kwa kukusudia kumtia dosari Imam Ali(a.s), na akitolea dalili kwa dosari zake kwa dhahiri ya Qur-an na riwa ya zilizothibiti toka kwa Nabii (S.A.W) na kutwambia "Amesema Mtume (S.A.W): Hakuteremsha Allah Aya yenye Kauli yake{Enyi mulioamini }isipokua na Ali ndie kiongozi na amiri wake"[79].

79 Angalia Al Yaqiin fii Imratil Mu-u-minin (uk. 177,174) ,Bihaarul Anwaar :(21/40)'

Na dalili ya haya ni yale yaliyothibiti kwenye Swahifa ya Imam Ridhw'aa (a.s)
Kauli yake :" Katika Qur-an hii hamna **{Enyi mulioamini }** ila hiyo kwenye haki yetu "[80]

Hivyo jawabu juu ya Nawaswibi kwa Aalil Baitin Naby (S.A.W) huwa kama jibu juu ya Naaswiby huyo ambaye amesimamisha uadui wa ujumla kwa Masahaba wa Nabii (S.A.W)

Suala la Nne:

Kauli kwamba Masahaba walikwenda kinyume na amri ya Nabii (S.A.W) katika Suluhu Ya H'udaibiyyah :

Vipi tuseme auadilifu wa Masahaba(r.a), nao wamempinga Mtume (S.A.W) kwenye suluhu ya Hudaibiyyah , kwa sababu ya kuasi kwao amri yake, pale alipowaamrisha wanyowe na wachinje wasitekeleze amri yake? bali kwamba Omar aliweka wazi upinzani kwa maamuzi ya kwenye makubaliano yake na suluhu yake pamoja na Washirikina Nabii (S.A.W) aksema: Jee mimi sie Nabii wa haki akasema ndio, Omar akasema:jee sisi hatuko kwenye haki na adui yetu yuko kwenye batili ?akasema ndiyo, Omar akasema (kwa hivyo hatutotoa dunia toka kwenye dini yetu)?

Jawabu:

Mwanzo: Ni wajibu juu ya muislamu kutorembea tuhuma bila ya bayana na utafiti wa sababu za matukiona inampasa awe mwenye insafu ikwa anataka haki ,wala astukane na kupandisha mori mwanzoni juu ya yeyote,na hasa kwenye Masahaba wa Nabii (S.A.W) bila ya ujuzi ,na lazimakiwango cha mapenzi ya Masahaba kwa Nabii wao ,na yanadhihiri wazi kwenye hali na minasaba kadha, na miongoni mwao ni kukimbilia kutafuta baraka kwa athari zake (S.A.W) kwa kuchukua makombo ya udhu wake, na hakuwa akitema mate wala mafua ila huyadaka kwa viganja vyao wakajipangusia nyuso na viwili wili vyao, kamwe unywele

80 Al manaaqib (53/3),Al Burhaan (Suratul Baqarah Aya: 153)..

wake (S.A.W) haumdondoki ila wanakimbilia kuuchukua ili wapate baraka toka kwake kama ilivyokuja kwenye riwaya ya U'rwah bin Masu'ud[81]

Pili: Masahaba kwenye Suluhu ya Hudaibiyyah kamwe hawakumuasi Nabii (S.A.W) pale alipowaamrisha, bali wao walikuwa na shauku kubwa na Nyumba Tukufu, hivyo walitamani pale Nabii (S.A.W) alipowaamrisha kukata U'mrah na kufanya tahallul kwa kunyowa vichwa vyao lau Nabii (S.A.W) angebadilisha hukumu yake, au Allah Tabaraka wa Taala angeteremsha Wahyi unaomuamrisha Nabii wake(S.A.W) aingie Makkah, hivyo wote wakangojea (bila ya kuwatowa wengine) huenda pakatokea kitu katika jambo hilo!, na kwa hivyo wakangojea kidogo katika kutekeleza amri ya Nabii (S.A.W) kwa raghaba ya kutokea mfano wa matarajio haya, basi alipotokea Nabii (S.A.W) akiwa amenyowa na kuchinja hadyu yake, na hapo Masahaba(r.a) wakaelewa kwa yakini kukatika kwa matarajio yao, na kuhakikishika kwa jambo lenyewe, na hapo moja kwa moja wakatekeleza amri yake wakanyoa vichwa vyao na na kuchichinja hadia zao bila ya tia toa, hivyo Allah akawateremshia Aya:

{Kwa hakika Allah amerushia waliomini pale walipokupa ahadi ya chini ya mti amesha elewa yaliyomo kwenye utulivu kwenye nyoyo zao na akawalipa ushindi uliowazi ulio [Al Faft-h] } [Al Faft-h18]

Tatu : Omar bin Khattab (r.a) hakupinga amri ya Mtume (kwenye suluhu, bali alikuwa akifanya utafiti pamoja nae na kumshauri katika jambo la Umma,mfano kama ilivyokuwa kawaida ya Nabii (S.A.W) katika kushauriana na Masahaba na haha wakuu miongoni mwao ,kwa kushauriana ni mwenendo aliokua akiurekeleza pamoja na Masahaba zake kwa amri yake Allah **(S.W) {Na washauri katika jambo }**[Al I' I'mraan:159]

Amesema Al Faidw'ul Kashshaany kuhusiana na kauli yakeTa'alaa:**{Na washauri katika jambo }** katika jambo la vita na mengineo , katika yafaayo kushauriwa kwa ajili ya Ummah toka

81 Angalia ;(uk. 32)

kwa Nabii (S.A.W) bila ya ukali ,jeuri au ujuba ,wala mashindano sio madhubuti zaidi kuliko ushauri .

Imekuja kwenye Nahjul Balaaghah:"Yeyote aliyetegemea rai yake tu basi huyo ameangamia .na aliewashauri watu basi ameshauriana katika akili zao., na kwenye ushauri ndimo ulimo mwongozo wenyewe, na hakika amehatarika alietoshelezeka na rai yake).Na katika Al Khiswaal toka kwa As Swaadiq(a.s): " Na uwashauri wanaomuogopa Allah katika jambo lako N" …mpaka hapa.[82]

Na tukio hilo Mtume (S.A.W) alichukua ushauri wa Omar (r.a), katika Makkah kumpeleka Othman bin A'ffaan(r.a), kwa ajili ya mazungumzo na Washirikina.

Ameeleza Shekh At T'ibrisy kwenye tafsiri yake Majma'al Bayaan kisa cha ushindi wa H'udaibiyyah kwa muhtasari na akasema:"Amesema Ibni Abbaas:" Hakika Mtume (S.A.W) alitoka akikusudia Makkah, alipofikilia H'udaibiyyah, ngamia akasimama, na kumshitua na hakushituka, ngamia akalala. Mtume (S.A.W) akasema:"Hii sio kawaida yake,lakini, amefungwa na mfungaji wa tembo ,na akamwita Omar ampeleke Makkah,ili akamtakie idhini toka kwa Makureshi aingie Makka na atoke kwenye U'mra yake, na achinje hadya yake, akamwabia :"Ewe Mtume (S.A.W) mimi sina rafiki, na kwamba mimi nahofu Makureshi kutokana na ukubwa wa uadui wangu kwao, lakini nitakujulisha mtu aliemakini zaidi kwa jhilo kuliko mimi,Othman bin Affaan! akamwambia umesema kweli.[83]

Nne: Kwanini kwani tumtie ubayana Omar(r.a) kwa ajili kumshauri kwake N na tumtuhumu kwa kupingana na Nabii (S.A.W), na tujengee juu ya hilo kwa matusi kadha na Mtume (tendo hilo hakumkatazaikiwa anastahiki kukatazwa na kutahayariswa?!)

82 Tafiirus Swaafii ,na uangalie:Tafsii Majmaa'al Bayaan ,Al Jawharth Thaman ,Tafsiiri Mui'iin ,Tafsiishibr:kwenye tafsiri ya (Surtil Aali I'mraan Aya :159).

83 Tafsii Majmaa'al, (Bayaan194/9), Bihaarul Anwaar :(329/20)

Jee sisi ni wajuzi na watambuzi zaidi kuliko Nabii wetu katika malezi ya Masahaba wake, na namna ya kutendeana nao kwenye maneno yake!? au sisi tumejua jambo lililofichika juu ya Nabii (S.A.W) ?! au ipo sababu nyengine inayotutia chuki na kutukera juu ya alivyofanya Omar (r.a).

Hakika mfano wa mashauriano hayo yametokea baina ya Ali na kundi lake kwa mfano mfano H'ijri bin A'ddy katika vita vya Swiffiin, pale Imam, Alialiwakataza kumlani Mua'awiyah na jeshi lake, H'ijri akamjadili katika hilo wala Imam Ali hakutoa kasoro, wala waliokuja baada yake pia kwa sababu ya H'ijri bin A'ddy kupinga amri ya Imam Ali (r.a).

Toka kwa Abdillaahi bin Shariik amesema :"Alitoka H'ijri bin A'ddy na A'mri bin Al H'amq wakidhihirisha kujitenga na lana juu ya watu wa Sham, Ali(r.a) akawapelekea ujumbe wacheni hayo yalionifika mimi toka kwenu. Wakamjia wakamwambia :"Ewe Amiiril Mu-uminiin hivi sisi hatuna haki ? akamwambia ndio .Wakawambia hivi wao hawako kwenye batili? Wakamwambia la.:"wakamwambia:" Basi kwanini unatuzuwia tusiwatukanae? akawaambia :Nimechukizwa nyie kuwa wenye kutukana na watengaji.

Tano: Lau tutakubaliana na mjadala kwamba aliyoyafanya Omar(r.a) yalikuwa mbali na usahihi kwa sababu ya kupingana na Nabii (S.A.W) ,basi jibu litakuwa lipi tutakapoambiwa na naaswiby:"Hakika Alialikuwa miongoni mwa viongozi wa wapinzani akaasi amri ya Mtume (S.A.W) pamoja na Masahaba wengine kwa kutokunyoa vichwa vyao na kuchinja hadiya zao?.

Bali kukataa kwa Alibin Abi Talib amri ya Nabii (S.A.W) inazidi ya kufuta kule kupinga Omar(r.a) pale alipomtaka afute jina lake pale alipoandika suluhu pamoja na mjumbe wa Makureshi , Suhail bin A'mri akakataa kutekeleza amri ya Mustwa'fa (S.A.W)?

Dalili ya hayo ni yaliyotoka Abi Abdillahi (a.s), kwenye hadithi katika kisa cha Hudaibiya:"Hakika Amiril Muumin katika uandikaji wa suluhu :"Kwa jina lako Ewe Mola,hivi ndivyo alivyoamua Muhammad Rasuulullaahi na viongozi wa Kikureshi

,akasema Suhail bin A'mri : :" lau tungeelewa kuwa wewe ni Mjumbe wa Allah tusingekupiga vita, andika Mohammad bin Abdillaahi, hivi wewe unakataa nasabu yako Muhammad? Nabii (S.A.W) akasema mimi ni Mjumbe wa Allah hata nyie musipokubali, akasema futa ewe Ali na uandike Muhammad bin Abdillahi, Amiiril Muuminin (r.a) akasema : "Sifuti unabii kamwe, Mtume (S.A.W) akafuta kwa mkono wake…" Habari [84]

Kwa nini tumpinge naswiby huyo anaposema: Kwa nini Ali bin Abi Talib akatae pale Nabii (S.A.W) alipomtaka afute jina lak e?jee Alini mchaji,mwenye pupa na mjuzi zaidi kuliko Nabii (S.A.W) katika kutopenda kufuta jina? Bali upinzani ulikariri toka kwake kwa amri ya Nabii (S.A.W) kama ilivyotokea kwenye vita vya Tabuuk, pale alipomtaka abakie Madina kama hali ilivyo kwa wenye nyudhuru , kama vile Ibni Ummi Maktuum na wegineo kwa sababu zilizoainishwa alizoziona Nabii (S.A.W) lakini alitoka na kumfika Nabii (S.A.W) akijaribu kumtoa katika maamuzi yake na amchukuwe pamoja nae kwenye vita.

Toka kwa Abdillahi toka kwa baba yake, toka kwa Abi Said, toka kwa Suleiman bin Bilal, toka kwa Jaiid bin Abdurahman toka kwa Aisha bint Saad, toka kwa baba yake Saad kwamba Alialitoka pamoja na Nabii (S.A.W) mpaka Thaniyyatil Wadaa' huku akilia na kusema :"hivi unaniwacha pamoja na wasiokwenda?akamwambia hivi wewe huridhii kuwa cheo chako wewe kwangu ni cheo cha Haaruun kwa Musa isipokua Unabii?"[85]

Basi kwa nini Ali asiridhie amri ya Nabii (S.A.W) kwa kumuwacha Madina kwenye vita vya Tabuuk ? jee Ali anamuasi Nabii (S.A.W) kwenye amri yake ? jee hakuwa akijuwa kwamba kuwekwa kwake Madina ni hadhi na ubora kwake au la ? iwapo hakuelewa basi huu ni msiba , na ikwa akijuwa basi huo ni msiba mkubwa zaidi .

84 Mustadrakul Wasaai-l(306/12),Bihaarul Anwaar(399/32),Waq-a'u Swiffiin:uk:((102)

85 Bihaarul Anwaar: (262/37) ,U'mdah (uk.127).

Na jibu juu ya Amiiril Mu-miniin ni mfano wa tulioyabainisha kwenye haki ya Amiiril Mu-u-miniin Omar (r.a) . hivyo haki ni moja hata sura za uzushi zikiwa nyingi .

Suala La Tano:
Raziyyah ya Siku ya Alkhamis :
Nini tuseme kuhusiana na tendo la Masahaba ya siku ya Alkhamis siku nne kabla ya kifo cha Nabii (S.A.W) ,na tofauti zilizotokea na unyanyuaji wa sauti zao juu yake na kuasi kwao amri ya Mtume (S.A.W) kwa kutoleta bega na kidawa cha wino ili awaandikie kitabu ambacho kamwe hawatopotea baada yake , na kumtuhumu (kwa kutokuwa na uwezo wa maamuzi) na Omar bin Khataab akasema :"Amezidiwa na maumivu na nyie munayo Qur-an kinatutosheleza Kitabu cha Allah" mpaka mpaka Nabii (S.A.W) akaghadhibika na kuwatowa toka kwenye nyumba yake , na Ibn Abbas akatafsiri kuwa hilo lilikuwa ni **raziin?**

Jibu :
Kwanza : Lazima tujiulize nafsi zetu , ilikuwa vipi hali ya kiafya ya Mtume (S.A.W) katika kipindi hicho ? na ipi ilikuwa sababu ya khitilafu zao mbele yake?

Hakika tukio hilo lilitokea siku nne kabla ya kifo cha Nabii (S.A.W) alikuwa juu ya kitanda chake nae akiwa akiumia maumivu makali sana, bali alikuwa kwenye maumivu makali sana,mara akizirai na mara kuleuka wakati huo akawambia Masahaba:" Nileteeni kitabu nikuandikieni musipotee kamwe baada yangu" hapo Masahaba wakatofautiana, mingoni mwao wapo waliotaka Mtume (S.A.W) asijiteze nguvu kwenye maradhi yake, na kudhania kwamba jambo halikuwa la wajibu, ila lilikuwa kwa njia ya hiari tu na ukumbusho, na wapo waliotakapaletwe bega na wino kwa ajili ya kuandikiwa.

Pili : Hakuna kiumbe chochote kinachoweza kufikiria kilichotokea dakika hizo, fikira iliyo ya wazi, mfano wa walivyoshuhudia wale

walioshuhudia dakika hizo tukio hilo na kuangalia ugumu wa hali iliyomkuta Nabii (S.A.W) kwenye maradhi yake ya mauti , na hasa kwamba ilikuwa bado kuwapitikia hali kama hiyo kabla kwa Nabii (S.A.W), hivyo rai zao zikatofautiana kwa kutowahi kutokewa na hali hiyo kabla.

Tatu : Kushikilia tukio hili na kwamba ndani yake muwe na istihizai na utiaji ila kwa Masahaba ni jambo geni lisilotanguliwa na yeyote kabla, hivyo ni kwamba tukio hilo liliwapita Masahaba (r.a) bila ya kulipa uzito wowote na kuelewa kwamba halikuwa na shubuha yoyote ya kutuhumiana Masahaba kwa unafiki, kufuru au kutomtii Mtume (S.W.A), hivyo basi jamani wale walioishi baada yao wawe ni wajuzi na wanaoona zaidi kuliko kundi lote hilo lililoishi baada ya Nabii (S.A.W) ?!

Nne: Lau tutafanyia muhtasari nukta zinazoweza kuwa ndani yake zimo kasoro katika uadilifu wa Masahaba (r.a) kutokana na tukio hili, ingewezekana kufupishwa katika nukta zifuatazo :

a)Ukataaji wa Masahaba kutekeleza amri ya Mtume (S. A W.) .
b) Kutofautiana kwao na unyanyuaji wa sauti zao mbele ya Nabii(S.A.W) kunajulisha kutokuwa kwao na unyenyekevu .

c) maneno maovu ya baadhi ya Masahaba mbele ya hadhi ya Nabii (S.A.W) na kumfanya kwao kutokuwa na maarifa.

d) Omar bin Khatab alikataa kutekeleza amri ya Nabii (S.A.W)

Tunaweza kuzirudi shubuhati hizo kwa muhtasari katika kauli ifuatayo:
(**Kutotekeleza amri ya Nabii (S.A.W**). Masahaba kamwe hawakuvunja amri ya Nabii (S.A.W), ila walikuwa wakidhania kwamba pengine maradhi yalikuwa yamemzidi kama hali ya watu wengine; kwani ndio mara ya mwanzo wanamuona Nabii (S.A.W) yuko katika hali hii, nao walikuwa wakielewa kuwa kitabu cha Allah kimo mikononi mwao, dini tayari imeshakamilika na sheria zake zimeshatimia , na hivyo wakawa wanataradadi kwa kutoelewa makusudio ya kauli yake Nabii (S.A.W)

.(**Kukhitilafiana kwao na kunyanyua sauti zao**) hakuna dalili ya wazi wazi juu ya kunyanyua sauti zao juu ya sauti ya Nabii,(S.A.W), na lau hilo lingetokea basi Allah angeteremsha Wahyi wa kuwalaumu na kuwatahayarisha, na hasa kwamba Suratul Hujurati ilikuwa imeshakamilisha na ndani yake mlikuwa na maelezo ya adabu ya namna ya kuzungumza na Mtume (S.A.W).
Kamwe Masahaba hawakunyanyua sauti zao juu ya sauti ya bali walinyanyuliana sauti wenyewe kwa wenyewe kutokana na kutaka kuelewa kuhusiana na makusudio ya amri ya Nabii (S.A.W) kutaka kuwaandikia makhsus na kwa kwamba Nabii (S.A.W) hajuwi kuandika[86],na majadiliano yao yalipozidi baina yao ndio Nabii (S.A.W) akawakatazakuhusiana na khitilafu hizo tu.

Na lau kwamba kungekuwa na jambo linalochupa kiwango hichi ingewateremkia amri toka kwa Allah (Subhanahu wa Ta'aala) inayong'oa kosa hilo toka kwenye mzizi wake.

(Kauli kwamba baadhi ya waliokuwepo: puuzeni maanani) mwanzo inatupasa kujuwa kwamba riwaya hakiufumga ni nani aliyesema kauli hii, huenda ni mmoja wa wanafiki waliohudhuria, au Sahaba aliuliza kuhusina na siha ya Nabii (S.A .W) baada ya kauli yake kuhusiana na kuandika akasema :" basi jee upuuzaji hutokea kama unavyotokea toka kwa mmoja wetu? Hebu hudhurisha kauli hii kwa neno moja.

Au pengine ni katika suala la alieuliza : vipi tusilete bega na kidawa?! Hivi inadhaniwa kuwa Nabii (S.A.W) anadharaauliwa kwa maneno na aseme kwa ghadhabu kama mwenginewe!

Kwani yeye pengine huenda kachanganyikiwa na kusikia maneno ya Nabii (S.A.W) na hivyo kwa sababu ya kukauka kwa sauti yake au kwa sababu ya ziada ya ukavu wa maneno juu ya ulimi wake, kama vile inavyotokea kwa mwernye homa zenye joto kali , na imethibiti kwa makubaliano ya wataalamu wa Sira kwamba Nabii (S.A.W) alikuwa na alikuwa na uzito sauti iliotokea kwenye kwenye maradhi yaliyopelekea kifo chake..

86 Angalia sababu za sharia (127/1),Bihaarul Anwaar (132/16).

Nyenginezo ni nyingi miongoni mwa njia zinazowezekana kuelekezewa,hasa baada ya kuangalia kwetu kwa kwenye Lugha ya Kiarabu, hakuna anaelewa kwa kina hali hiyo aliekuwepo karibu na Nabii (S.A.W), wala hatukuelewa kwa njia ya elimu sio kufungia tendo kwa asiyekuwa Omar, Ali, Ibn Abbas na ni wajibu kwa msomaji kutoona ajabu wingi wa mafunzo haya kuhusiana na neno hili, kwani yule ambaye maneno haya yamesemwa mbele yake kamwe hakumtolea ukali aliyeyasema bali Allah (Subhanahu wa Ta'aala) ambaye hafichikiwi na chochote hakutowa maelekezo yoyote.kuhusiana na kipenzi chake Al Mustafaa (S.A.W).

(Omar kukataa kutekeleza amri ya Nabii (S.A.W)), vipi adhaniwe Omar kwamba anakataa amri nyepesi ya Nabii (S.A.W), nae katika kipindi chote cha usuhuba wake na Nabii (S.A.W) kamwe hakuwahi kumfanyia ubakhili kwa cho chote?

*Ama kauli ya Omar bin Khataab (r.a) kwa Masahaba(r.a) : **("Maumivu yamemzidi nanyi munayo Qur-ankinatutosheleza Kitabu cha Allah"),** inawezekana kulielekeza kama ifuatavyo:Hakika Omar alitaka wasimtilie ngumu Nabii (S.A.W) kwa maneno na masuala mengi, akiwa kwenye ugonjwa mkali, kwa ajili ya kumuonea huruma Nabii (S.A.W),na hili ndilo alilolibainisha kwa kauli yake :" Nanyi munayo Qur-an kinatutosheleza Kitabu cha Allah " yaani hakika Allah (Taa'aala) ameshakamilisha dini yake na kubainisha kwenye sharia zake**{Na hatukuwacha cho chote kwenye Kitabu}**[Al An-a'am :38]; na kama ilivyo kwenye kauli yake :"**{Leo nimekukamilishieni dini yenu na nimekukamilishieni neema zangu juu yenu na nimekuridhieni Uislamu kuwa dini yenu }**[Al Maaidah:3]

Na lile lilowazi kwenye Kitabu alichotaka kukiandika Nabii (S.A.W) ni katika njia ya kukielekeza na kuboresha, na sio jambo jipya lililowajibu kufikishwa, vilevile sio jambo ambalo lazimalifikishwe wala lisilowezakuepukika katika Uislamu, kwani Nabii (S.A.W) ni mwenye kukingwa na kufanya makosa na mwenye kuhifadhika na kuwacha ubainishaji wa aliyoamrishwa kubainishwa kwake na ufikishaji wa yale yaliyowajibishwa na Allah (S.W) kufikishwa kwake.

Na lau kama ni katika anayotaka yale anayotaka Nabii kuyafikisha ni kitu cha wajibu na chenye manufaa kwa ummah hivi jee Allah angelimwachia bila ya kukibainisha kabla ya kifo chake (S.A.W) .

Tukishaelewa yaliyotangulia, hivyo basi itatubainikia kwamba lau jambo hilo ni katika yaliyoamrishwa kuyafikisha wakati wa ugonjwa au siha yake basi angelifikisha kwa hali yoyote ile, na ingekuwa lengo lake ni kuandika jambo la lazima kamwe asingeliwacha kwa sababu ya khitilafu zao, wala za wengine, kutokana na Kauli yake Ta'aala **{Fikisha yale yaliyofikishwa kwako}.**[Al Maaidah :68] Kama vile ambavyo hakuwacha kufiksha yasiyokuwa hayo kwa sababu tu eti ya kwenda kinyume nalo mwenye kwenda kinyume nalo na uadui wa mwenye kufanya uadui, hivyo basi uwachaji wake umejulisha kwamba uandishi wake (S.A.W) unachukuliwa kuwa kwa ajili ya usunna wake na ukumbusho na sio kwa ajili ya uwajibikiwaji na uwekaji wa sheria mpya, nae (S.A.W) akaishi siku nne baada ya hapo, na kamwe hakuamrisha kurejea kuandika.

Tano: Ni lazima kwa muislamu kusafisha moyo wake kutokana na chuki, na bughudha dhidi ya Masahaba wa Nabii (S.A.W), na awapende kama vile ulivyokua uongofu wa Maimamu, na tuseme: Jambo lolote litakapo kukanganya juu jako kuhusiana na haki za Masahaba (r.a) au wenginewe, basi watafutie udhuru (uwatolee), kama ilivyothibiti hivyo toka kwa maimamu (r.a) kwamba walisema: "Mchukulie ndugu yako muislamu kwa ihtimali sabiini za kheri…Hadithi na kauli yao (Allah awarehemu):"Yakadhibishe masikio na macho yako -yasione na kusikia mitelezo ya- ndugu yako " Ama iliosimuliwa kwenye Kaafiy toka kwa Husein bin Mukhtar toka kwa Abi Abdillahi (r.a) amesema :"amesema Amiiril Muumniin (r.a) kwenye maneno yake:"Liweke jambo la ndugu yako kwenye kiwango chake cha juu cha wema mpaka ufikiwe na taarifa itakayokushinda (kufaya hivyo)-wala usidhanie uovu – kutokana na neno moja lililotoka kwa ndugu yako –wakati unaweza kulipatia sababu ya kuwa kwake sio kweli"..Toka kwa

Ubay bin Kaab :"Munapomuona mmoja wa ndugu zenu yupo kwenye jambo lisilokupendezeni basi lifanyieni taawili sabiini".[87]

Ni aula juu yetu kwenda mwenendo wa maimamu, na kutafuta udhuru kwa Masahaba wa Nabii (S.A.W) na yale waliokuwa nayo wakati wa kuwa pamoja na Nabii (S.A.W) na yale yanayoleta utata wakati wa kuyaona na yale yanayopatikana katika maumivu makubwa akiwa katika hali ya sakaratulmaut.

Allah amewasifu kwa kauli yake **{Mulikuwa umati bora uliotolewa kwa ajili ya watu munaamrisha mema nakukataza maovu na kumuamini Allah }**[Aal I'mraan :110] nao wao walikuwa wakipinga baadhi ya masuala ya kifiqhi kwa uchache zaidi wa hayo.
Na kwanini basi tuwatie dosari leo hii baada ya kupita karne hizo kadha kwa Masahaba wa Nabii (S.A.W) kwa tukio hili na mengineyo! na nini malengo yetu katika jambo hilo? Hivi sisi ni wajuzi na wenye pupa juu ya Nabii (S.A.W) kuliko yeye mwenyewe?
Hivi sisi tunampenda Nabii (S.A.W) zaidi kuliko Masahaba zake(r.a)!

Au sisi ni watu wa matamanio ya nafsi ?!

Sita : Hakika uelezeaji wa Ibni Abbas (r.a) kwa yale yaliyotokea kwenye (raziyyah) alipokuwa akisimulia Hadithi hakuwepo pale tukio lilipotokea, lakini alikuwa akilieleza hilo baada ya tukio hilo kwa miaka kadha, pale alipokuwa akielezea kifo cha Nabii (S.A.W) na huzuni yake,na riwaya zote zinajulisha hivyo.

Saba: Lau tutendeleza njia ya utiaji ila na upekuzi basi jibu itakuwaje pale mmoja wa Nawasib atakapotwambia:'Kwamba Ali bin Abi Talib ndie sababu ya matatizo hayo, kwani yeye ndiye aliekuwa mara nyingi akipingana na Nabii (S.A.W),wala hatekelezi amri zake, kama vile ilvyotokea kwenye Suluhu Hudaibiyyah katika kutofuta jina la Nabii (S.A.W), kutonyoa nywele na kuchinja

87 Angalia 'Hadaaiqi nadhwirah (353/15).

hadyi yake kama Masahaba wengine, na kutokubali kuwa mwakilishi wake Madina kwenye vita vya Hudaibiyah.

Bali pia alishirikiana na wenginewe katika kupinga amri ya Nabii (S.A.W) ya kuleta bega na kidawa ili waislamu wasipotee, na hakupeleka hayo mpaka Nabii (S.A.W) alipokufa, bali alibadilisha hukumu za sheria za kiislamu juu ya wachupaji mpaka (Ghulaat) kwa kuwaadhibu kwa kuwachoma moto na kuwacha kisasi cha kisheria.[88]

Hivyo kwa suala hili mpango wa maadui wa Uislamu na wale waliosimamisha uadui kwa Ahlil Bait na wale waliosimamisha uadui dhidi ya Masahaba wa Nabii (S.A.W) unajiweka wazi.

Suala la Sita:
Msimamo wa Abubakri (r.a)kuhusiana na mirathi ya Fadak-

shamba katika Khaibar-**:**
Lau muulizaji angetwambia :Ewe Muislamu utasemaje kwenye msimamo wa Abubakri (r.a) pale alipokuwa hakumpa Fatma haki yake toka kwenye mirathi yake kwenye ardhi ya Fadak na nyenginezo ,baada ya kifo cha baba yake (S.A.W), na akafa akiwa hamsemeshi? pamoja na kwamba Allah (S.W) ameweka mirathi kwenye Kitabu ChakeKitikufuAkasema : **{Allah anakuusieni kwenye watoto wenu, mwanamme anayo haki ya wanawake wawili… }** [An N isaa:11] na akaamua hivyo hivyo baina ya Manabii, akasema kuhusiana na Zakariyya (a.s): **{Na Hakika mimi naogopa viongozi bada yangu na mke wangu ni tasa hivyo nipe msimamizi toka kwako anirithi mimi na awarithi katika kizazi cha Yaqub, mjaaliye awe mwenye kuridhia }** [Maryam :5-6] na Allah(S.W) akasema kuhusiana na Suleiman (a.s){ Na Suleiman akamrith Daud} [An Naml:16]
Na sababu ya matendo haya kwa bibi wa wanawake wa walimwengu wote (a.s) basi atakuwa amemkera Nabii (S.W.A) kutokana na kauli yake kuhusiana na haki yake: ”Hakika Fatma ni kipande cha kiwili wili changu,yeyote atakaemghadhibisha atakuwa amenighadhibisha mimi ”

88 Angalia Bih’aaril Anwaar(414/34)

Jibu :
Mwanzo :inapasa tusisahau kwamba Fatma na mumewe wanaayo hadhi kubwa mbele ya Abubakri (r.a) na wenginewe katika Masahaba(r.a)

Na katika dalili za hadhi hiyo ni kwamba Abubakri (r.a)ndiye aliyeashiria kwa Ali (r.a) kwa kumuowa kwake Azahraa (a.s)[89] na kuamrishwa kwake na Nabii (S.W.A) kusimamia kutayarishwa kwake-Azahraa-kwa ajili yakuolewa na Imam Ali (r.a)[90]na mke wake Asmaa bint 'Umeis vilevile akashirikiana nae katika kumuandaa Fatma siku ya arusi yake; na Fatma Azahraa (s.a) alipofariki mke wake Abubakri (r.a) nafsi yake alisimama mbele kuandaa sanda ya Fatma Azahraa a.s) na kumkosha.[91]

PILI
Huenda waislamu walio wengi leo hii wanajingikiwa kuwa ilikuwa ni Fay-i –mali wanayoupata waislamu toka kwa makafii vitani bila ya vita-toka kwa Allah juu ya Mtume (S.A.W) kutokana na Khaybar, na Fay-a ni ngawira inayokuwa bila ya vita na kisa hichi kimetajwa kwa urefu wake kwenye Suratl H'ashr amesema Allahu Taaa'ala: **{ Na ile fay-a aliompatia Allah Mtume wake toka kwenye watu wa vijiji basi ni kwa ajili ya Allah, Mtume wake, wenye ujamaa, mayatima, maskini ,na wasafiri ile isije ikawa kinyang'anyiro baina ya matajiri miongoni mwenu, na kile alichokupeniMtume basi kichukuweni na kile alichokukatazeni basi kiwacheni na mumche Allah ,hakika Allah ni mkali wa adhabu}**[Hashr;7] .

Na ile fay-i Allah aliompa Mtume (S.A.W) basi ni yake (S.A.W) na Nabii (S.A.W) akaijaalia kwenye haja zake, watu wa nyumbani mwake na sadaka zake, nae alikuwa akiisimamia na kuishughulikia, na kamwe haikurithiwa na jamaa zake,nayo imeandikwa kwenye vitabu vya historia, alipofariki Nabii (S.A.W), Abubakr akawa ndiye alieshika nafasi yake katika jambo hilo na

89 Bih'aaril Anwaar(138/43)

90 Bih'aarul Anwaar (94/43)),Al Amaaly cha At Tusy: (uk.40) .

91 Bih'aarul Anwaar(185/43)

baadae Omar, na katika wakati wake Imam Ali bin Abi Talib na Abbas wakaomba waisimamie wao na Omar akakubaliana na rai hiyio, hivyo usimamizi ukawa juu kwao, na likawa kwa Imam Ali na kuendekela kuwa kwenye mikono yake kwenye utwala wa Omar na Othman na kipindi chake, na baada ya kifo chake Al Hasan bin Ali aksimamia yeye baadae Imam Husein, halafu Alhasan bin AlHasan (Al H'asan Al Muthannaa), na pamoja na Ali bin Husain, baadae Zaid bin Hasan, baadae na Hasan hakuzuwia na kamwe hakuna aliyeizuwia.

Tatu:
Ama kuhusiana na kadhia ya mirathi, alishatowa habari kwa Masahaba kwamba Manabii hawarithiwi mali wala dinari baada ya vifo vyao kinyume na watu wengine, kitakachobakia katika mali zao basi ni sadaka,na hivyo ndivyo walivyofahamu na kubainishwa na maimamu (r.a) baadae.

Toka kwa Abi Abdillahi (r.a)amesema :"Amesema Mtume (S.A.W) :" Yeyote aliefata njia akitafuta elimu kwenye njia hiyo, basi Allah atamuwepesishia kwayo njia ya kwenda Peponi, na kwamba Malaika huweka mbawa zao kwa wenyekutafuta elimu kwa ajili ya kumridhia na kwamba walioko mbinguni na ardhini humuombea maghufira, mpaka hata samaki baharini, na ubora wa mwenye elimu juu ya mfanyaji ibada ni ubora ni Mwezi juu ya sayari nyengine usiku wa mbaamwezi, hakika wanazuoni ni warathi wa Manabii, na hakika Manabii hawakurithiwa Dinari wala Dirhamu, lakini walirithiwa elimu hivyo aliechukua toka kwenye elimu hiyo amechukua sehemu yenye kutosheleza.[92]

Abi Abdillahi (a.s) amesema vile vile: " Hakika wanazuoni ni warathi wa Manabii na hivyi ni kwa sababu Manabii hawakurithiwa dinar wala dirham bali walirithiwa Hadithi katika Hadithi zao, hivyo aliechikua kitu cho chote katika hilo basi amechukuwa sehemu iliyokubwa.[93]

92Al Kaafy(34/1), Bihaarul Anwaar1(64/1),Amaaliyas Swaduuq(uk. 60) ,Baswaairuld Darajaat(uk. :3) Thawaabul Aa'maal (uk. 131),A'waalyl Aaly⊗358/1)

93 Al Kaafy(32/1), Al ikhtiswaaasw(4)Wasaaili Shiia'a (78/28), Mustadrakul Wasaai-l(299/17)

Kutoka kwa Jafar toka kwa baba yake (a.s) Hakika Mtume hakurithiwa dinar wala dirham, mtumwa wala suria, wala mbuzi wala ngamia, kwa hakika alitolewa roho Mtume (S.A.W) wakati ngao yake iko rahani kwa myahudi katika wayahudi wa Madina kwa pishi ishirini za shairi, aloikopa kuwa ni chakula kwa ajili ya watu wake)[94]

Basi huyu anaemiliki Fadak anakopa pishi ishirin na aweke rahani ngao yake!
Nae Amiril Mu-u-miniin(a.s) akasema:"Elimu ni bora kuliko mali kwa sababu saba:

Kwanza : Ni mirathi ya Manabii na mali ni mirathi ya Mafir-a'auna.

Pili: Elimu haipungui kwa kuitowa, mali hupungua kwa kutolewa.

Tatu:Mali inahitajia muhifadhiji, na elimu huhifadhiwa na mwenyewe.

Nne: Elimu huingia kwenye sanda ,na mali hubakia.

Tano: Mali hupatikana na muislamu na kafiri,na elimu haipatikani ila na muislamu tu.
Sita: Watu wote wanamuhitajia mwenye elimu kwenye mambo ya dini yao na hawamuhitajii mwenye mali.
Saba :Elimu humpa nguvu mtu kupita kwenye Siraat na mali humzuwia"[95]

Nane: Ama kauli ya uhaki wa Fatma kwenye mirathi ya baba yake kwa utoleaji dalili kauli yake Taala:{**Na kwa hakika mimi nimeogopa wasimamizi wa mambo nyuma yangu na mke wangu wangu alikuwa ni tasa, basi unipe msimamizi wa mambo atakaenirithi mimi na atakaerithi jamaa wa Yaqub na Ewe Mola mjaalie mwenye kukubalika }** [Maryam :5-6]na Kauli

94 Qurbul Isnaad (uk. 44) Bihaarul Anwaar (219 /16).

95 Bihaarul Anwaar (185 /1).

yake Taala**{Na Daawuud akamrithi Suleiman}** [An Naml :16], ni utoleaji dalili batili toka kwa wasiokuwa na elimu, kunakojulisha uchache wa elimu zao kwani mirathi iliyotajwa hapa ni mirathi ya Unabii, elimu na Hikma, na sio mirathi ya mali, na hivyo ni kutokana na dalili za kunukuu na kiakili: Ama za kunukuu zimeshapita, ama za kiakili hujulikana kama ifuatavyo :
Aya ya mwanzo ambayo ni kauli yake Taala **{atakaenirithi mimi na atakaerithi jamaa wa Yaqub }** [Maryam : 6]

Amesema Seyyid Muhammad Husein Fadhlullaahi: Ili awe endelezo la hadhi ya utume ambao watalingania kwa Allah na kumfanyia kazi, apigane kwenye njia yake, ili ujumbe uendelee kwa sababu yake kwenye roho, fikra na elimu yake.[96]

Jee inaingia akilini kwa Mtume wa Allah anaechunga kuingia Pepo yenye kubakia amuombee mwanawe dunia yenye kutoweka? hili alimstahikii mtu mchaji wa Allah kumuomba Allah amruzuku mtoto sio kwa ajili yoyote ile ila kwa ajili ya kumrithi dunia inayotoweka.?
Manabii wa Allah Tabaraka wa Taala wao ndio vigezo vilivyobarikiwa na wao huamrisha watu kufanya mema na kuifanya, basi iwapo huwausia watu mali waitowe basi itakuwaje wawabakishie watoto wao jambo hili la kidunia lenye kutoweka?**{ Hivi jee munawaamrisha watu kufanya mema na nyie munasahau nafsi zenu hivi nyie hana akili }** [Al Baqarah :44],bali huwaona wakiitolea swadaqa katika njia za kheri .
Na katika yanayobainisha kauli na kuiweka kwenye uwazi na kwamba mirathi ka**,** tika maneno ya Zakariyya (a.s) haikuwa mali inabainishwa na nukta ifuatayo.

Lau tungeikamilisha Kauli yake Taala:**{… na atakaerithi katika jamaa wa Yaqub }** [Maryam : 6] inatubainishia kwa uwazi na bila ya tia toa kwamba mirathi iliyokusudiwa ni elimu na Unabii na sio kitu chengine.

Na wallahi lau ombi toka kwa Nabii wa Allah Zakariya lingeambatana na mali basi jee ingewezekana kwa mtafiti yo yote

96 Tafsiiru wahyil Qur-aan (Suurat Maryam : 6)

yule katika historia atupe habari ni watu wangapi walikuwa kwenye nyumba ya Yaqub? bali iko wapi nafasi ya Yahya katika aal Yaqub?

Msomaji –mwenye inswaaf- kwenye vitabu vya historia baada ya kusoma Kitabu cha Allah Taala anaelewa kwa uhakika kwamba kila Nabii katika Manabii wa Bani Israil ni katika Aali Yaqub, kwani Israil ni Nabii wa Allah Yaqub (a.s), hivyo basi vipi Bani Israil wasiokuwa manabii ? na pamoja na idadi hii kubwa sehemu ya Yahya ni kiasi gani?

Hivyo basi hapana shaka kwamba ufahamu wa Kauli yake Taala:**{… na atakaerithi katika jamaa wa Yaqub }** [Maryam 6] ni kutokana na ufahamu wa Wanazuoni, vile vile uzingatiaji wa kiwango cha juu katika Tafsiri tukufu na uangaliaji wa kihistoria unapinga kauli ya anayesema :"Hakika Aya inazungumzia mirathi ya mali .

Na kwa mtazamo wa kiakili tu ni kwamba mara alipotajwa Yaqub kuwa ni Nabii, na Zakariya vile vile ni katika Manabii ufahamu uliosahihi unalazimisha tuelewe kwamba alitaka mirathi ya unabii, elimu na hekima na kamwe hakukusudia mirathi ya mali, na kwamba Zakariya hakuwa tajiri bali alikuwa seramala akila kutokana na kazi ya mikono yake, basi aipate wapi mali hiyo itakayarithiwa na Yahya ?!

Ama utoleaji wa dalili wa Aya ya pili Kauli yake Taala:**{Na Daud akamrithi Suleiman}** [An Naml :16] vile hakurithi mali toka kwake, bali imekusudiwa mirathi ya Unabii, hekima na elimu.
Amesema Sheikh Mohammad ASabzawaariy An Najfiy: "Yaani alimrithi ufalme na unabii kwa kukaa nafasi yake na sio mwanawe mwengine nao ni kumi na tisa .[97]

Na ni jambo lijulikanalo katika Historia kwamba Nabii wa Allah Daud (a.s) anao wake wengi na idadi kadha ya masuria, na Allah akamruzuku watoto wengi, hivi tuseme kuwa hakurithiwa na ye yote isipokuwa Suleiman ?

97 Tafsiirul Jadiid ,na angalia Tafsiiril Mui'in(Suurin Namli :16).

Inajulikana vile vile ndugu hurithi toka kwa mzazi wao, hivyo kuifanya mirathi makhsusi kwa Suleiman tu sio sahihi wala uongofu ikiwa anao warathi wengine.

Hata tukikubali kuwa mirathi inahusika na mirathi ya kidunia, hivyo basi kuna faida gani ya kutajwa kwenye Kitabu cha Mola wetu Tabaraka wa Taala, na hivyo ni kwamba ni katika maumbile kwamba mtoto atamrithi baba yake? hivyo basi ipo wapi Balagha , ibara au faida katika Kitabu cha Mola wetu kutajwa kitu ambacho kutokea kwake kunajulikana kwa watu

Tano : Na hapa mpendwa –msomaji - anawezakusimama kisimamo kifupi na kujiuliza :
Jee Fatma Zahraa (a.s) aliotaka Fadak toka kwa Abubakr kwa sababu ni urithi au kwa kuwa ni hiba na zawadi toka kwa baba yake (S.A.W) aliyompa hiba na zawadi yeye baada ya ukombozi wa Khaibar?
Hivyo ni kwamba makusudio ya kujiuliza huku matunda yake ni kwamba mipaka yake itadhihiri mwisho wa kisa, hivyo ni kwa sababu kwamba Fatma (a.s) baada ya kuuliza kwake Fadak toka kwa abi Abubakr na Abubakr kutaja hoja yake ya kuzuwia aliondoka na hakumjadili, basi jee kitu hichi akikitaka kwa kuwa ni mirathi au ni hiba toka kwa baba yake.iwapo ni mirathi basi Manabii hawarithiwi dinari wala vifaa kama tulivyobainsha kwenye kauli, na iwapo ni hiba Nabii (S.A.W) aliyompa Fatma (a.s) basi inapasa hapa tusimame kidogo na kujiuliza pia katika hili. Hivyo tunasema:

1- Nabii (S.A.W) kamwe hakumpa Fadak Fatma kwenye wakati wowote ule, na hilo alilielewa Fatma pale aliitaka kwa Abubakri, akaitaka kwa misingi kwamba ni katika njia ya mirathi, sio katika njia ya hiba, na kihistoria inaeleweka kwamba ukombozi wa Khaibar ulikuwa mwanzo wa mwaka wa saba Hijriyyah, na Zainab bint Nabii (S.A.W) alifariki mwaka wa nane Hijriyyah, na dada yake Ummu Kulthuum alifariki mwaka wa tisa Hijriyyah, hivyo vipi basi ampe Fatma makhsusi peke yake na awawache dada zake Ummu Kulthum na Zainab(a.s)?!

Hivyo hii ni tuhuma iliyo ya moja kwa moja kwa Nabii (S.A.W) kwamba anatofautisha baina ya watoto wake, na hilo ni hasha kwa Nabii (S.A.W) .

2-Tuchukulie kuwa hivyo ndivyo, lau tutasema kwamba Fadak ilikuwa hiba kwa Fatma (a.s) basi huenda (a.s) akawa ameikabidhi au la !

Iwapo bado alikuwa ameshaikabidhi, hivyo kwa nini aitake toka kwa Abubakri (r.a) ? na iwapo alikuwa hajaikabidhi basi hiba kisheria ikiwa haijakabidhiwa aliyepewa hiba hiyo ni kama hajapewa, na wakati huo huwa ni haki warathi baada ya mauti ya mtoaji hiba.
Sita :Ni jambo linalojulikana katika Fiqhi kwetu kwamba mwanamke hana mirathi kwenye mirathi ya mashamba bali hupewa kima chake, na hivi ndivyo ilivyosimuliwa kutoka kwa wanazuoni :

Toka kwa Yazid As Saaigh amesema :"nilimwambia Aba Abdillah kuhusina na jee mwanamke wanarithi ardhi ? akasema :" La lakini hirithi kima cha jengo, akasema: nikamwambia kwani watu hilo hawaliridhii, akasema tutakapo pata madaraka wasiliridhie tutawapiga kwa bakora, na wasipotengenea tutawapiga kwa panga"[98]

Na kutoka kwa Abaan il Ahmar amesema :" hilo silielewi ila toka kwa Muyassir Bayyaaa' Zaitw'iy, akmesema nilimuuliza yaani Abu Abdillahi - kuhusiana na wanawake nini wanacho katika mirathi ,akasema wanayo haki ya kima cha matofali, jengo, mbao na mianzi, ama ardhi na mashamba wao hawana mirathi, akasema : nikamwambia nguo? akasema nguo wanayo sehemu yao,akasema : nikamwambia : "imekwendaje hili na, kima hichi na nae anayo robo iliyotajwa?"

Akasema :"ni kwa sababu mwanamke hana nasabu anatoirithia, ila yeye ni mwenye kuingia kwao, na kwamba hivi imekuwa hivyo ili

98 Al Kaafy (129),na angalia :Wasaaili Shiia'a (70/27) Tahdhiibul ahkaam(299/9).

mwanamke asijeolewa akaja mume au mwanawe akawafanyia watu kwenye shamba yao .”[99]

Saba : Sababu sahihi na bayana inayotosheleza kwa yaliyotokea baina ya Zahraa na Abubakri (r.a) ni kama ifuatavyo Insha Allah :”Bibi wa wanawake wa Peponi (a.s) kamwe hakudai asichokuwanacho, ila (a.s) alitaka kile alichodhania kwamba ni haki yake, na baada ya Abubakri kumbainishia sababu ya kuzuwiliwa mirathi,(a.s) akaenda zake na kamwe hakuzungumza nae kuhusiana na jambo hili mara nyengine.

Na jambo linashuhudia usahihi wa sababu na bayana hii : ni vile alivyokwenda-alivyofanya - (a.s)- kwa kutowapa Fadak watoto wake pale aliposalimisha Ukhalifa wa waislam, na pale alipotakiwa kurejesha alisema: ”Hakika mimi namuonea haya Allah kukirejesha kitu alichokizuwia Abubakri, na kuendelezwa na Omar[100]”, hvyo basi ikiwa hukumu juu Abubakri kwamba ni dhalimu kwa kuzuwia kwake haki ya Zahraa (a.s) basi jee hukumu hiyo pia itamteremkia Imam Ali (a.s) -Allah atulinde-,kwani hakuwarejeshea wanawe haki katika mirathi ya mama yao ?

Na kipenzi cha Aalil Sheria na waislamu wanawatakasa wote kutokana na dhuma, anawatakasa wote tutokana na dhulma, na kujiweka mbali na kumdhania vibaya Abubakri.(r.a) na wenginewe, na haya ndiyo yanayobainika kwenye nukta mbili zifuatazo:

Nane: Kamwe Abubakri hakuiwacha mali hii kwa bintie Aisha wala yeyote katika mama wa waumini, bali uhramishwaji ulihusisha Aalil Bait wote, na jee kushikamana na wasia wa Nabii (S.A.W) ni makosa!

Tisa: Sio lazima Abubakri kutompa mirath Fatma iwe kunajengeka juu kumchukia kama wanavyoeneza watu wa fitina**.**

99 Al Kaafy (130/7),

100 Sherhe Nahjul Balaagha (252/16).

Nabii (S.A.W) vile vile hakumpa mtumishi Fatma, binti yake pale alipomuomba, nalo ni jambo la mubaha katika na anisaidie katika mambo ya nyumba, akamwabia ewe Fatma! hivi wewe hutaki bora zaidi kuliko mtumishi? Aliakamwambia :"sema ndiyo akamwambia Ewe baba yangu :bora kuliko mtumishi akamwambia : umsabihi Allah, kila siku mara thalathini na tatu, na umuhimidi mara thalathini na tatu, na aseme Allahu Akbaru,hivyo hivyo mara thalathini na nne, hizo ni mia kwenye ulimi na mema elfu kwenye mizani "[101] .

Kumi:Kauli kwamba Nabii (S.A.W) kwamba alikuwa akighadhibika kwa ghadhabu za Fatma (a.s), hili ni sahihi wala watu wawili hawatofautani kwa hili .

Ieleweke kuwa kumzuwilia kwake Abubakri hakukusudia kumghadhibisha, kwani uzuwiaji huo ulikuwa utekelezaji wa amri ya Mtume wa Allah (S.A.W), na hili Sidiq wala mwenginewe hatiliki aibu anapolifanya.

Wala hailazimiki kwamba kila ghadhabu anayoghadhibishwa kwayo Zahraa (a.s) linamghadhibisha Nabii (S.A.W), kwani paqlitokea tofauti kadha za kifamilia baina ya Imam Ali na Zahraa mfano wa yaliyotokea baina ya wake -na waume zao basi jee tutie dosari kwenye uadilifu wa Alikwa mujibu wa walivyofahamu baadhi yao kwa mujibu wa Hadithi ya kughasadhibishwa Fatma vile vile moja kwa moja, na tuseme: kwamba Mtume (S.A.W) amemughadhibikia Ali kwa kumghadhibisha kwake Fatma?!

Bali Nabii (S.A.W) alisimama baina ya binamu yake na baina ya binti yake bibi wa wanawake wa Peponi msimamo wa uadilifu na insafu , na sio msimamo wa huruma na hamasa za kibaba!

Toka kwa Abi Dharri (r.a) amesema :"Nilikuwa mimi na Jaafar bin Abi Talib tulihajiri kueleka Habasha, Jaafar akapewa zawadi ya kijakazi chenye thamani ya dirham elfu nne, basi tulipofika Madina akampa zawadi Ali bin Abi Talib amuhudumie basi akamuweka kwenye nyumba ya Fatma, siku moja Fatma akaingia akaona

101 I'lali Sharaai'i (163 /1),Al Manaaqib(342/3),Bihharul Anwaar(208/39)

kichwa cha Ali kwenye chumba cha kijakazi, akamwambia ewe Abal Hasan! umefanya hivyo? akamwambia hapana Wallahi! Ewe bint Muhammad! sijafanya chochote kwani unataka nini? akamwambia unaniruhusu niende nyumbani kwa baba yangu Nabii (S.A.W) ? akamwambia nimeshakupa idhini . akavaa jilbabu lake, akielekea kwa Nabii (S.A.W), Jibril (a.s) akamwambia:"Ewe Muhammad hakika Allah anakusalimu, na anakwambia :Hakika Fatma huyu amekujia kukushtakia, hivyo usimkubalie chochote kuhusiana na Ali!!, Fatma akaingia akamwambia Nabii (S.A.W) :"Umekuja kumshtaki Ali akasema naam; naapa na Mola wa Kaaba akateremka! akamwambia:" Rejea kwake, akamwambia lazima akuridhishe"[102]

Toka kwa Jaafar bin Bin Mohammad (r,a) amesema:"Fatma alimshtaki Alikwa Mtume wa Allah akamwambia ewe Mtume wa Allah !hawachi chote chote katika riziki yake ila anaigawa kwa maskini !akamwambia :"Ewe Fatma !hivi wewe unanichukia kwenye ndugu yangu na binamu yangu, hakika kumghadhibisha yeye ni kughadhibika kwangu, kughadhibika kwangu ni kughadhibika kwa Allah Azza wa Jalla)[103]

Kumi na Moja : Na tujikumbushe mwanzoni kwamba hakika miongoni mwa malengo ya maadui ya uislamu ni kuvunjavunja umoja wa waislamu kupitia kwenye kauli za batili za kubabaisha babaisha, na kueneza habari za uzushi zenye kuonesha kuchukiana na kubughudhiana kwenye kizazi cha mwanzo kilichobarikiwa, na lau tungeuliza nafsi zetu na kutumia akili zetu, tutafaidika nini kutokana na kisa kinachorejewa rejewa kila wakati kwenye baadhi ya majlisi za waislamu kila mwaka ili kuchochea nyoyo na kuvumisha pepo ili kuzifikisha kwenye hali za kinafsi mwisho wake ni kueneza uvumi wa kuwepo uadui uliochopea dhidi ya Ahlil Bait. ya Mtume (S.A.W)

Hivyo mwenye insafu, mwenye akili lau angetafiti alivyofanya Abubakr kwa Fatma (a.s) wakati alipotaka ardhi ya Fadak, angeona kwamba vile alivyo hukumu Abubakri kuhusiana na ardhi ya Fadak

102 Ilal Sharaaii':(163/1) ,Al Manaaqib (243/3) Bihaaril Anwaar (208/39) .

103 Bihaaril Anwaar(153/43) na angalia Kashfil Ghumma h:(473/1)

hakukua ila kwa mujibu wa nasi ya kisheria iliyotokana na aliekingwa na kufanya makosa ambaye kutiiwa kwake ni jambo lililofaradhishwa, basi ni ipi dhambi yake kuhusiana alichoamrishwa na akakitekeleza?!

Na kwa hivyo tutasema kwa mpakaji matope miongoni mwa nawasib kwa bibi wanawake wa peponi anaposema kuhusiana na yeye :
Mambo ya Fatma ni mageni !anahamaki na kwenda kinyume na waislamu wote, mpaka hasama na kuchama kwake kufukilia kuwa ya mile mile ambayo imekatazwa na uislamu, na hilo halikuwa ila ni kutokana na matamanio ya nafsi yake , na wingi wa kupenda kwake mali na takataka za dunia yenye kutoweka, kama vile yaliyotokea baina yake na Khalifa wa Nabii (S.A.W) Sidiq katika kudai kwake mirathi na kutotekeleza kwake wasia wa baba yake Nabii (S.A.W), na vile vile alikuwa mwingi wa kumfanyia fujo Nabii (S.A.W) kutokana na kuhoji kwake kwenye kuendelea juu ya mumewe, Ali bin Abi Talib kutokana na ufakiri wake na uchache wake wa mali, na baada ya hapo vilevile, na hivi ndivyo ilivyoelezwa na riwaya zilizothibiti, kama vile:

Toka kwa Abi Is-haaq As Sabii'iy, toka kwa Haarith, toka kwa Aliamesema:" Hakika Fatma alishitaki kwa Nabii (S.A.W) akamwabia:"Hivi wewe huridhiki mimi kukuozesha mtangulizi wa umati wangu kwa uislamu, mpole wao, mwingi wao wa elimu? Hivi wewe huridhii wewe kuwa bibi wanawake wa Peponi, isipokwa tu vile Allah alivyojaalia kwa Maryam bint Imraan, na kwamba watoto wako wawili wa kiume Hasan na Husein ni mabwana wa watu wa Peponi ?"[104]

Toka kwa Abii Saleih toka kwa Ibni Abbaas :"Hakika Fatma (a.s) alilia kwa sababu ya njaa na upungufu wa nguo, hivyo akaambiwa na Nabii (S.A.W) Kinai – ewe- Fatma kwa mumeo, kwani naapa kwa Allah : hakika yeye ni bwana duniani bwana Akhera, na atakapopatanisha baina yao .." [105]

104 Amaaliy At Tw'uusiy:(248)

105 Limnaaqib(319/3),Bihaarul Anwaar:(99/24)

Hivyo ewe kipenzi cha Aalil Beit ya Nabii (S.A.W) hivyo wewe unaridhia kuwa kwenye kundi la wachukivu wenye vitimbi kwa Aalil Beit waliotoharika kama nawaaswib na wengineo? Au au wewe unalinda himaya ya Aalil Bait kupitia kwenye kukamatana na mwongozo uliosahihi uliobarikiwa, pamoja na ya salama wa moyo wako kuhusiana na wale waliokuwa pamoja na bwana wa watu Muhammad (S.A.W) ? lipi katika makundi mawili haya unachagua?
Suala la saba: ((Kauli ya udhalilishaji wa Abubakr kwa Fatma)):
Lau msemaji angetwambia :nini mnasema juu yale yaliofanywa na Abubakr Sidiq, Omar, Khalid (r.a) baada ya kifo cha Nabii pale walipohujumu nyumba ya Ali (a.s), wakamfunga kamba, wakampiga mkewe mpaka wakamvunja ubavu wake na kutowa mimba yake, na wakachoma nyumba yao, kama riwaya za kihistoria zilivyosimulia.

Hivyo jee vitendo hivi viovu vinajulisha mapenzi na mshikamano ,au kushikana, ugomvi na kutoshikamana na Ahlil Bait wa Nabii (S.A.W) ?

Jibu :
Kwanza :haimpasii mtafutaji wa haki kung'ozoka kwa kusoma tu riwaya ya kihistoria na nyenginezo zinazozungumzia vipenzi vyake, wala kujuwa kianzio chake,seuze kwamba anaelewa sahihi na mbovu zake. Wala kamwe asighurike na wingi wa riwaya za uongo kwenye tukio maalum japo likkiwa mashuhuri.

Pili :hakika kisa hichi ni katika uzushi unaotumiwa na watu wa fitina katika kupasua na kufarikisha safu za waislamu, nasi tunamtaka kila mtafiti wa haki ajitahidi na kufanya utafiti riwaya moja iliyo sahihi inayotegemezewa kisa hicho za kuzushwa na riwaya inayokwenda na misingi ya na masharti ya hadithi sahihi, katika kuungana kwa sanad, na riwaya ya Imamu muadilifiu mwenye hifidhi iliyo madhubuti .

Na katika maajabu ni kwamba tunawaona wengi wanaokamatana na kisa hichi wanayo imani ya yakini juu ya riwaya hizo, kwa kufuata huruma tu bila ya kuangalia kwa mtazamo wa mwenye

akili mtaalamu katika dini yake kama vile kutafiti kwenye kushi na kutosihi kwa sanad!

Amesema Seyyid Haashim Maa'ruuful H'asaniy baada ya kuleta riwaya zinazoelezea juu ya yaliyotokea kwa Zahraa (a.s)..kuelekea kwenye riwaya nyingi sanad zake zisiszo thibiti kwa misingi ya udadisi wa kielimu.[106] Na akasema vilevile :"vyovyote hali iwavyo ,ni kwamba hadithi kuhusiana na Fadak na mirathi ya Zahraa toka kwa baba yake na misimamo yake kuhusiana na hilo toka kwenye ukhalifa ni ndefu na nyingi, na bila shaka wapenzi na maadui wamezusha sehemu kubwa miongoni mwa zile zilizomo kwenye mikono ya wasimulizi na baada ya utafiti na upekuzi kamwe hakuna inayothibiti isipokuwa kidogo katika kidogo.[107] Amesema kwenye kashfil-ghitaa :"lakini kadhia ya kupigwa kwa Fatma Zahraa, na kupigwa mashavu yake ni katika mambo yasiyoingia akilini wala kukinaisha mawazo sahihi ,sio kwamba kaumu inaonea vibaya jambo hilo na kuhofu ukatili huu mkubwa ,bali ni kwamba tabia za kiarabu na silka za kijahiliya zimetiliwa nguvu na Sheria ya kiislamu na kusisiza nguvu –zinazuwia kwa nguvu zote kupigwa kwa mwanamke.

Seyyidul Khawi-iy aliulizwa kuhusiana na kusihi kwa kuvunjwa ubavu Zahraa akawajibu :"kwa umashuhuri –kwenye itikadi ya baadhi ya watu- , na kamwe hakuhukumu kwa kusihi kwake.[108]
Tatu inaweza ikasemwa kwamba Ali aliamrishwa kutopigana na Masahaba walipomfanyia uadui mke wake Bibi wa wanawake wa Peponi (a.s), kwa ajili ya kuhifadhi bendera ya Uislamu isianguke na watu wa Milla wasifarikiane baada ya kifo cha Nabii,na kuamrishwa kuvumilia maudhi yao .

Lakini sisi tunasemana kujiliza :
Kwa kunzia tunasema ea umbali wa maneno haya na usahihi, na hata tukichukulia kutekea hayo yaliyosemwa ,basi kwanini akapigana nao siku ya Jamal na jeshi la Talha na mama wa waislamu pale walipotoka kuelekea Kuufah -nae alikuwa Makkah –

106 Angalia Siiril Aimma ahtil ithnaa'shariyyah :(133/1)

107 Maswdar ilyotangulia (140/1).

108 Angalia : Jannatul Ma-a-waa :(uk.135)

akalipiga vita jeshi la Mua'awiya baada ya hapo -Swiffiin-, na hivyo hivyo Katika Nahraan pale alipowapiga vita Khawaarij,basi kwanini pakatokea vita vyote hivi na umwagikaji wa damu, jee vitendo hivyo hajulishi utupiliaji mbali wa wasia wa Nabii (s.a.w) baada ya kutofautiana kwa kundi la waislamu?

Lakini usahihi unaendana na matukio ni kwamba Ali hakumuamrisha yeyot kwa kutokuwepodhulma juu ya mke wakemtukufu na kwamba hakumuombea nusra ,na riwaya hizi kabla ulimi wa muislamu kajatamka chochote kuhusiana na riwaya hizi akumbuke hali ya Amiril muu-miniiin na wivu wake juu ya dini ya Allah, kasha juu ya mkewe toka kwenye nyumba ya Mustafa (S.A.W) .

Na kwa hakika imethibiti toka kwa As Swaadidiqil Amiin kwamba amesema :"Alieuliwa akitetea kudhulumiwa kwake basui huyo ni shahidi"[109]

Hivyo basi huyu anaeitakidi anamuhofia Amiiril Mu-u-miniin na shujaa wa mashujaa?!
Na tahadhari muislamu mwenye akili kutamka maneno yatakayokuwa dhidi yake na yasiyokuwa kwa ajili yake, yasiyokuwa na nusra kwa Ahlil Bait watukufu, hivyo ni kwamba anaedai kwamba Ali alikuwa shujaa, akapiga vita jeshi la Talha na wa baadae miongoni mwa watu wa Swiffiin kwa ajili ya kunusuru uongozi, kwanini alikuwa mbali na kuwanusuru watu wa nyumba yake pale walipopigwa mpaka kukaribia kuuawa?!

Nne Kila mwenye fitina anaweza-asiefungika na riwaya sahihi-akasimulia riwaya bila ya sanad sahihi, kwa kuziona kwake tu na kuenezwa kwake kwenye baadhi ya vitabu vya kihistoria na kifasihi, na kuamini baada ya hapo, na kwake zikawa katika yanayokubalika kwa yakini ambayo hayakubali kutiliwa shaka katika kusihi kwake.

Bali pia kila anaechukia na muongopeaji wa Atarah kudai kwamba hakika kadhia ya kupigwa kwa Zahraa, kutoka kwa mamba yake na

109 Angalia Al Kaafiy (52/5),Tahdhiibul AShkaam(168/6)

kuchomwa kwa nyumba yake ni njama zilizopikwa, zilizofanywa na Abubakri na Omar kwa kushirikiana na mumewe Ali, katika njia ya kummaliza Zahraa(a.s).
Na tuhuma hizi na uzushi wa batili unaweza ukajengeka kwa kuwafikiana na la chuki hiyo juu dalili na ishara anazozitowa toka kwenye kisa chenyewe kilichozushwa, na kitakuwa kikilingana na dai la kuchukia kama ifuatavyo:

1-Imamu amefanya tamthilia ya kina pale alipowafiki kujifuma kwake kwa njia ya Masahaba pale walipoingia kwenye nyumba na kumpiga kwake, ilikuwazuga watu wa nyumba yake kwamba yeye na muhanga wa mkusanyiko na njama hizo kutokana na mtu umri wake uliopita miaka sitini, na mwengine aliezidi miaka hamsini, pamoja na kuelewa kuwa nguvu za imamu Ali hakuna anaeweza kuzikabili miongoni mwa wanaadamu wala majini, kama vile ilivyonukuliwa kutoka kwake kwamba aling'oa lango kuu la Khaibar peke yake wakati watu arobaini hawawezi kuubeba.

2- Imam Ali kutoa kwake udhuru wa kutopambana kwake na Masahaba kwa kwa sababu ya kuhifadhi kwake damu ya waislamu isimwagike kwa hoja zisizokuwa na msingi, kuwa eti Masahaba walikuwa wamertadi baada ya kifo cha Nabii (S.A.W) isipokuwa watatu kulingana na riwaya toka kwa Ahlil Bait!basi jee makusudio ya Imam Ali (a.s) yalikuwa ni kwa damu za watatu hao tu;?!

Na jee damu za Masahaba ni ghali zaidi na takatifu kwake kuliko damu za Zahraa (a.s) ,hiyo haihifadhiwi wala kulindwa?!! Imam Ali kuowa baada ya kifo cha Zahraa mke wa toka kwa bani Hanafiyyah siku tisa tu baada ya kifo chake,na mwanawe akampa laqabu ya ibin hanafiyyah, na tukio hilo hilo kwenda sambamba na kumuozesha Omar bin Khataab mmoja wa wanachama wa njama-Ummu Kulthuum binti ya Zahraa (a.s), ni miongoni mwa yanayojulisha juu ya hamu yake ya kukuza uhusiano na maadui wa mkewe, na kutompenda kwake na kumuenzi Zahraa(a.s).

3-Pale Imam Ali alipokuwa Qadhi na waziri katika kipindi cha Khalifa wa mwanzo na wa pili, hili lilikuwa mfano wa malipo kwa kile alichokisimamia katika kufaniksha njama.

4-Hamu yake ya kuwaita wanawe majina ya Abubakri, Omar na Othman kuowa kizuka wa Abubakri ndani yake imo dalili juu ya hamu yake juu ya kujifakharisha kwake kwa waliyoyafanya zamani na kuendeleleza kwake kazi waliyoifanya lau ingekuwa dhidi ya Zahraa.

5- Imam hakuwapa watoto wa Zahraa mirathi yao toka kwa mama yao katika Fadak pale aliposhika ukhalifa wa waislamu, na akaenda mwenendo wa wenzake Makhalifa waliomtangulia,bali bali hakuzuwia Tarawiih wala kurejesha muta'a.Hivi basi jee kipenzi cha Ahlil Bait kinaweza kunasibisha mtu wa fitina naaswiby mwenye chuki mfano wa tuhuma hizi kwa Masahaba wa Mtume (S.A.W) kwa kumpiga kwao Zahraa na kuchoma moto nyumba yake, na Amiirilmuumina kumwachia mkono kwa kutomnusuru, kwa sababu ya kufungamana kwake na riwaya vya uzushi vilivyo juu yake, wala hana njia ya utoleaji dalili au kufanyia uchunguzi na kubainikiwa na ukweli na haki ambayo inakusanya wa haifarikisha?

Suala la Nane:Msimamo wa Khalid binil Walid kuhusiana na Malik bin Nuwairah na mke wake:

Unasema nini kuhusiana na Abubakri Sidiq kuhusiana na Abubakri,na yaliyotokea mwanzoni mwa ukhalifa wake kutokana na kumpeleka kwake Masahaba chini ya uongozi wa Khalid bin Walid na kuhalalisha kwake damu za waislamu kwa kutokuwa kwao tu na maarifa na kulikoonekana kwenye uzuwiaji wao kutowa zaka kama walivyofanya kwa kaumu ya Malik bin Nuwairah, na kuuliwa kwake na Khalid,na kuingiliwa kwake mkewe Malik na Khalid katika usiku huo huo ?

Jibu :
Kwanza :Zaka ni nguzo muhimu katika nguzo za uislamu baada ya shahada na sala, nayo ni haki ya mafukara, masikini na wengineo toka kwenye mali ya matajiri, na hivyo ndiyo mara nyingi Allah (S.W) akaiambatanisha baina ya sala na zaka kwenye kitabu chake kitukufu kama kwenye kauli yake Taala:**{Na simamisheni sala na mtowe zaka na murukuu pamoja na wanaorukuu}**[Al Baqarah:43]

{Na simamisheni Sala na mutowe Zaka na chochote kile munachokitanguliza kwa ajili ya nafsi zenu katika kheri mutaiona mbela ya Allah Hakiak Allah ni Mwenye kuwa na kuona kwa munayoyafanya } [Al Baqarah:11]

Na kutoka kwa Abi Jaafar (a.s) amesema :"Hakika Allah 'Azza wa Jalla ameambatanisha baina ya Zaka na Sala akasema**{ Na simamisheni Sala na mutowe Zaka}, hivyo anaesimamisha Sala na asitowe Zaka hakusimamisha Zaka"**[110]

Na toka kwa Mohammad bin Muslim, Abi buaswiir, Buraid na na Fadhl wote toka kwa Abi Jaafar na Abi A'bdillah i(a.s) wamesema :"Allah amefaradhisha zaka pamoja na Salaa ."[111]

Hivyo hukumu katika mwenye kuwacha zaka ni kama hukumu ya mwenye kuwacha Sala na kwamba ni kuuliwa.,na hivi ndivyo walivyothibitisha Thaqalani :(Kitabu cha Allah na Maimamu) amesema Taala :**{Hivyo miezi ya H'aram ikipita wauweni washirikina popote munapowaona, wachukuweni, muwazingire na muwawekee kila ulinzi, wakitubu na wakasimamisha sala na kutowa Zaka basi wawachieni hakika Allah ni mwingi wa usamehevu na mwingi wa urehemevu }**
[At tawabah:5]
Na kutoka kwa Abaana bin Taghlib amesema ;amesema Abu Abdillahi:" Damu mbili katika uislamu ni halali toka kwa Allah, yeyote hahukumu kuhusiana nazo ila Allah atatapeleka msimamizi wetu sisi Ahlil Bait hivyo Allah atakapopeleka msimamizi wetu sisi Ahlil Bait ahukumu kwenye damu hizo kwa hukumu ya Allah hataki ushahidi katika mambo mawili hayo mzinifu aliewahi kuowa atamrembea mawe ,na mwenye kuzuwia Zaka atamkata shingo yake "[112]
Na toka kwa Ali bin Ibrahim, toka kwa baba yake, toka kwa Ismail bin Miraar, toka kwa Yunus toka kwa Ibn Miskaan anaisimulia toka kwa Nabii (S.A.W) toka kwa mtu, toka kwa Abii Jaafar (a.s)

110 Al Kaafiy:(503/3),Man lam yahdhw'uruhu l Faqiih: (10/2),Wasaailsh Shiia'a: (22/9).

111 Al Kaafy : : (497/3) Wasailu Shi'ah(13/9)

112 Al Kaafiy:(506/3),Man lam yahdhw'uruhu l Faqiih: (12/2),Wasaailsh Shiia'a: (22/9). 112Al Kaafy(34/1), Bihaarul Anwaar1(64/1),Mustarakuyl Wasaail (25/7).

amesema:”Wakati Mtume (S.A.W) akiwa kwenye msikiti aliposema :”Simama ewe Fulani, simama ewe fulani, simama ewe fulani mpaka wakatoka watu watano akawambia tokeni kwenye msikiti wetu humu, hamsali humu wala nyie hamtowi aka”[113]

Pili : Ni jambo linalojulikana katika mambo yaliyothibitishwa na riwaya za kihistoria walizozisimulia wanazuoni wakubwa kwamba waliortadi wengi wa mabedui baada ya mauti ya Nabii, na baadhi yao wakaacha -kutowa-zaka na mambo mengine.

Ametaja Atuusiy kwenye Aamaaly toka kwa Ibrahim bin Muhaajir, toka kwa Ibraahim,amesema:alirtadi Asha’th bin Qais Ashath bin Qais na watu katika waarabu pale alipokufa Nabii (S.A.W), tunasali wala hatutotowa zaka, hivyo Abubakri akawakatalia., na akasema:” kamwe sitofungua fundo alilolifunga Mtume (S.A.W), wala kupunguza chochote katika vile alivyokuwa Nabii (S.A.W) akichukuwa kutoka kwenu na nitakupigeni vita, hata mutakaponizuwilia kamba aliyokuwa akichukuwa Nabii (S.A.W) toka kwenu nitakupigeni vita,na akasoma **{Na kamwe Muhammad hakuwa ila Mtume na kwa hakika wamepita kabla yake Mitume –wengi -}** [Aal I’mraan:144]

Na kutokana na msimamo huu ndio Abubakri akapeleka majeshi ya waislamu chini ya uongozi wa Khalid bin Walid (r.a) kwa ajili ya kuwapiga vita wenyekurtadi hao, na miongoni mwa aliowaendea Khalid bin Waaliid ni kaumu ya Malik bin Nuwairah[114] , nao walikuwa wamezuwia zaka za mali zao na hawazikutowa kwa Abubakri wala kwa mwenginewe.
Tatu: Waovu na wenye matamanio ya nafsi wengi na fitina waliwamemtia ila Abubakri kwa kumpeleka kwake Khalid bin Walid kwenye vita na mapigano, kwenda kuuwa watu, na kuhalalisha mali zao, kama vile walivyozuwa uongo na uzushi .
Na usahihi ni kwamba Abubakri kamwe hakumpeleka Khalid kuongoza majeshi bali alitanguliwa na Mtume kwa hilo, kwani

113 Al Kaafiy:(503/3),Man lam yahdhw’uruhu l Faqiih: (10/2),Wasaailsh Shiia’a: (22/9), Tahdhiibul ahkaam (111/4).

114 Al Aamaali cha Tw’Tw’uusy (272),Bihaaril Anwaar(11/28)

Nabii (S.A.W) alimpeleka Khalid kuwa kiongozi kwenye vita kadha kwa ajili ya kueneza uislamu, kama vile kumtuma kwake Taif, kwa watu wa Yemen, Uzaa, Bahrain , Dawmatil Jandal na mwenginewe wengi.

Pamoja na jumbe hizo kubwa alizompelekwa Khalid na Nabii (S.A.W) na wenginewe katika Makhalifa, bado tunaona wanaomtia kasoro Sahaba huyo mtukufu kwa kudhihirisha kutetea kwake na kumzushia, kuficha mema yake, kwa lengo la kumpakia matope historia yake na nafasi yake kwa Nabii (S.A.W).

Nne :Allah amesema (S.W) **{Allah ametowa ahadi kwa wale walioamini na kutenda amali njema kwamba atawapa usimamizi kama alivyowapa usimamaizi wale waliokuwa kabala yao , na kuwathibitishia Dini yao aliyowateulia wao na hakika atawabadilishia baada ya woga wao kuwa na amani - kwani wani - wananiabudu mimi na kamwe hawanishirikishi na chochote, na wowote watakaonikufuru basi hao ni waovu }** [An Nuur:55]

Hakika masharti haya matatu yamekamilika kwa Masahaba (r.a) , kupewa usimamizi na kuthibitishiwa dini, kubadilishiwa hofu, na hapa ni pale watu waliportadi baada kifo cha Nabii (S.A.W), Masahaba wakawapiga vita na hapo ndipo amani na utulivu ukapatikana.

Tano : Kisa cha cha Khalid kumuuwa Malik bin Nuwairah, zimekuja riwaya tatu kuhusiana nacho :
Kwanza : Kwamba Khalid bin Walid alimjia Malik bin Nuwairah na kaumu yake, akawambia ipo wapi zaka ya mali ? hivi nyie mna nini mpaka mkatofautisha baina ya Sala na Zaka?
Malik bin Nuwairah akamwambia: Hakika mali tulokuwa tukiitowa kwa sahibu yako katika uhai wake ,amekufa, iweje kwa Abubakri? Khalid bin Walid akaghadhibika ,hivi yeye ni sahiba yetu wala sio sahiba yako?

Hivyo akamuamrisha Dhiraar bin Azwar ampige shingo yake.
Na imesemwa :Hakika Malik bin Nuwairah alifuata nyendo ya waliodai unabii .

Na zipo riwaya tatu nazo ni :Kwamba Khalid bin Walid (r.a) alipozungumza na kaumu ya Malik bin Nuwairah, na kuwakaripia kuhusiana na jambo hili na kumsemesha siri, alimwanbia mmoja wa walinzi wake: (ادفئوا الرجل)Wafunikeni mateka wenu ! nao ulikuwa usiku wa kipupwe na ilikuwa katika lugha ya Thaqiif (ادفئـوا الرجـل) kunamaanisha :wauwe, hivyo mlinzi akadhania kwamba Khalid bin Walid (r.a) anataka kuuwa basi akawauwa kulingana na ufahamu wake bila ya amri ya Khalid bin Walid (r.a).

Basi lau tutakamatana na riwaya yoyote ile katika zilizotangulia , ikiwa ni kosa lililotokea toka kwa Khalid bin Walid (r.a) katika kumuuwa Malik bin Nuwairah, basi udhuru uko pamoja nae kwa njia ya kumuuwa kwake mzuwiaji zaka, au kwa kufuata tenzi za uzushi.au kwamba yeye alikuwa mwenye kufanyia taawili, na taawili hii haipelekei usimamishaji wa H'adi na kisasi juu ya Khalid bin Walid (r.a) Khalid bin Walid (r.a) , kwani ilishatokea mfano wa hili kwa Sahaba Mtukufu Usama bin Zaid (r.a), pale alipofanya taawili kumuuwa yule mtu aliyetamka (لا اله الا الله) na Nabii (S.A.W) kamwe hakumuwajibishia kutowa fidia wala kafara

Amesema Allah **{Enyi muliomini munapo pigana katika njia ya Allah basi tafuteni uhakika na kamwe musimwambie yule anaekutoleeni salamu wewe sio muislamu kwa kutafuta maslahi ya kidunia}** [An Nisaa:94]:"Hakika hii iliteremka pale Mtume (S.A.W) aliporejea toka kwenye vita vya Khaibar,na kumpeleka Usama bin Zaid kwenye upande wa Fadak ili akawalinganie uislamu, nae alikuwa mtu katika mayahudi aliyekuwa akiitwa :Mirdaas bin Nahiik Al Fadaky yuko kwenye baadhi ya vijiji, basi alipohisi –sauti ya- farasi wa Mtume (S.A.W) alikusanya familia na mali yake , na kwendea kwenye upande wa mlima, basi akawa anakwenda huku akisema :"Nashuhudia kwamba hapana Mola apasayekuabudiwa isipokuwa Allah na kwamba Mohammad ni Mjumbe wa Allah,basi akampita Usama bin Zaid akamchoma na kumuuwa, hivyo alivyorejea kwa Mtume (S.A.W) akampa habari juu ya hilo, basi Mtume (S.A.W) akamwambia :(hivi umemuuwa aliyesema nashuhudia kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah na kwamba Mohammad ni Mjumbe wa Allah na mimi ni Mtume akamwambia Ewe Mtume (S.A.W) hakika alilisema hilo kwa kujikinga na

kuuawa! Mtume (S.A.W) akamwambia hivi ulimpasua kifuniko cha moyo wake, alilolisema kwa ulimi wake hukulikubali wala hukufanyia kazi lililokuwa kwenye naf si yake ,basi Usama baada ya hapo akaapa kwamba hatompiga vita yeyote alieshuhudia kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa isipokuwa Allah na kwamba Mohammad ni Mjumbe wa Allah”

Ama kauli kwamba Khalid bin Walid (r.a) alimuuwa Malik bin Nuwairah na akamuowa mkewe usiku huo huo, basi hiyo ni kauli batili isiyotegemezewa riwaya iliyo sahihi, na kamwe haistahiki kupotezea chochote katika wino wa haki, na inatosheleza katika kubainisha kutokuwa na nguvu kwa kauli -hii- kumuuliza yeyote anaetaka insafu na uadilifu, na tunamwambia:

Wapi wewe ulijuwa kwamba Khalid bin Walid (r.a) alimuingilia mke wa Malik bin Nuwairah usiku huo huo alimuuwa mumewe?jee unaweza kuleta isnadi moja iliyo sahihi inayojulisha dai lako hilo ?

Hakika watu wa matamanio ya nafsi na fitina kamwe hawakuwa na kigezo chema kwenye mapenzi yao kwa Masahaba wa Nabii (S.A.W), wala insafu kwa yaliyotokea toka kwao, bali hakika wao hutumia riwaya dhaifu zilizoenea kwenye vitabu, pamoja na kuharibu maana zakena kuzifanyia taawili batili, kama ilivyo hali katika kisa cha ndoa ya Khalid bin Walid (r.a) na mke wa Malik bin Nuwairah, pale walipomfanya Khalid bin Walid (r.a) anafanya pupa la kumuuwa Malik kwa ajili ya kunyang'anya mkewe, huu ni katika uzushi.
Na kauli hii siyo nzito kwa anayetaka kueneza utiaji kasoro na fitina kwa Masahaba wa Nabii (S.A.W). ,bali kila mwenye fitina anaweza kufanyia taawili na kuvigeuza visa, riwaya na historia kulingana na matamanio yake ya uongo ya nafsi yake miongoni mwa uongo na mengineyo, bila ya kurejea kwenye sanadi sahihi zinazowafikiana na usahihi.

Kwa sababu hii tu mustashrikina wameweza kumtukana Nabii (S.A.W) kama alivyotiwa ila Khalid bin Walid (r.a).

Hivyo tutasemaje na kumrudi lau mmoja wa mustashrikina mwenye chuki atasema: hakika Nabii (S.A.W) alimuangalia mke

wa Zaid bin Haritha akiwa anakoga na kumpendeza, na kumuachisha toka kwa mumewe ili amuhalalikie ?

Amesema Ar Ridhw'aa (a.s) :" Hakika Mtume (S.A.W) alikusudia kwenda kwenye nyumba ya Zaid bin Haaritha bin Shurahbil Al Kalbiy katika jambo lake alililokuwa akilitaka ,akamuona mkewe anakoga akamwambia :"Ametakasika aliyekuumba! na kwamba yeye kwa kauli yake hiyo alitaka kumtakasa Muumbaji A'zza wa Jalla, hivyo Allah A'zza wa Jalla akateremsha : **{ Hivyo Mola wenu amekuchagulieni watoto wa kiume na yeye akajifanyia watoto toka kwenye Malaika, hakika nyie munasema maneno makubwa }**[Al Israa:40]

Nabii (S.A.W) akasema : pale alipomuona anakoga : Ametakasika aliyekuumba kutokana na kujifanyia mtoto anayehitajia kujisafisha na kukoga huku,basi Zaid bin Haritha alipoerejea nyumbani kwake mkewe akampa taarifa ya ujio wa Mtume (S.A.W) na kauli yake kwake: "Ametakasika aliyekuumba!" na Zaid bin Haritha hakuelewa makusudio ya kauli yake hiyo, na akadhania kwamba alisema hayo kwa kupendezwa na uzuri wake, hivyo akamjia Nabii (S.A.W) na kumwambia. Mtume wa Allah Hakika mke wangu kuna ubaya kwenye tabia zake ,na mimi nataka nimtaliki ! Nabii (S.A.W) akamwambia : "kuwa naye mkeo, na umuogipe Allah.Na kwamba hakika Allah A'zza wa Jalla alishamjulisha idadi ya wake zake na kwamba mwanamke huyo ni katika wao basi hilo akalificha kwenye nafsi yake na kamwe hakulidhihirisha kwa Zaid na kuhofia watu wasije wakasema :"hakika Mohammad anamwambia aliyemuwacha huru "Hakika mkeo atakuwa ni mke wangu , watu wakamtia aibu kwa jambo hilo , Allah A'zza wa Jalla akateremsha Kauli yake**:{Na kumbuka pale ulipomwambia yule Allah aliyemneemsha }**[Al Ah'zaab :37]

yaani kwa Uislamu **{ Na wewe ukamneemesha}** yaani kwa kumuwacha huru, **{kuwa na mkeo na umche Allah na wewe unaficha kwenye nafsi yako yale amabayo Allah amaeyadhihirisha na unaogopa watu na Allah ndiye nayestahiki kuogopwa zaidi }** {Ahzaab: 37}

hakika Zaid bin Haritha (r.a) alimuwacha na kukaa eda kutokana Zaid; na Allah A'zza wa Jalla akamuozesha Mtume wake Mohammad (S.A.W) na kuteremsha Qur-ankutokana na kadhiya hiyo, Allah A'zza wa Jalla akasema:**{ Basi zaid alipomaliza haja yake kutokana na mwanamke huyo tukakuozesha wewe ili kusije kukawa na makosa juu ya walioamini kwenye wake – waliokuwa kwenye ndoa za - watoto wao wa kulea pale wanapomaliza hamu zao kutokana na wanawake hao ,na hakika jambo la Allah lilikuwa lenye kutendeka}**
[Al Ah'zaab :37][115]

Hivyo kafiri mwenye chuki furaha zake huzidi kwa mfano wa kauli hizi zisizokuwa na vichwa wala miguu, lakini mpenzi wa Allah A'zza wa Jalla, Nabii (S.A.W) na Masahaba zake (r.a) huwatafutia udhuru baada ya udhuru panapotokea toka kwake kile anachodhania kwamba ni kuteleza au kupitiwa na kijikosa chepesi na kuitakidi kwamba kamwe hakuna kikosa wala utelezi kwa Nabii (S.A.W) kutokana na kukingwa kwake kufanya kosa, na hata kutelea huku kukithibiti kwa upande was Sahaba (r.a) kwa riwaya zenye kutgemewa na kukubalika,basi ni wajibu juu yake kutodhihirisha makosa; bali alizamishe kwenye bahari za mema yao,na aipe mgongo, azifumbie macho na kulifumbia masikio; kwani dalili za mapenzi ni msamaha, kutojali na kutupilia mbali mitelezo.
Na ama riwaya zilizo batili, basi ni kama alivyosema Allah :**{Basi ama povu huondokelea mbali }** [Ar Ra'ad:17]

Neno la Mwisho

Huzuni zenye Kupita

Hakika tumeleewa kutokana na dalili za kiakili na za kunukuu kwamba hakika Masahaba wa Nabii (r.a) ndicho kizazi bora kilichowahi kujulikana na jamii yote yote ile ya mwanadamu nao ndio viumbe bora baada ya Mitume na Manabii, na kwamba bora wa karne ilikuwa karne yao, kama alivyosema Allah Taala :**{ Hakika nyie mulikuwa umati bora uliotolewa kwa watu**

115 U'yuunil Akhbaar Ridhwaa (1/203) ,Al Ih'tijaaj : (431/2),Bih'aaril Anwaar : (216/22)

munaamrisha mema na mnakataza maovu na mnamuamini Allah } [Aali I'mraan :110]

Ama kauli ya kurtadi kwao hiyo kamwe haikubaliki muislamu yeyote mwenye akili yake, bali kila muislamu wa kawaida asiyesoma mwenye itikadi salama kubatilisha itikadi hizi zilizopandikizwa kwenye uislamu kwa baadhi tu masuala, yanayoweza kuzungumziwa na nafsi yake bila ya kurejea kwenye Qur-ani wala Sunna, au kwa mtaalamu wa dini, nayo ni kama vile huzuni na fikra zenye kupita kwenye akili yenye kufuata haki inayowafikana na akili yenyekuangaza, hivyo miongoni mwa mawazo hayo ni kusema-kwa mfano -:

Kwanza : Vipi iwe sawa -kiakili - Masahaba wa mwisho wa Mitume na Manabii wawe makafiri wakati wamesifiwa na Allah (S.W) kwenye Kitabu chake Kitukufu, na hivyo Nabii wake Mohammad (S.AW) na watu wa nyumba yake tukufu iliyotoharika ndani na nje yake? [116] Hivyo jee Allah Azza wa Jalla awasifu wanafiki, na walioritadi ?! na kweli Nabii na Ahlil Bait wafanye hivyo?!!

Pili:Hakika mwenye kurtadi ni kwamba hurtadi kwa sababu ya shubha au kwa matamanio ya nafsi, na ni jambo linalojulikana kwamba shubha na matamanio ya nafsi mwanzoni mwa uislamu yalikuwa yenye nguvu na mengi zaidi, kiasi ambapo waislamu wakati huo walikuwa wenye kudhoofishwa, wakati ambapo makafiri walikuwa wametawalia pembe zote za ulimwengu, waislamu walikuwa wakiudhiwa Makkah, walikuwa wakitukanwa na maudhi toka kwa jamaa zao matusiyaliyo mazito nao wakiwa wenye kuvumilia juu ya maudhi yaliyokuwa yakiwafika, wakiwa wenyekushindwa, wenyekutezwa nguvu wakati makafiri wote wakiwa kwenye nguvu moja juu ya uadui wake

Hakika baadhi ya waislamu walihama na kuwacha nyumba na mali zao, wakawacha vyeo na utukufu waliokuwa nao kwenye jamii yao kwa ajili ya kumpenda Allah A'zza wa Jalla Mtume wake (SA.W) .

[116] Angalia (24-48) kwenye kitabu hichi

Haya yote waliyafanya kwa utii, hiari na mapenzi, kwani yule ambaye imani yake imezama mfano wa jabali lililopaa juu katika hali ya udhaifu na utashi, hivyo itakuwaje imani yake baada ya kushinda dalili za uislamu, na kuenea kwa bandera zake?

Na ni jambo gini litakalowapelekea kumuasi Mtume (S.A.W) baadae, huku akielewa wazi kwamba kwenda kinyume na amri zake ni kumkufuru Mola wao, na kurejea toka kwenye dini yake?

Jee inaingiaje akilini Muhajirina na Ansaari wote wamtii Abubakr (r.a) kwenye kumkufuru Allah! na wawache kufuata kauli ya Mtume (S.A.W), na huku wao wametoka kwenye nchi zao wakitafuta fadhila na uradhi wa Allah na kumnusuru Allah na Mtume wake?!

Tatu: Vipi kuwe kwepesi kuwahukumu Masahaba(r.a) kwa kukufuru na kurtadi kwao kwa nafsi iliyosafi, pamoja na kwamba Imam Ali(a.s) nae akiwa ni mtaalamu wa Fiqhi, aliyesimuliwa toka kwake kwamba amesema :"Niulizeni kabla sijakuondokeeni" kamwe hakuwakufurisha wale waliompiga vita katika watu wa ngamia na Swiffiin, kama ambavyo kamwe hakumteka yeyote katika vizazi vyao wala kuzifanya ngawira mali zao, lakini aliwaweka watu kuwa mbali na jambo hilo, na yote haya ni pamoja waliompiga vita basi itakuwaje kwa wale wasiompiga vita kama vile Abubakri, Omar na Othman na wengineo?!

Bali kamwe hakuwahukumu hao kwa hukumu ya waliortadi ,mfano wa alivyowahukmu Abubakr na Masahaba wengine wale Bani H'anifah na mfano wao mingoni mwa waliortadi,nae (a.s) mtaangazaji wake alikuwa akitangaza alikuwa akitangaza siku ya Jamal na kusema:" Kamwe aliyekimbia asifuatwe, wala kukatwakatwa aliyejeruhiwa, utupu usijefichuliwa, wala pazia kuondolewa!".[117]

Kama Imam, Ali (a.s) alivyokuwa akisema kwa wapiganaji wake "Hakika sisi kamwe hatuwapigi vita kwa sababu ya kuwakufurisha, na kamwe hatuwapigi vita kwa sababu ya wao kutukufurisha sisi,

[117] Angalia Mustadrak il Wasaail(52/11), Bihaaril Anwaar,:252/32).

lakini ni kwamba sisi tunajiona tuko kwenye haki na wao wamejiona wako kwenye haki .”[118]

Nne: Vipi Nabii (S.A.W) atuamrishe kukaa kwenye majlisi za watu wema, na atukataze kukaa kwenye majlisi za waovu, na Nabii (S.A.W) –awe –amekaa na Masahaba waliortadi, wanafiki –kama walivyodai !- hivyo basi ewe mwenye akili ni yupi aliyemkosa?! na vipi Allah asimuepushe Nabii wake (S.A.W) kutokana wenyekurtadi hao –kama wanavyodai – katika maisha na baada ya kifo chake?!

Tano : Vipi Nabii (S.A.W) atuamrishe kuwa na ukwe na watu wema na wenye dini, na atukataze kuwaozesha watu wa madhambi makubwa, na makosa mengi, na yeye mwenyewe aende kinyume na na amri hii katika kuwa na ukwe na kundi hilo kama vile Abubakri, Omar, Othman na Abii Sufiyan basi jee Nabii (S.A.W) alikosea kwa kuwa na ukwe na kundi hilo?!

Sita: Kwanini Ahlul Bait wawaite watoto wao kwa majina ya Masahaba wakubwa ,kama vile Abubakri,Omar na Othman ya ni yenye kuhamwa na watukufu wa zama zetu hizi!?

Basi yeyote anaedai kwamba wao ni makafiri wenye kurtadi anapaswa ajuzishe kuitia majina ya Firaun na wengineo, kwa vile jambo hili linalo asili moja na lile, na kufru ni mila moja.
Na sisi tunaelewa fika kwamba hakuna dalili yoyote ile ya kudhihirisha mapenzi kwa Ahlil Bait ila kwa kuchukuwa elimu yao iliyotukuka, pamoja na kufungamana na mwenendo wao uliobarikiwa!

Saba: Vipi tujuzishe laana na matusi juu ya waliokenda kinyume na Imam Ali(a.s) na kumuuwa ,wakati yeye amekana kwa nafsi yake juu ya kundi lake kutukana na laana yao kwa Muawiyah?!
Walaanaji na watukanaji !

Nane: Kwa mujibu wa asomavyo mwenye insafu kwa historia, kamwe hapakuthibiti kwamba Masahaba walieneza fikira batili

[118] Qurbul Isnaad uk.54) , Bihaaril Anwaar (324/32).

kwenye zama za Nabii (S.A.W).au kumuasi pale ilipoanzishwa Dola ya Kiislam na kutilia nguvu nguzo zake?!Bali walikuwa wakipigana jihadi kwa mali na roho zao,baadhi wakafa kwa ajili ya ya jambo hilo ..basi hivi mnafiki hufanya hivi au anajizatiti kwa hifadhi ya nafsi yake, na kutafuta fursa ya kupata hadhi za kidunia!
Tisa: Kombozi na vita vya Kiislam, jee ndani yake hamuna dalili juu ya ukweli na uthabiti wao juu ya mpango wa Nabii (S.A.W) ?

au ni dalili ya Masahaba kuipenda dunia, matamanio ya nafsi na kutowa damu na nafsi kwenye batili?

Kumi:Viongozi wa dola za nyakati hizi huteua watu wenye sifa zifaazo ili wamasaidie katika kuanzisha dola yao.

Hivyo basi inaingiaje akilini kwamba Allah (S.W) ambeze Nabii wake kwa malezi na kumuenzi, akamchagulia – kiholelaholela bila ya kuchunga wala kuakadiria matokeo ya mambo –kundi la wanafiki ili kumsaidia Nabii wake (S.W.A) kueneza dini yake, pamoja kwamba ni Mwisho wa Mitume na Allah awapenguvu kwenye zama za Makhalifa watatu, na wengine kwenye dola za kiislam?!

Kumi na moja: Asiye na elimu yoyote anayo haki ya kuuliza katika kuuliza kuhusiana kadhia muhimu: Iwapo masahaba ni wenye kurtadi waliojivua toka kwenye dini ya Allah..hivyo kwa mujibu wa hali hii ni kwamba kila kilichosimuliwa toka kwao ni batili! kama vile hukumu za Kisheria na mengineyo, kwa hivyo ni sheria ipi iliyosahihi tumuabudiye kwayo Mola wetu?! na vipi tuitegemee Qur-an iliyonukuliwa na watu hao?!

Ewe mpenzi msomaji : Ni wajibu juu yetu kuelewa elimu ya yakini kwamba maadui wa uislamu wameanzisha utiaji kasoro kwenye Masahaba wa Nabii (S.A.W), kwa vile wao ndio walionukuu Qur-an na Sunna kwa Sanadi zilizo mutawatiri toka kwa Nabii (S.A.W) na kamwe haipo dini yoyote ile juu ya uso huu wa Ardhi yenye sanadi mutawatiri zenye kutoshelza kwa kitabu chake Kitakatifu, au suna ya Nabii wake – wakiwa ni watu wa Vitabu vya mbinguni - isispokuwa waislamu ,ambao wanawapenda Masahaba wa Nabii wao (S.A.W) na kuwafanya wandani wao. Hivyo basi Qur-an

Tukufu na Sunna ya Nabii(S.A.W) vilitufikia kwa njia ya Abubakri, Omar, Othman na ndugu zao (r.a) ,na wale wanaowafata kwa wema na kwenda kwenye nyendo na miongozo yao ,na kwa hivi basi inatubainikia kwa uwazi zaidi kwamba mtandao wa chuki wenye kulenga kuvunja dini, kuwaweka mbali waislamu na uislmu wao, na kuwafanya wafuate mila za kiyahudi na kikristo .kama alivyotutahadharisha Mola wetu (S.W) tuwe mbali nao, akatwambia :**{Na kamwe hawatoridhika nawe mayahudi wala manasara (wakristo) mpaka mufuate mila zao }**
[Al Baqarqh:12]

Na mwisho wa dua zetu tunasema yale aliyoyasema Nabii Bwana wetu Muhammad (S.A.W) kwenye dua ya kuondokea kutoka kwenye majlisi :
“Ewe Mola wa Jibril, na Mikail na Israfil, Muumba wa mbingu na ardhi Mjuzi wa yaliyojificha na yenye kuonekana,wewe utahukumu baina ya waja wako katika yale waliyokuwa wakitofautiana, tuongoze kwa yale –watu waliyotofautiana - miongoni mwa haki kwa idhini yako, hakika wewe unamuongoa umtakaye kwenye njia iliyonyooka.”

وصلى الله على نبينا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين